**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Saba – Tarehe 7 Februari, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaye Balozi wa Uingereza, *can you please rise up, thank you very much.*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 84

**Misaada Tuliyopata Wakati wa Njaa**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu ilikumbwa na maafa ya njaa, hali iliyosababisha kupata misaada ya fedha ndani na nje ya nchi:-

(a) Je, Serikali inaweza kutoa takwimu za misaada hiyo?

(b) Je, ni nchi gani iliyokuwa ya kwanza kutoa msaada?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI** alijibu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuitikia wito wa Serikali wahisani wa nje, Asasi mbalimbali na watu binafsi waliotoa misaada mbalimbali zikiwemo fedha, vyakula na vitu vingine. Hadi kufikia tarehe 30 Desemba, 2006, wahisani wa nje walitoa jumla ya fedha kiasi cha sh.16,662,334,793.22 na vyakula kiasi cha tani 130.75. Aidha, asasi binafsi wa hapa nchini wametoa jumla ya fedha kiasi cha Sh.5,241,400,177 na vyakula tani 5,485.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lililotolewa na Serikali kwa mashirika na wahisani wa nje, lililenga kwenye msaada wa tani 100,000 za chakula, tani 3,434 za mbegu na fedha za kununulia dawa za kuulia viwavijeshi.

Katika kutoa misaada yao baadhi ya wahisani walitoa michango yao kupitia Shirika la Chakula na Kilimo Duniani *(FAO)* kwa ajili ya kununulia mbegu na dawa za kuulia viwavijeshi, na wengine kupitia Shirika la Chakula Duniani *(WFP)* kwa ajili ya kununua na kusambaza chakula. Aidha, baadhi ya wahisani walitoa michango yao moja kwa moja kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli kuwa misaada hiyo toka kwa wahisani wa nje ilikuwa inaratibiwa na makundi matatu tofauti, inakuwa vigumu kwa Serikali kujua hasa ni nchi gani iliyokuwa ya kwanza kutoa msaada kwa ujumla misaada yote ilitolewa kwa wakati muafaka na ilitumika kuwasaidia walengwa kama ilivyokusudiwa.

**MHE. SULEIMAN MOSSY MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza, kwa kuwa nchi yetu ina upungufu mkubwa wa maghala ya chakula. Je, Serikali ina mpango gani wa ujenzi wa maghala hayo angalau kuanzia kwa ile mikoa inayozalisha chakula kwa wingi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya Serikali ya kujitoa kwenye shughuli za uzalishaji umeathiri pia shughuli za ujenzi wa maghala, kwa sasa wawekezaji katika uzalishaji ndio wamepewa jukumu la kuandaa mahali pa kuhifadhi mazao au bidhaa zao na kutafuta masoko.

Serikali inatoa sera miongozo na kusaidia upatikanaji wa maeneo yanapohitajika na sio kujenga, kwa kuanzia endapo uzalishaji utaongezeka katika mkoa unaohusika, maghala ya *SGR* yaliyopo jirani na mkoa huo yatatumika wakati Serikali ikitafuta ufumbuzi. Kwa sasa Serikali inajumla ya maghala 30.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa sababu kampeni hii ya kuomba msaada wa fedha ndani na nje ya nchi kwa ajili maafa ya chakula haikutupa utatuzi wa tatizo hili la kudumu.

Je, Serikali haioni kwamba labda kampeni ambayo ingekuwa nzuri zaidi ya Waziri Mkuu na Rais kufanya ni kuomba msaada kama uleule lakini wa kuweza kupata fedha kununua miundombinu ya kuweza kutoa mazao ambayo yanakwama kule Sumbawanga, Ruvuma na Mbeya ili tuweze kutatua tatizo la njaa kwa njia ya kudumu kuliko kuomba kila mwaka ambavyo nategemea Waziri Mkuu ataomba miaka mingine ijayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wake wa maendeleo wa miaka mitano, Serikali imeweka bayana kipaumbele cha kuboresha miundombinu

katika nchi hii ili kuweza kuwafikia wazalishaji wa mazao sehemu mbalimbali na hivyo kuwarahisishia usafirishaji wa mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa mpaka sasa tunategemea misaada toka nje, lakini pia na sisi tuna malengo ya muda mrefu ili kuweza kuboresha miundombinu ilituweze kufanikiwa bila kuwategemea wafadhili wa nchi.

Na. 85

**Ubovu wa Barabara ya Lawate – Kashahi**

**MHE. AGGREY MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu barabara itokayo kijiji cha Lawate kwenda kijiji cha Kashashi Wilayani Siha imekuwa na hali mbaya sana, hali inayoleta usumbufu kwa wananchi hasa nyakati za mvua; na kwa kuwa, barabara hiyo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi katika kusafirisha mazao mbalimbali kama kahawa, ndizi na mahindi.

Je, Seikali haioni umuhimu wa kusaidia ujenzi wa barabara hiyo angalau kwa kiwango cha moramu hasa ikizingatiwa kuwa hali ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai kifedha si ya kuridhisha na hivyo kushindwa kuihudumia barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri Mbunge wa Siha kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambayo Mbheshimiwa Mbunge anizungumzia ina urefu wa Km. 7.3 na ipo chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai. Barabara hii inahudumia vijiji vya Lawate, Kashahi na Lukani. Kijamii barabara hii ni muhimu kwa kuwa inahudumia Taasisi mbalimbali zikiwemo shule za msingi na zahanati. Kiuchumi barabara inatumika kwa kusafirisha mazao ya biashara na chakula yakiwemo mahindi, maharage, ndizi na kahawa. Hivyo Serikali kupitia Halmashauri ya Hai inafahamu umuhimu wa barabara hii lakini tatizo kubwa ni ufinyu fedha ambazo zinapatikana kutoka katika Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Halmashauri ya Hai haina mapato makubwa ambayo yanaweza kutosheleza kuhudumia barabara zake kwa kiwango hicho. Hata hivyo, kwa sababu ya umuhimu unaonekana, Halmashauri ilikuwa ikifanyia matengenezo barabara hiyo kila mwaka ili kuhakikisha kuwa inapitika kama ifuatavyo:-

- Mwaka 2003/2004 matengenezo yenye gharama ya shilingi 3.42 milioni, fedha zilitumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo na, mwaka 2004/2005 shilingi 3.0 milioni zilitumika,

- Mwaka 2005/2006 matengenezo ya daraja la Mtukuro yalifanyika kwa gharama ya shilingi 3.0 milioni. Fedha hizi zote zimetokana na Mfuko wa Barabara. Aidha,

kwa mwaka 2006/2007, shilingi 15.2 milioni zimetumika kujenga daraja la Losavana ambalo ni kiungo muhimu kwa barabara ya Lawate hadi Kashashi na vijiji vya jirani pia katika soko la Lawate. Fedha hizo zimetokana na Mfuko wa Maendeleo wa Serikali za Mitaa *(LGCD).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007/2008 barabara hiyo imetengewa Sh.7.3 milioni na wananchi wa maeneo hayo watashirikishwa ili kufanya matengenezo sehemu korofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Hai imeshauriwa kuandaa maombi maalum ya matengenezo ya barabara hiyo kwa kiwango cha Changarawe kama mradi wa maendeleo na kuyawasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili yaweze kufikiriwa pindi hali ya fedha itakapokuwa nzuri.

**MHE. AGGREY MWANRI:** Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa hapa. Kwa kuwa, hali ya barabara hii ninayoizungumzia ya kutoka Lawate kwenda Kashashi, na kwenda mpaka Lukali, sasa hivi iko katika hali mbaya sana na kwa kuwa wananchi wanaitegemea sana barabara hii kama mwenyewe Naibu Waziri alivyozungumza hapa. Je, ni hatua gani za kidharura ambazo zinaweza zikachukuliwa sasa kwa sababu barabara hii imekatika natambua kuwa mvua zimekuwa zinanyesha nchi zima, ili kuondokana na hilo tatizo?

Kwa kuwa sasa tunategemea sasa Halmashauri ya Wilaya ya Hai itakuwa imeandaa huo utaratibu wa kuweka Bajeti kwa ajili ya hiyo shughuli, ningetaka kujua ni lini sasa tunategemea kwamba tutafanya kazi hiyo tunangoja mpaka Bajeti mpya hii inayokuja au kutakuwa na utaratibu wa sasa hivi wa kufanya kazi hiyo? Pamoja na hilo nataka kujua, je, ule utaratibu wa stabex ambao umekuwa unasaidia masuala haya ya barabara ambao wamelima kahawa unawezaje ukasaidia tatizo hili ambalo nalizungumza hivi kwa sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama nilivyokiri kwenye jibu langu la msingi kwamba barabara hii ni muhimu kwa kiuchumi na kijamii, hatua ambazo tumedhamiria kuchukua ni pamoja na kuwaomba wenzetu wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai waombe *special request* katika ofisi yetu ili wawe *considered.*

Pia mipango ya muda mrefu ni kuhakikisha kwamba wanapanga Bajeti ya kila mwaka kuhakikisha kwamba barabara hii inakuwa *maintain,* na kuhusu mpango wa *stabex* suala hili litaangaliwa zaidi na Serikali.

Na. 86

**Kupunguza Adha kwa Walimu Kufuata Mishahara**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo Kijiografia ina Tarafa ya Sasawala ambayo ina Kata za Lusewa na Magazini zilizo zaidi ya km. 220; na kwa kuwa walimu wa sehemu hizo husafiri kwa kutumia siku zisizopungua 5 kufuata mishahara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa walimu walio pembezoni kwa kuwapunguzia adha hiyo ili wafanye kazi zao kiufanisi bila kupoteza siku za kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa Halmashauri wakiwemo walimu walikuwa wanapelekewa mishahara na kulipwa katika Kata au Tarafa kulingana na mazingira ya Halmashauri husika. Kazi hii ilifanyika na kuonekana kuwepo matatizo kadhaa ya utekelezaji. Matatizo yaliyobainishwa ni pamoja na gharama za kulipa posho za wasindikizaji na walipaji, usalama mdogo wa fedha na watumishi na uhaba wa vitendea kazi kama magari na mafuta. Baadhi ya Halmashauri ili uweze kuwalipa watumishi wote ilikuwa inachukua zaidi ya wiki moja kukamilisha mzunguko kwa kuwa na kata nyingi ambazo ziko tofauti kulingana na jiografia yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha imewataka watumishi wake wote wa Umma wakiwemo walimu kufungua akaunti katika benki ambayo mtumishi anaihitaji ili mshahara wake upitishiwe huko. Kwa kupitishia mshahara benki kila mtumishi anajipangia muda wake na siku yake kwenda benki kuchukua mshahara. Aidha, utaratibu huu umepunguza wimbi la upotevu wa mishahara ya watumishi ambalo lilijitokeza wakati mishahara ikipelekwa katika ngazi ya Kata na vilevile imepunguza gharama nyingine za usambazaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya makubaliano na Benki ya *NMB* na kuweka utaratibu unaowezesha ulipaji wa mishahara ya walimu na watumishi wengine kila ifikapo tarehe 25 ya kila mwezi. Katika utaratibu huu Halmashauri hazitafuata tena Orodha ya kulipa mishahara Hazina bali (*Payroll*) kila ifikapo tarehe 15 Halmashauri zitachukua vifurushi (*Payrolls*) vya mishahara katika Hazina ndogo zilizopo katika kanda zao. Utaratibu huu utarahisisha upatikanaji wa mishahara na itapatikana kwa wakati. Hii itasaidia kupunguza usumbufu uliokuwa unajitokeza kwa walimu kusubiri mishahara yao kwa muda mrefu.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kwanza kabisa naomba niipongeze Serikali kwa hatua nzuri iliyochukua ya maana kabisa ya kuhakikisha mishahara ya walimu na watumishi wa Serikali wanapata mishahara yao kabla ya tarehe 25 na imewezekana.

Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza, kwa kuwa, tatizo la walimu walioko pembezoni linatokana na huduma za kibenki kuwa mbali, lakini hivi sasa kuna Benki Kata au *SACCOS* ambazo zinatoa huduma za kibenki na walimu ni wanachama wake.

Je, Serikali inaweza kutumia busara yake ya kushawishi benki *NMB* kuwa na *link* na benki Kata hizo ili walimu na watumishi wa Serikali walio mbali waweze kupata huduma hizo huko huko katika kata zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Kwa sasa hivi *NMB* imeziagiza Halmashauri kwamba wa-*identify* sehemu zile za kata ambazo ziko pembezoni kuangalia ni sehemu gani ambazo zinafaa kuwa vituo vya malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Kwa hiyo, kwa sasa hivi wakurugenzi wote walioko katika wilaya za pembezoni, wamelitimiza agizo hilo wameshaanza kuahinisha sehemu ambazo ziko pembezoni kwa hiyo *NMB* haijashindwa kulipa sehemu zile ambazo ziko pembezoni. Iliyoko ni kwamba tumeshakubaliana kwamba sehemu hizo zilizoko pembezoni Halmashauri husika zita-*identify NMB* itachukua siku moja au mbili kwenda kulipa sehemu hizo ambazo ziko pembezoni.

Kuhusu kutumia Benki Kata, suala hili bado hatujalifikiria na naomba nilipokee ili tulifanyie kazi. (*Makofi*)

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililoko Namtumbo, linafanana kabisa na tatizo lililoko katika jimbo la Msanda ambalo walimu husafiri sana kutoka mbali kwa mfano Bukondo, Kaseme, kufuata mishahara na karibu wote wanapokwenda inabidi walale Makao Makuu ya Wilaya. Sasa, matokeo ni kwamba unakuta sehemu kubwa ya mshahara wao inatumika kwenye usafiri. Je, Serikali haioni kwamba ni vizuri walimu kama hao wakaweka angalau *flate rate* ya nauli au *night* moja kwa sababu wanakuwa wanaenda kikazi ikaingia kwenye mshahara wao ili waweze kupunguza makali ya maisha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa naibu Spika, nafikiri katika jibu langu la pili nimeeleza wazi kwamba sasa hivi kwenye sehemu hizo ambazo ziko pembezo Wakurugenzi wameagizwa kwamba wa-*identify* sehemu kama hizo. Kwa hiyo, ina maana kwamba baada ya muda sehemu hizo ambazo ziko pembezoni, *NMB* watakwenda kulipa mishahara moja kwa moja katika vituo husika ambavyo vitakuwa vimeshaainishwa na Halmashauri husika. Na kwa zile wilaya mpya ambazo hazina matawi ya *NMB* kwa sasa Halmashauri ina mpango wa kuwalipia katika *Headquarter* ya Halmashauri lakini hapo hapo wameshaambiwa kwamba watajenga benki za *NMB* katika sehemu hizo. Kwa hiyo, *NMB* hili suala wamelichukua *serious* na Serikali imelichukulia *serious* kwa kuona kwamba wafanyakazi wetu wanazunguka muda mrefu katika kutafuta mishahara yao. Kuhusu suala la posho ya *flate rate* naomba nilichukue kama lilivyo ili lifanyiwe kazi.

**MHE. ELIZABETH M. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kila mtumishi anapaswa kupata mshahara wake ukiwa umekamilika, lakini hawa watumishi wanaotoka katika vijiji vya mbali, kata ambazo ziko mbali sana na makao makuu ya benki wanapaswa kutumia mishahara yao kama nauli, wanatumia mishahara kama posho. Lakini alivyojibu yaelekea yote ni mipango ya muda mrefu sana, kwa sababu benki kuja kujengwa huko vijijini ni muda mrefu sana, lakini hakuna njia ya haraka ya kuweza kuwasaidia watumishi hawa wanaotoka Kata za mbali kama vile Ngenge, Mrusagamba, Mrongo na nyinginezo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, njia ya haraka ambayo

tumeifanya ndiyo hiyo niliyowaeleza kwamba Mkutano wa Wakurugenzi wote pamoja na *NMB* na Hazina ulikaa mwezi wa kumi na mbili. Nafikiri Wabunge wote ni mashahidi kwamba mwezi huu uliopita karibuni watumishi wengi wamelipwa mshahara tarehe 25. Hiyo ni hatua moja. Kwa hiyo, kwenye Mkutano huu ndiyo ulioagiza Wakurugenzi kwamba waka-*identify* sehemu ambazo ziko pembezoni si Wilaya zote ambazo ziko pembezoni na sio Kata zote. Wakisha *identify* hizo sehemu *NMB* itakuwa inachukua siku mbili au tatu kwenda kulipa mishahara katika sehemu hizo. Kwa hiyo tatizo la watumishi kuzunguka kufuata mishahara halitakuwepo tena. Hiyo ndiyo njia ya haraka ambayo Serikili imeichukua. Hizo *long term plan* ndiyo kwa Wilaya zile ambazo hazina matawi ya *NMB*, ndiyo *NMB* wamekubali kwamba watajenga Halmashauri kama Ruangwa. Kwa hiyo, kwa sasa hivi mishahara inalipwa chini ya uongozi wa *NMB* pale pale *Head quarter* ya Halmashauri na wameshawaagiza wa *identify* sehemu zile ambazo ziko pembezoni. Naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira mambo ya mishahara ya Wafanyakazi inaangaliwa vizuri na tunatekeleza vizuri kwa haraka iwezekanavyo.

Na. 87

**Mashamba ya Serikali Yaliyo West Kilimanjaro**

**MHE. ELISA D. MOLLEL** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna mashamba ya Serikali yaliyokuwa chini ya *NAFCO*, huko *West Kilimanjaro* ambayo hayatumiki kwa muda mrefu sasa; na kwa kuwa, kuna wananchi wengi waliyoyazunguka mashamba hayo na wana shida ya ardhi. Je, Serikali haioni kuwa ni uamuzi wa busara kuwapa wananchi hao mashamba hayo kwa taratibu zilizopo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Elisa David Mollel, Mbunge wa Arumeru Mashariki, napenda nitoe maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mashamba ya *West* Kilimanjaro ikiwa ni pamoja na mashamba mengine ya *NAFCO* yako chini ya *PSRC specified* kwa ajili ya ubinafsishaji. Aidha, katika mchakato wa ubinafsishaji wa mashamba ya *NAFCO* Serikali inatumia njia mbalimbali ambazo zinatofautiana kwa kila shamba. Baada ya maelezo hayo mafupi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mollel, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Ili kuwezesha mashamba ya Kanamondo, *Harlington*, *Fosters*, Matadi na *Journey's End* kubinafsishwa, Serikali kupitia *PSRC* iliamua kuyapima kwa nia ya kuelewa ukubwa wake hasa ukizingatia kuwa yalikuwa yamevamiwa na baadhi ya watu kujenga makazi ya kudumu. Upimaji huo uliiwezesha Serikali kujua ukubwa wa maeneo yaliyobaki kabla ya kutangaza ubinafsishaji. Aidha, shamba la *Fresian* liliondolewa katika utaratibu wa ubinafsishaji, kwa vile ni mali ya Kampuni ya Bia. Shamba la *Rosylin* lenye ukubwa wa ekari 2000 limegawanywa kwa baadhi ya wananchi waliokuwa wamevamia msitu wa Mlima Kilimanjaro. Shamba la Matadi kwa upande mwingine limepata mwekezaji, ambae amelipia nusu ya gharama zinazotakiwa kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa ubinafsishaji wa mashamba ya Kanamondo, *Harlington*, *Fosters* na *Journey's* yenye jumla ya ekali 5935 unaendelea.Kuhusu hoja ya kugawa mashamba haya kwa wananchi imedhihirika kuwa zoezi hilo haliwezekani hasa ukizingatia kwamba idadi ya watu wanaoishi ndani ya msitu wa Kilimanjaro wanaokadiriwa kuwa zaidi ya 12,000, hawataweza kutoshelezwa na ekari 5,935 zilizopo, kuwawezesha kujitegemea kiuchumi. Kwa vile kuna uhaba mkubwa wa ardhi katika eneo hilo. Dawa siyo kugawana ardhi kidogo kidogo, bali ni busara kwa wananchi wasiokuwa na ardhi katika maeneo hayo kutafuta ardhi katika sehemu nyingine ya nchini.

Na. 88

**Uuzaji wa Mazao ya Wakulima**

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali za Awamu zote zina dhamira kamili ya kutaka kuondoa umaskini katika nchi yetu; na kwa kuwa njia mojawapo ya kuondoa umaskini ni pamoja na mkulima kuuza mazao yake, hasa mazao ya biashara kama Korosho na Kahawa.

(a) Je, Serikali ina imani gani na utaratibu wa sasa wa kuwaacha wafanyabiashara waendelee kununua mazao hayo ambao mara nyingi wangependa kununua kwa bei ya chini ili wapate faida zaidi na kuwaacha wakulima wakiendelea kuwa maskini?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kutazama utaratibu wa uuzaji wa mazao ya biashara ili mkulima awe na matumaini kuwa akiuza mazao yake ataondoa umaskini?

(c) Je, Serikali sasa itawadhibiti hao wafanyabiashara wanaojenga kiburi na kujiona kuwa wako juu ya sheria?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a) (b) na (c), naomba kutoka maelezo yafuatayo:-

Kuanzia mwaka 1980 Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta ndogo ya mazao nchini imekuwa ikitekeleza sera zilizolenga kujitoa katika shughuli za uzalishaji, ununuzi na uuzaji wa mazao ya kilimo. Mashirika na taasisi za Serikali zilizokuwa zinafanya shughuli hizo katika sekta ya kilimo, yamebinafsishwa. Aidha, mamlaka za mazao, zilizokuwa zikizalisha na kuuza mazao sasa zinawajibika kusimamia sera, sheria, kanuni na uendelezaji wa mazao *(crop promotion).*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Kumchaya, kama ifuatavyo:-

(a) Sera ya Serikali kuhusiana na ununuzi wa mazao, ni kuruhusu wanunuzi mbalimbali kushiriki katika ununuzi wa mazao ya wakulima na kwa njia ya ushindani. Utakaowapatia wakulima bei nzuri ya mazao hayo.. Wafanyabiashara ni sehemu ya soko la mazao ya wakulima wetu.

Kinachotakiwa katika kutekeleza sera hii, ni kuhakikisha kunakuwepo na ushindani wa kweli na wa haki utakaotoa manufaa kwa pande zote mbili kwa maana ya wakulima na wafanyabiashara, na si upande mmoja kudhulumu upande mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ambalo limejitokeza hivi karibuni ni la wanunuzi wa korosho kushirikiana badala ya kushindana. Ushirikiano ambao umeashiria kuwepo kwa bei ya chini ambao haumlipi mkulima bei yenye motisha.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifuatilia kwa makini hali ya uuzaji wa mazao ya biashara nchini pamoja na mazao mengine. Aidha, Serikali itaendelea kurahisisha kazi na mujukumu ya taasisi zinazosimamia mazao ya kilimo zikiwemo Bodi za Mazao na Vyama vya Ushirika. Kama sehemu ya urahisishaji huo, kuanzia mwezi Julai, 2006 Serikali imesimamisha utozaji wa kodi kwa wakulima kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mazao na hivi sasa Serikali inagharamia Bodi hizo kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Wakati huo huo Serikali inatekeleza Mpango Kabambe wa Kuimarisha Vyama vya Ushirika nchini, ili kuwa na Vyama imara vinavyowajibika kwa wanachama na kuwa na uwezo wa kuwahudumia kwa ufanisi zaidi kuliko ilivyo sasa. Kwa kweli Vyama vya Ushirika vinavyofanya kazi kwa uaminifu kwa wanachama wao ndiyo jibu la matatizo wanayopata wakulima hivi sasa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina wajibu wa msingi wa kusimamia sheria kanuni na taratibu za uuzaji na ununuzi wa mazao ya kilimo. Kama mfanyabiashara au Chama cha Ushirika kinachojihusisha na ununuzi wa mazao kitakwenda kinyume na sheria na taratibu zilizopo, Serikali haitasita kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mhusika; kwa mfano hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na wafanyabiashara waliokuwa wanakwamisha ununuzi wa zao la korosho katika mwezi wa Desemba 2006, ni pamoja na kufutiwa leseni zao za ununuzi wa korosho na hii ni kwa wanunuzi ambao hawakufuata agizo la Serikali. Huu ni uthibitisho kwamba Serikali haitawavumilia wafanyabiashara ambao lengo lao ni kuwagandamiza wakulima. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

La kwanza, kwa kuwa hivi karibuni Serikali ilitaka kuwanusuru wakulima wa zao la korosho kwa kukidhamini kiwanda cha *BUCO* kununua korosho hizo. Lakini kinyume chake kiwanda hicho kiliamua kuwataka wakulima wakauzie korosho zao pale pale kiwandani na kwa kufanya hivyo walijichomoza wafanyabiashara wababaishaji waliokuwa wananunua korosho vijijini kwa bei ya chini na kuja kuuza kwa bei juu hapo kiwandani. Je, Serikali inaeleza nini juu ya suala hili? *(Makofi)*

La pili, kwa kuwa Serikali inazungumzia juu ya kuimarisha Vyama vya Msingi ili vije kufanya kazi ya kununua zao la korosho; na kwa kuwa Vyama hivi huko nyuma tulikotoka vilikuwa na matatizo. Kwa hiyo, uwezekano wa Vyama hivi kufanya kazi haraka ni ndogo sana. Je, Serikali inasema nini katika msimu ujao wa ununuzi wa zao la korosho ili wakulima wa zao la korosho wasitokewe tena na tatizo hilo la kununuliwa korosho kwa bei ya chini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** kwanza ni kweli kwamba kumekuwepo na matatizo katika ununuzi wa zao la korosho. Lakini ni kweli vilevile kwamba Serikali imejihusisha kikamilifu sana katika kushughulikia matatizo ya ununuzi wa korosho.

Kuhusu suala la Kiwanda cha *BUCO* kusema watu lazima wapeleke mazao yao pale pale Kiwandani ilitokana na upungufu wa fedha iliyokuwa nayo *BUCO* kabla hawajapewa *guarantee* na Benki Kuu. Walikuwa na fedha kidogo shilingi milioni 300 ambazo kwa ununuzi wa korosho ni fedha kidogo sana. Ndiyo maana *BUCO* walifikiri itakuwa ni busara wakinunua korosho pale pale Kiwandani kuliko kusambaza fedha kidogo waliyokuwa nayo katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshauriana na *BUCO* nilipokutana nao Masasi hivi karibuni wakati natoka katika safari yangu ya Tunduru na tukakubaliana nao kwamba wakati fedha zitakapopatikana baada ya *guarantee* ya Benki Kuu watasambaza fedha zile na kununua korosho katika maeneo ya vijijini badala ya kusubiri kuletewa kiwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahia kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Benki Kuu sasa imetoa *guarantee* na Kiwanda cha *BUCO* kinazo fedha na kupitia Bunge hili tunaiagiza *BUCO* iweke utaratibu mzuri wa kununua korosho zote zilizobakia katika Mikoa ya Lindi na Mtwara*.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuimarisha Vyama vya Ushirika jibu la msingi linasema ndiyo njia ya pekee na sisi tunadhani kwamba ni sahihi. Kwamba mazao haya ni ya wakulima na kule ambavyo Vyama vya Ushirika vinafanya kazi vizuri pamoja na kwamba kuna wanunuzi binafsi lakini ushindani unawapa bei nzuri wakulima.

Katika Mkoa wa Kilimanjaro kwa mfano ambako kuna zao la kahawa na kuna Vyama vya Ushirika vinavyofanya kazi mpaka sasa bei ya kahawa anayopewa mkulima ni nzuri na ushindani ni wa uhakika. Kwa hiyo, ushauri wa Serikali kwa Vyama vya Ushirika vya Korosho ni kwamba kati ya sasa na msimu unaokuja Vyama hivi vijiimarishe vikopesheke, viweke viongozi wazuri na watendaji wazuri ili zao la korosho liendeshwe kwa ufanisi kama linavyoendeshwa zao la kahawa. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wafanyabiashara wamekuwa sasa wakiwafuata wakulima mashambani na kununua hususan zao la kahawa likiwa bado halijakomaa yaani liko shambani wananunua kwa wakulima na kwa kufanya hivyo na kwa kuzingatia pia

kwamba wakulima wetu hali yao ya kiuchumi wengi siyo nzuri, hulazimika kuuza kahawa yao hivyo hivyo ikiwa shambani kwa kweli kwa bei ndogo sana.

Sasa je, Serikali inawaeleza nini wananchi hao na ina mpango gani wa kutunga angalau sheria ya kuwadhibiti hao wafanyabiashara ambao wanaenda kununua mazao yakiwa shambani ili waweze kuacha kufanya hivyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza si busara nzuri kwa wafanyabiashara kwenda kununua mazao yale yakiwa bado shambani. Kwa hiyo, natoa wito kwa wakulima wawakatalie wale wafanyabiashara wanaoenda kununua mazao mashambani moja kwa moja bali watumie taratibu ambazo zipo.

Kwa mfano, kuna Vyama vya Ushirika ambavyo vinachukua yale mazao wanayapeleka kwenye Vyama Vikuu vya Ushirika kwa ajili ya mnada katika zao hilo la kahawa. Lakini pia kuna wafanyabiashara binafsi ambao wanakuja wananunua kwenye *centres* zile za vijiji kwa ajili ya kupeleka kwenye mnada. Lakini pia kuna *Organization* inaitwa *Kill Coffee* ambayo pia inachukua kahawa iliyo bora na kuuza nje moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara ambao wanakwenda kwenye mashamba na kununua kwa bei rahisi kusema kweli wakulima wawakatalie moja kwa moja kwa sababu wakulima hao hao wanaelewa kwamba kuna Vyama vya Ushirika. Zao la kahawa halijapata matatizo sana na wanaelewa kabisa wapo wanunuzi ambao wana leseni kwa ajili ya kupeleka kwenye minada. Kwa hiyo, natoa wito na ninarudia tena tusaidiane kuwaelimisha wakulima wasiweza kuuza mazao yako yakiwa bado shambani ambapo ni bei ndogo zaidi.

Na. 89

**Malezi ya Watoto ambao Mama zao wanatumikia Vifungo**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa ni dhahiri kuwa katika maisha ya kawaida, mwanadamu anaweza akakumbwa na mikasa mbalimbali na tuhuma za jinai au madai ambapo watuhumiwa hupewa adhabu mbalimbali kulingana na uzito wa kosa lenyewe; na kwa kuwa baadhi ya wanawake wanaotuhumiwa na hatimaye kufungwa huwa wajawazito na hatimaye hujifungua wakiwa jela; na kwa kuwa wanawake wengine huhukumiwa vifungo hali wanatunza watoto wachanga:-

(a) Je, Serikali inasemaje kuhusu malezi ya watoto hao wachanga ambao mama zao wanatumikia vifungo katika magereza?

(b) Je, Serikali haioni kwamba watoto hao kuendelea kuishi na mama zao wakiwa jela ni kutokuwatendea haki kwa kuwafanya kutumikia jela hali hawana makosa?

(c) Je, kwa nini Serikali haiandai utaratibu kwa akinamama hao kutumikia adhabu zao kwa kifungo cha nje ili watoto wao wapate malezi bora?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba wapo baadhi ya wahalifu wanawake wanaohukumiwa adhabu za vifungo magerezani wakiwa na watoto wachanga au wakiwa ni wajawazito na hivyo kufanya kuwepo watoto wachanga wanaoishi na mama zao magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafungwa wa kike walio na watoto wachanga magerezani hupewa maeneo maalum katika magereza ya wanawake ili waweze kuwahudumia watoto wao. Serikali ndiyo inayotoa huduma zote muhimu kwa watoto hao na mama zao.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa malezi ya watoto hao nje ya magereza, baada ya kumalizika kwa kipindi cha kunyonyesha (*lactation period*) ndugu za wafungwa hushauriwa kuwachukua watoto hao. Hata hivyo, iwapo ndugu hawapatikani au hawataki, watoto hao hulazimika kuendelea kubaki na mama zao gerezani hadi itakapopatikana asasi inayoweza kuwachukua hususan asasi ambazo hujishughulisha na malezi ya watoto wadogo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali, watoto wadogo wanapokuwa na mama zao magerezani hulelewa na kutunzwa kama ilivyo uraiani na Serikali hugharamia mahitaji yao yote muhimu, ili mtoto husika aweze kupata malezi bora na mama yake hupewa muda wa kutosha kumtunza mtoto wake kwa kumtenga katika mabweni maalumu kwa ajili ya huduma za mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wafungwa wanawake wanaoishi na watoto wao wadogo magerezani kuwekewa utaratibu wa kutumikia adhabu zao nje ya kuta za magereza, suala hili hutegemea kosa lililomtia hatiani mfungwa mhusika na kifungo anachotumikia. Lakini kila inapowezekana wafungwa wenye watoto wachanga ambao hawakupewa msamaha na Rais kwa vipengele vingine, ufikiriwa kuachiwa kwa kigezo cha kuwa na mtoto mchanga.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

(a) Kwa kuwa mtu anapofungwa huwa anatakiwa kurekebisha tabia yake; na kwa kuwa mtu anapokuwa gerezani hufanya kazi za kuzalisha mali kwa ajili ya Taifa. Je, akinamama hao kulingana na makosa yao kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, wanapokuwa nje ya kingo za gereza watoto wao huwa wanalelewa na nani wakati huo?

(b) Kwa kuwa katika magereza hayo kuna msongamano mkubwa wa wafungwa na pia kuna magonjwa ya maambukizi. Je, Serikali inawakinga vipi watoto hao na

magonjwa hayo ya maambukizi kwa sababu tayari wamechanganywa pamoja akinamama mbalimbali na watoto wao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi wafungwa ambao ni wajawazito au wale ambao wana watoto wametengewa maeneo maalum kwa ajili ya kukaa na hawakai katika maeneo na wenzao. Ina maana kwamba suala la kuweza kupata magonjwa ya maambukizi kutokana na wafungwa wengine halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nani anawatunza hao watoto pale ambapo mama zao wanatumikia vifungo nje ya gereza. Hapa tumeishasema kwamba wanatumikia vifungo vyao nje ya gereza. Hawa ni watu ambao wako katika majumba yao wanaenda wanatumikia vifungo vyao nje ya magereza na wanatunzwa na ndugu zao na familia zao kama inavyopaswa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maelezo ya ziada kwa maelezo mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri. Kama maana ya Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga alipozungumzia wafungwa wanawake wakiwa wanafanya kazi na watoto kubakia gerezani. Yaani anazungumzia wakati wafungwa wanawake wakiwa wanafanya kazi. Basi napenda nitoe maelezo kwamba utaratibu uliopo ni kwamba wale wafungwa wanawake wenye watoto wachanga hawapangiwi kazi za kwenda kufanya nje wakaacha watoto wachanga ndani ya gereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia nitoe maelezo ya ziada. Pamoja na kwamba kuna msongamano wa wafungwa katika magereza yetu hivi sasa. Maeneo ya wafungwa wanawake hakuna msongamano mkubwa kwa kiasi hicho. Hili nalieleza kutokana na mimi mwenyewe kutembelea magereza na kukutana na wafungwa hao na kuona hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nichukue nafasi hii kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba kwa Mujibu wa Sheria *Prisons Ordinance* kila Mheshimiwa Mbunge ni *Visiting Justice* wa kutembelea gereza lililoko katika eneo lake. Kwa hiyo, natoa wito kwamba Waheshimiwa Wabunge mtumie fursa hiyo ili muweze kujionea hali halisi ilivyo katika magereza ili muweze kuishauri Serikali na tuweza kufanya maamuzi yaliyo mazuri zaidi. *(Makofi)*

Na. 90

**Tume ya Kurekebisha Sheria**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa Bunge lilipitisha Sheria Na. 11 ya mwaka 1980 ya kuunda Tume ya Kurekebisha Sheria (*Law Reform Commission*):-

(a) Je, kwa nini Bunge haliambiwi mpaka sasa juu ya Sheria ambazo zimerekebishwa ziko ngapi na zilizobaki ni zipi?

(b) Je, kwa nini Waziri mwenye dhamana ya Sheria hawasilishi taarifa ya utekelezaji wa Tume hiyo kama jinsi inavyosema?

(c) Kwa kuwa Kamati ya Kudumu ya Utawala, Katiba na Sheria ingefanya kazi hiyo kwa niaba ya Bunge, je, mpaka sasa Kamati hiyo imepokea taarifa yoyote ile ya Tume?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuundwa kwa Tume ya Kurekebisha Sheria jumla ya ripoti 22 zimewasilishwa Serikalini zikiwa ni matokeo ya tafiti mbalimbali katika masuala ya Sheria na mapendekezo ya Tume hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ripoti za Tume na mapendekezo yake Sheria mbalimbali zimerekebishwa, ama kutungwa na Bunge hili Tukufu. Mathalani, kutokana na ripoti ya Tume kuhusu tatizo la msongamano wa wafungwa magerezani ya mwaka 1994, Sheria ya Huduma kwa Jamii (*The Community Service Act*), na Sheria ya Bodi ya Parole zilitungwa na Bunge lako Tukufu. Kadhalika kutokana na mapendekezo ya Tume Sheria ya Kanuni za adhabu Sura ya 16 ilirekebishwa hususan kuhusiana na makosa ya kujamiiana.

Aidha, Sheria za Kazi za mwaka 2004 zilitungwa na Bunge lako Tukufu kutokana na mapendekezo ya Tume kwenye ripoti iitwayo "*Review of Labour Laws*" ya 2001. Kutokana na mapendekezo ya Tume Sheria 28 zilizotolewa mapendekezo na Tume ya Nyalali zimerekebishwa. Marekebisho mengi ya Sheria hizo yaliletwa kama marekebisho ya Sheria mbalimbali na kupitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wiki iliyopita tu Bunge limepitisha Marekebisho ya Sheria mbalimbali za ushahidi ambayo msingi wake ni ripoti ya Tume inayoitwa *Report on the Legal Framework on E-Commerce and Ciber Crimes*, 2006. Tarehe 8 mwezi huu, Muswada wa Sheria ya Kuzuia na kupambana na rushwa utasomwa ndani ya Bunge lako Tukufu. Muswada huu umetokana na ripoti ya Tume iitwayo *Report on Review of Legislation Relating to Corruption.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti hizo zote ukiondoa zile za mwaka 2006 zimeletwa mbele ya Bunge lako Tukufu na kugaiwa kwa kila Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, sanjari na kurekebishwa au kufutwa kwa baadhi ya Sheria kunakofanywa na Wizara yangu, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kutokana na ripoti na mapendekezo ya Tume, mchakato wa Kurekebisha Sheria za Ndoa, Sheria za Mirathi na zile za watoto unaendelea. Aidha, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa sasa inashughulikia Sheria ya Uraia wa nchi mbili ambayo msingi wake ni Ripoti ya Tume iitwayo *Report on Introduction of Dual Citizenship* ya 2006. Utaratibu uliop ni kuwa ripoti za Tume zinapopelekwa kwa Waziri wa Katiba na Sheria yeye huzipeleka kwenye Wizara husika ili zichukuliwe hatua muafaka. Sheria nilizozitaja hapo juu zitaletwa hapa Bungeni na Wizara husika.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Naibu Waziri kwa maelezo mazuri na majibu ya jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu kwa kuteuliwa kushika wadhifa katika Wizara hii muhimu sana katika historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Rais anateua Baraza lake la Mawaziri alishauriana na Mheshimiwa Waziri Mkuu waliona kwamba kwa kipindi kirefu kilicho ndani ya Bunge hili ilikuwa ni kuangalia upya Sheria zote zinazomkandamiza mwanamke pamoja na watoto. Kwa sababu Waswahili tunasema uchungu wa mwana ajuaye mzazi, walifanya makusudi mazima kumpa nafasi hiyo Mheshimiwa Dr. Mary Nagu ajaribu kupitia sheria zote za akinamama zinazowakandamiza pamoja na watoto na wazee.

La kwanza, kwa kuwa zipo sheria ambazo tumekuwa tukizungumza ndani ya Bunge hili Tukufu ya kwamba Sheria ya mama aliyezaa nje ya ndoa kupewa matunzo ya mtoto ya shs. 100 kwa mwezi yamepitwa na wakati na tumezungumza hili suala kwa kipindi kirefu. Je, Mheshimiwa Waziri haoni ya kwamba masuala mengine haya ni ya kuchukua dharura ili Tume inayohusika ichukue hatua zinazotakiwa? *(Makofi)*

La pili, kwa kuwa zipo sheria nyingine hata hufanyaje haziwezi kutekelezeka. Kwa mfano, sheria ya kunyonga watu ambayo Mheshimiwa Rais amepewa madaraka ya kunyonga watu. Lakini kwa kipindi kirefu tunafahamu matatizo ambayo Waheshimiwa Marais wetu wote kuanzia Awamu ya Kwanza mpaka wa Awamu ya Nne wanapata matatizo kuwanyonga Watanzania wapiga kura wao. Je, kwa nini kusiwe na marekebisho ya sheria hiyo. Aidha, turuhusu kuwe na jopo la Majaji watatu wakamilishe hiyo kazi badala ya kumuachia Mheshimiwa Rais ndiyo atoe uamuzi ya mwisho na kama haiwezekani kwa nini sasa basi tusipate maelezo tunashindwa nini kurekebisha sheria hiyo ambayo imekuwa ni ngumu kutekelezeka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli sheria ile ya matunzo ambayo inasema mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa atalipiwa shs 100 kwa mwezi imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba sasa hivi Wizara ya Katiba na Sheria iko mbioni kuandaa Sheria ambayo kwanza imetokana na mapendekezo ya Tume ambapo Tume ilileta taarifa kuhusu kubadili mfumo wa malipo ya Mahakama na faini kwa ujumla kwa kuweka kitu kinachoitwa *Currency Points*. Sasa *Currency Points* ni Sheria ambayo tutaileta katika Bunge hili ambayo itarekebisha mfumo mzima wa malipo ya faini na malipo kama hayo yanayowahusu watoto wanaozaliwa nje ya ndoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa *Currency Points* ni kwamba Mahakama pamoja na Wizara ya Fedha walikaa pamoja na kuweka utaratibu wa kusema kwamba *Currency point* moja ina thamani ya kiasi fulani na kwa wakati fulani. Kwa hiyo, utakapopigwa faini utaambiwa shs. 5 lakini utaambiwa ni *Currency Point* moja labda

ambayo sasa thamani yake itakuwa inabadilika kulingana na hali ya uchumi inavyokwenda hapa nchini. Kwa sheria hiyo tunadhani ikishapitishwa na Bunge hili basi utaratibu mzima wa malipo kama hayo ya watoto utakuwa unakwenda sambamba na hali ya uchumi wa nchi unavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sheria ya kunyonga ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba sasa hivi Tume ya Kurekebisha Sheria inapitia sheria hiyo na itatuletea mapendekezo tuone. Je, kama wakati muafaka umefika sasa wa kubadilisha sheria hii au bado. Lakini kimsingi wapo watu wengi sana katika nchi hii ambao wanasema sheria hii lazima ibakie na wapo wengine wengi pia wanaosema sheria hii iondolewe. Kwa hiyo, si rahisi kwa sisi kutamka kwamba tutaifuta au tutatumia utaratibu gani mpaka hapo Tume itakapotuletea mapendekezo na tunategemea mapendekezo hayo yataletwa ndani ya mwaka huu.

Na. 91

**Program ya Maji – Rufiji**

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mji wa Utete, Ikwiriri , Kibiti na Bungu imo katika mpango wa Programu ya maji ya Miji Midogo; na kwa kuwa, Mji wa Utete ni Makao Makuu ya Wilaya ya Rufiji lakini Mji huo hauna huduma ya maji, hali inayosababisha watu kunywa maji yasiyo salama toka mto Rufiji; na kwa kuwa, utekelezaji wa Mradi huo unasuasua mpaka inakatisha tamaa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huo?

(b) Ikiwa kuna matatizo katika mikataba ya Mradi huo. Je, Serikali ina mpango gani mbadala ya kuwanusuru wananchi wa Rufiji ili wapate huduma ya maji safi, salama na kwa uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Utete ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Rufiji unapata huduma ya maji kutoka katika bwabwa la asili la Ligongwe. Kutokana na hali ya miundombinu inayotumika, hivi sasa upatikanaji wa huduma ya maji unafikia mita za ujazo 450 kwa siku. Kiasi hiki ni asilimia 67 ya mahitaji halisi ya maji kwa mji mzima yanayokadririwa kufikia mita za ujazo 670 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la kifedha la *AFD*, ilibuni Programu ya aji na Usafi wa Mazingira katika Miji Midogo.

Programu hii inatekelezwa katika Miji Midogo ya Utete, Ikwiriri na Kibiti katika Wilaya ya Rufiji, Turiani na Mvomero katika Wilaya ya Mvomero, Kilosa na Gairo katika Wilaya ya Kilosa, Kibaigwa katika Wilaya ya Kongwa na Mpwapwa katika Wilaya Mpwapwa. Utekelezaji wa Programu hii upo katika hatua mbalimbali.

Hadi sasa, kazi ya uchimbaji wa visima vya utafiti katika Miji yote tisa na usanifu wa awali wa miundombinu ya maji zimekamilika. Aidha, mchakato wa uundaji na uimarishaji wa vyombo huru vya kisheria vya kusimamia uendeshaji wa miradi ya maji itakayojengwa katika kila Mji umeanza na upo kwenye hatua za mwisho kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Prof. Mtulia, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa utekelezaji wa programu hii umechelewa. Kuchelewa huku kumetokana na sababu kuu mbili. Sababu ya kwanza, ni uchimbaji wa visima vya utafiti kuchukua muda mrefu zaidi kuliko ilivyotarajiwa. Hali hii ilitokana na kazi ya uchimbaji visima kufanywa na Mkandarasi mmoja kwa Miji yote tisa.

Hapo awali, tenda za kuchimba visima zilitolewa katika makundi matatu, kwa lengo la kupata Wakandarasi watatu tofauti. Hata hivyo, ni Mkandarasi mmoja tu ndiye aliyeshinda tenda katika makundi yote matatu, na hivyo kufanya uchimbaji katika Miji yote tisa, ikiwa ni pamoja na Utete. Sababu ya pili, ni mchakato mrefu wa uchujaji wa miji kutoka tisa hadi idadi inayolingana na kiasi cha fedha kilichotengwa na mfadhili. Vigezo vinavyotumika katika kuchuja

Mheshimiwa Naibum Spika, Miji ni pamoja na kuwepo kwa vyanzo vya maji vya uhakika na chombo imara cha kusimamia uendeshaji wa huduma ya maji katika Mji huo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa programu hii, Serikali kwa kushirikiana na mfadhili imeamua kufanya usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni za ujenzi kwa miji yote tisa, bila kujali miji itakayoachwa katika mchujo huo. Hivi sasa, Serikali inakamilisha marekebisho ya mkataba wa awali ili kumwezesha mtaalam mshauri kufanya kazi hii ya nyongeza.

Aidha, napenda niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka kwenye Majimbo yenye programu hii, kuwa miji ambayo haitapata fedha za ujenzi chini ya ufadhili wa Serikali ya Ufaransa, utekelezaji wake utazingatiwa katika Programu ya Kitaifa ya Kuendeleza Sekta ya Maji, kwani usanifu wa miji hiyo utakuwa umekamilika. Kazi yake itaanza mara moja.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Mikataba inayohusu Programu hii haina matatizo. Serikali ipo makini na itaendelea kusimamia kwa karibu Programu hii ili kuhakikisha kuwa lengo lililokusudiwa la kuwapatia wananchi huduma endelevu ya maji safi na elimu ya usafi wa mazingira kwa miji yote tisa, linafanikiwa.

Aidha, wakati ambapo programu hii inaendelea kuandaliwa, Serikali itaendelea kuimarisha huduma iliyopo ya maji yanatokana na Bwawa na Ligongwe, ambayo inakidhi asilimia 67 ya mahitaji ya sasa, Serikali itahudumia kulingana na uwezo wake wa kifedha.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini bado, kwa sababu huu mradi ulibuniwa karibu miaka sita iliyopita, hilo la kwanza.

La pili, kwamba hiyo asilimia 67 si kweli na ninaomba kama yupo mhakiki twende naye Utete pale aingie nyumba yoyote afungue maji kama yatatoka. Kwa maana hiyo ninaomba Serikali, naijua Wizara ya Maji ina uwezo mkubwa wafanye mpango wa dharura kabisa ili tupate maji kwa uhakika katika mji wa Utete na miji mingine?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza tutakuwa tayari kwenda naye ili kuangalia vizuri huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kwa kupitia Wizara yangu ya Maji iko mbioni na inafanya mipango mingi kuhakikisha maji yanaongezeka ikiwemo kwa sasa hivi katika jimbo lake la Rufiji kuna miradi minne ya maji ambayo tunategemea itakayoanza wakati wowote kuanzia mwezi wa Nne chini ya Programu ya Maji Safi na Mazingira ikiwemo katika kijiji cha Kiwanga, Mbwala, Ngorongo na Nyawanja.

Pia katika miradi midogo midogo ambayo tunaita *quick wings* kwa mwaka huu ambapo Wizara yangu itahudumia miradi mingi midogo midogo ya kuchimba visima na kurekebisha miradi iliyopo ikiwepo Utete yenyewe, Ukiwa Zimbwini Shule ya Sekondari, Ikwiriri, Kibiti, Mahege, Msona na Nyamwili.

Na. 92

**Ukosefu wa Maji – Makere**

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika kijiji cha Makere Wilaya ya Kasulu Mkoani Kigoma, Shirika la Wakimbizi la *TCRS* lilichimba visima vya maji ambavyo mpaka sasa havitoi maji hali inayosababisha wananchi wa kijiji hicho kupata shida ya maji; na kwa kuwa, kijiji hicho kinapakana na Nyarugusu ambapo kuna mashine kubwa ya kupampu maji yenye uwezo wa kupeleka maji hayo katika kijiji cha Makere:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maji wananchi wa kijiji hicho ikiwa ni pamoja na Kituo cha Polisi kilichopo Kijiji hapo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Kijiji cha Makere ni miongoni mwa vijiji vitatu vinavyounda Kata ya Nyamidaho. Vijiji vingine ni Nyamidaho na Mvugwe. Kijiji cha Makere kipo jirani na Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu. Kijiji hiki kina wakazi wapatao 7,000.

Katika kuhakikisha kuwa wananchi wa Kijiji cha Makere wanapata huduma ya maji safi na salama, Serikali kwa kushirikiana na wafadhili mbalimbali imefanya yafuatayo:-

(i) Mwaka 2005 Shirika la *TWESA* lilifunga pampu ya mkono kwenye kisima ambacho kilikuwa na pampu ya kusukuma maji kwa mashine. Kisima hiki kinaendelea kutoa huduma ya maji kwa wananchi.

(ii) Mwaka 2006 Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *TWESA* na *UNICEF* ilichimba visima vifupi saba, vinne vimekamilika na vinatoa huduma ya maji na vitatu havikukamilika kutokana na wananchi kushindwa kufanya kazi za kujitolea ili kukamilisha ujenzi huo. Pampu 3 za visima ambvyo havikukamilika zimehifadhiwa katika Bohari ya Shirika la *TWESA*. Aidha, uongozi wa Wilaya unaendelea kuhamasisha wananchi ili kuhakikisha kuwa visima vitatu vilivyobaki vinakamilika na kutoa huduma ya maji.

(iii)Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006, Serikali kwa kushirikiana na *TWESA* ilitumia shilingi 44,780,000 kuchimba visima virefu vitano kwa kutumia mkandarasi *TCRS Kibondo.* Visima vitatu vimekamilika na kufungwa pampu za mkono na vinatoa huduma ya maji. Visima vingine viwili havina maji ya kutosha. Halmashauri ya Wilaya imepanga kuchimba visima katika maeneo mengine ndani ya kijiji, ili pampu mbili zilizobaki ziweze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada zote zilizofanywa na Serikali na wafadhili mbalimbali wa kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuwa na Kamati za maji na mifuko ya maji, hadi sasa kijiji hakijaanzisha Kamati ya Maji na mfuko wa maji kwa ajili ya kuendesha miradi yao. Uongozi wa Wilaya unaendelea kuhamasisha wananchi ili waunde Kamati ya Maji na mfuko wa maji kwa ajili ya huduma endelevu ya maji. Baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mpango uliopo wa kuwapatia maji wananchi wa kijiji cha Makere katika mwaka wa fedha 2006/2007 ni kukamilisha uchimbaji na ujenzi wa visima virefu viwili. Pia, mpango ni kukamilisha visima vifupi vitatu na kufunga pampu zake ambazo zimehifadhiwa na Shirika la *TWESA.* Aidha, mashine ya kusukuma maji iliyopo Nyarugusu ina uwezo wa kuhudumia wananchi wa Nyarugusu tu. Kwa vile kijiji cha Makere kina vyanzo vya maji ni vizuri basi vitaendelea kutumika hivyo na kufadhiliwa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Mbunge aendelee kuhamasisha wananchi ili waanzishe Kamati na Mifuko ya Maji kwa ajili ya uendeshaji na matengenezo ya miradi yao ya maji ili iwe endelevu.

**MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa katika kijiji cha Makere kuna kituo cha Polisi na hicho kituo cha Polisi kiko karibu na Kambi ya Nyarugusu na kituo hicho kwa kujionea mimi mwenyewe hawana maji wanapata shida kabisa ya kupata maji pale kituoni na kuna wananchi ambao wamezunguka kituo hicho. Je, kwa kuwa katika Kambi ya Nyarugusu kuna mashine kubwa ya kuweza ku-*supply* maji mpaka pale kwenye kile kituo cha Polisi, Serikali inasemaje kuhusu hilo?

Pili, kwa kuwa tatizo hilo ni sambamba kabisa na tatizo lililoko Kigoma Vijijini hasa kijiji cha Simbo ambacho kilichimbiwa visima saba kuanzia mwaka 1990. Kuanzia mwaka 2002 hawajapata maji wanakuwa wanapata shida ya kufuata maji wanakwenda kuchota katika Mto Luiche na wengine wanaliwa na mamba. Je, Serikali inasemaje?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Suala la Kijiji cha Nyarugusu napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kijiji hicho kuna mradi wa visima vifupi 5 ambavyo bado havijaanza kufanya kazi vinaendelea kuchimbwa. Visima hivi vitano ni visima ambavyo vinafadhiliwa na Shirika la Umoja wa Wakimbizi *UNHCR* na ambapo wakimaliza itaboresha huduma ya maji na nina uhakika kwamba sehemu hiyo yote pamoja na Kambi ya Polisi ya Kituo cha Polisi watapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la pili la kuhusu vijiji vya jirani huko. Ni kweli kwamba vijiji vya Kigoma Vijijini havina maji baadhi yao ni kwa sababu ya chini ya ardhi hakukupatikana maji. Lakini hata hivyo kwa sasa hivi tuna utaratibu mkubwa wa kutumia maji ya mtiririko ambayo kuna miradi sasa hivi ipatayo mitano ya sehemu za mtiririko ambazo zitategwa maji kwa ajili ya sehemu mbalimbali za Kigoma Vijijini. Pia naomba kwa Mheshimiwa Mbunge kwamba orodha ya vijiji hivyo ninavyo lakini naomba nimpatie baadaye ili tuokoe muda.

Na. 93

**Uwakilishi wa Wanafunzi katika Bodi ya Mikopo**

**MHE. MWANAHAMIS K. SAID** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kutekeleza mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya mwaka 2005/2006 kuhusu uwakilishi wa wanafunzi katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu tayari wameshateuliwa wawakilishi wawili, mmoja kutoka Visiwani.

Je, mwanafunzi anayetoka Visiwani anaitwa nani na anatoka Chuo gani Chwaka, SUZA, Tunguu au Chukwani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwanahamisi K. Said, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake, kwanza napenda kumsahahihisha kuwa hakuna vyuo vya Elimu ya Juu vinavyoitwa Chwaka, Tunguu au Chukwani. *(Makofi)*

Pili, uamuzi wa kuwa na uwakilishi wa wanafunzi katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu siyo kutekeleza mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya mwaka 2005/2006 bali ni kutekeleza Sheria namba 9 ya mwaka 2004 iliyoanzisha Bodi ya Mikopo sehemu ya 5(1) inayozungumzia muundo wa Bodi (*Composition of the Board*) ambayo pamoja na mambo mengine inataka uwakilishi wa mjumbe mmoja kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu binafsi na mjumbe mwingine kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma. Kwa hiyo, wajumbe hawa wanaweza kutoka Tanzania Bara au Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bada ya kufanya masahihisho hayo napenda kumjibu Mheshimiwa Mwanahamisi K. Said, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake kama ifuatavyo:-

Mwanafunzi aliyekuwa mwakilishi katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka Visiwani na ambaye alikuwa anawakilisha Vyuo binafsi anaitwa Ndugu Said A Mkasiwa, kutoka Chuo Kikuu cha Zanzibar (*Zanzibar University*) ambaye kwa sasa amehitimu masomo yake. Hata hivyo, mawasiliano yamefanyika tayari na vyombo husika ili aweze kupatikana mwakilishi mwingine kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu binafsi.

Na. 94

**Azma ya Kuwa na Akiba Maalum ya Mafuta**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa, sasa Serikali imeona umuhimu wa kuwa na akiba maalum *(Strategic Reserve)* ya mafuta ya petroli ambapo kimsingi yanaweza kusaidia kuwezesha bei za mafuta hayo kutulia kwa muda na hata mafuta hayo kutumika wakati wa dharura au upungufu:-

(a) Je, ni mkakati gani umeandaliwa sasa ili kutekeleza azma ya Taifa ya kuwa na akiba ya maalum kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa;

(b) Je, yapo Makampuni ya mafuta ya ndani au nje yanayotaka kushirikiana na Serikali katika kutekeleza azma hiyo ya kuwa na akiba maalum ya mafuta.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mntangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tamko la kuruhusu Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* kuanzisha, kuendeleza na kusimamia hifadhi ya mafuta ya dharura ya Serikali lilitolewa tarehe 18 Julai, 2006 mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, tamko hilo liliiruhusu *TPDC* kushiriki katika uagizaji na usambazaji wa mafuta ya petroli nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, tangu tamko litolewe, *TPDC* wamekuwa wanaandaa mkakati wa namna ya kutekeleza azma hiyo. Mchakato wa awali umehusisha tathmini ya faida za kiuchumi na kifedha. Taarifa ya awali hiyo *(Business Plan)* ilichambuliwa na taarifa kamili (*The New Business Plan)* ilipitiwa na wadau na hatimaye Bodi ya Wakurugenzi wa *TPDC* kabla ya kuwasilishwa Serikalini.

Taarifa hiyo ina mapendekezo kadhaa ambayo yanafanyiwa kazi, kama vile kuangalia upya sheria zilizopo pamoja na kutafakari sheria zitakazohitajika katika kuanzisha na kuendesha hifadhi ya mafuta ya akiba ya dharura. Vile vile kumekuwepo pia na haja ya kuangalia *risk* zote wakati wa kutekeleza majukumu hayo kwa lengo la kuchukua tahadhari mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sehemu ya maandalizi ya *Business Plan, TPDC* pamoja na wataalamu wengine wa Serikali wamekuwa wakitathmini uzoefu wa nchi mbalimbali ambazo tayari zinatekeleza mikakati kama hiyo ikiwemo Serikali hizo kuwa na hifadhi ya mafuta ya dharura na Kampuni za Serikali zinavyoshiriki katika biashara ya mafuta ili kulinda maslahi ya Taifa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia ziara ya Mheshimiwa Rais katika Nchi za Falme ya Kiarabu mwezi Mei, 2006 Wizara kupitia Ubalozi wetu nchini humo imekwishawasilisha mchakato wa kiasi na ubora wa aina zote za mafuta ya akiba ya mafuta ya dharura ambayo *TPDC* itahitaji.

Aidha, Wizara inakamilisha Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu kuanzisha na kuendesha hifadhi ya akiba ya mafuta.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu haya ni wa gharama kubwa hivyo inatubidi kujitayarisha kikamilifu na kutafuta rasilimali ya kutosha. Ili kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi na kwa uwazi *TPDC* waliitisha zabuni kutoka kwa Makampuni ya nje na ndani ya nchi yenye nia ya kushirikiana na *TPDC* katika kutekeleza azma hizo. Zabuni hizo zilifunguliwa tarehe 26 Oktoba, 2006, uchambuzi ukafanyika kwa ajili ya kumpata mshindi. Mshindi alipatikana na sasa unasubiriwa uamuzi wa Serikali ili mbia huyo aweze kuwasilisha *detailed plan* kwa ajili ya majadiliano (*negotiations).*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana aliyoyatoa. Lakini naomba pia

kumpongeza sana Mheshimiwa Rais pamoja na Shirika la Maendeleo la *TPDC* kwa jitihada ambazo wanafanya katika kuhakikisha *Business Plan* hiyo inakamilika. Baada ya kusema hayo naomba kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hapo awali Kiwanda cha *TIPPER* kilikuwa na hifadhi kubwa sana ya mafuta. Je, Serikali ina mkakati wowote wa kufikiria ili kama sehemu ya kupunguza gharama au kusaidia na kubeba hizi gharama. Je, wale waliouziwa Kiwanda hicho Serikali inaweza kuwa na hisa ili tupate mahali pa kuanzia kuhifadhi mafuta hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mpaka sasa hivi Serikali ina hisa katika hilo Shirika ama Kampuni iliyokuwa inaitwa *TIPPER* na wana hisa katika hilo Shirika ama Kampuni ni Serikali yenyewe kwa asilimia 50 pamoja na Kampuni moja ya Uswiss inaitwa *ADARTS.* Lakini mkakati uliopo unahakikisha kwamba rasilimali tunaendelea kuitumia kwa maslahi ya Taifa. Lakini kwa sasa hivi Serikali bado inaendelea na kuangalia utaratibu mzuri zaidi ambao utatuwezesha kuifaidi hiyo rasilimali yetu ambayo tulishawekeza kwa miaka mingi.

Na. 95

**Uhusiano Kati ya Dhahabu na Utajiri**

**MHE. OMAR S. KWAANGW' (k.n.y. MHE. DAMAS P. NAKEI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Dhahabu ni Madini yenye thamani kubwa; na kwa kuwa, utajiri wa Nchi huhusishwa na utajiri wa Dhahabu ulioko katika Nchi husika:-

(a) Je, kuna ukweli kuhusu uhusiano huo?

(b) Je, kwa nini utajiri wa Dhahabu na kazi ya uchimbaji inayoendelea Nchini haifanani na kasi ya maendeleo kiuchumi au kijamii?

(c) Je, kuna matumaini yoyote kuwa, kuna siku tutaona umaskini unatoweka kwa kiwango kilekile ambacho kinaongezeka katika uchimbaji wa Madini hususan Dhahabu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nchi yenye dhahabu nyingi kwenye hazina ya Benki Kuu yake ni tajiri. Aidha, uchumi wa nchi hiyo utakuwa hauyumbiyumbi kwa kuwa thamani ya dhahabu haiathiriwi na kupanda au kushuka kwa thamani ya fedha ya nchi husika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, utajiri wa nchi hautokani na kuwepo kwa dhahabu pekee bali utajiri huoanisha rasilimali mbalimbali za nchi. Madini yaliyopo chini ya ardhi, kama ilivyo kwa rasilimali zingine ambazo hazijavunwa, ni utajiri uliolala (*dormant wealth*) na hauna manufaa ya moja kwa moja kwa maendeleo ya wananchi mpaka ukigeuzwa kuwa thamani.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, sio rahisi kupima kasi ya maendeleo ya kiuchumi au kijamii yanayotokana na utajiri wa dhahabu wa nchi yetu na uchimbaji unaoendelea. Aidha, vigezo vya maendeleo, ikiwemo ukuaji wa pato la Taifa, huorodhesha ongezeko la uzalishaji wa bidhaa na huduma mbalimbali katika sekta mbalimbali za uchumi pamoja na shughuli zake. Uchimbaji wa dhahabu ni moja ya shughuli katika ubadilishaji wa utajiri uliolala kuufanya uwe thamani inayouzika ndani na nje ya nchi.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa sekta hii ya Madini ina wawekezaji wakubwa. Na kwa kuwa sekta hii inahusisha mapato makubwa kutokana na madini na vile vile kwa kuwa udhaifu wowote katika kuweka nyaraka na kumbukumbu za mapato unaweza ukaiületea hasara kubwa sana nchi. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kwamba uwekaji wa nyaraka na kumbukumbu muhimu katika sekta hii unapewa kipaumbele?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mikakati mingi ambayo itahakikisha inapata uelewa mkubwa lakini pia inakuwa kwenye nafasi nzuri ya kudhibiti ama kupata manufaa zaidi kutokana na shughuli ambazo zinatokana na madini. Mojawapo ni hili hili ambalo tunafahamu sisi sote. Serikali kupitia Wizara husika imemwajiri Mkaguzi ama mtaalamu wa shughuli ambazo zinatokana na shughuli za migodi. Lakini kwa kumwajiri yeye sisi kama nchi tunakuwa tunafaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera na sheria za madini zinapitiwa kuhakikisha kwamba mapungufu ama udhaifu ambao umejitokeza katika sera na sheria zetu kwa sasa zinarekebishwa ili ziwe za manufaa zaidi kwa nchi yetu na watu wake.

Na. 96

**Ununuzi wa Pantoni – Kigamboni**

**MHE. MINCHOUM A. MSOMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika makisio ya mwaka wa fedha 2006/2007, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa pantoni moja kubwa itakayokidhi mahitaji yaliyopo kulingana na kivuko cha Kigamboni – Feri; na kwa kuwa, wananchi wana hamu ya kujua suala zima limefikia wapi:-

(a) Je, ni lini pantoni hiyo inatarajiwa kuanza kazi?

(b) Kwa kuwa, Kivuko cha Kigamboni – Magogoni ni kama njia. Je. Serikali haioni umuhimu kwa sasa kurudisha utaratibu wa watu kuvuka bure ila wenye magari na baiskeli waendelee kulipa kama ilivyokuwa awali?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA )** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mbunge wa Kigamboni, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kivuko cha Magogoni kuna pantoni mbili zinazotoa huduma ya kuvusha abiria na magari kutoka pande zote mbili za Magogoni na Kigamboni. Pantoni hizi zilianza kutoa huduma hiyo kuanzia mwaka 1990. Aidha, vivuko hivyo vilifanyiwa ukarabati mkubwa mwaka 1996 na 1999 Mombasa, Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Abdurahman Msomi, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mwezi Oktoba 2006 Serikali ilisaini mkataba na Kampuni ya *Neue Ruhrorter Gmbh* kutoka Ujerumani itakayojenga na kuleta kivuko kipya cha Kigamboni. Kivuko hiki chenye uwezo wa kubeba, tani 500 kinategemea kuanza kazi mwezi Aprili, 2008.

(b) Ni kweli kivuko ni kama njia, lakini kwa kuwa abiria wanaovuka katika kivuko cha Magogoni huchangia takriban asilimia 60 ya mapato ya kivuko kwa siku, na kwa kuwa Serikali ilikwishaamua kwamba gharama zote za uendeshaji wa kivuko hiki zitoke kwenye mapato yanayotokana na nauli ya abiria na magari, hivyo kurudisha utaratibu wa zamani wa abiria kuvuka bila kulipa nauli kutasababisha kushindwa kuendesha kivuko.

**MHE. MINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri. Kwa kuwa usalama wa wananchi ni muhimu. Na kwa kuwa katika kivuko cha Kigamboni pale hivi sasa magari yanayosafirisha mizigo ya mafuta yaani petroli na dizeli yanapita katika vivuko hivi. Na kwa kuwa katika vivuko hivyo hakuna angalau vifaa vya kuzimia moto.

Je, Serikali haioni kwamba ni muhimu kuwashauri wenye bidhaa hizo kutumia barabara ya Kongowe hadi Ferry ili kupeleka bidhaa zao hizo, kuepusha maafa kwa wananchi?

La pili, kwa kuwa maboya yanayotumika katika vivuko hivi hayakuwekwa mahali ambapo wananchi wanaweza kuyafikia kwa haraka pindipo dhahama ya aina yoyote ikitokea. Je Wizara haioni kwamba hili tatizo kwa wananchi na kama dhahama itatokea maafa makubwa yanaweza yakatokea kutokana na kuyafungia?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu la magari yanayovusha bidhaa za petroli kupita katika pantoni ile nadhani tulishatoa maelekezo. Kama bado magari hayo yanapita kwenye pantoni na bidhaa za mafuta nadhani hili tutalifuatilia kama tulivyokwishasema magari ya aina hiyo yazunguke kwenye barabara badala ya kupita pale.

Lakini ni kweli vile vile kwamba katika pantoni zetu kuna *fire extinguishers* labda tatizo ni uelewa ambao wanatakiwa wananchi waelewe kwamba vifaa vile vipo na vinaweza vikatumika.

La pili, kuhusu maboya kutoonekana, hili ni suala lenyewe ambalo tumeshalisisitiza sana kwamba maboya waelewe kwamba maboya yapo ili pindi kama kunatokea matatizo yoyote basi waweze kujua namna gani ya kujiokoa.

Lakini tutaendelea kusisitiza basi ili maboya yale yaweze kujulikana kwamba yako wapi na yanafikiwa kwa urahisi kiasi gani.

Na. 97

**Maslahai ya Askari wa Chini ya Jeshi la Polisi**

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliahidi kuboresha maslahi ya askari wa chini wa Jeshi la Polisi; na kwa kuwa, iliahidi pia kurekebisha sheria mbalimbali zilizopitwa na wakati hasa *Police General Order (P.G..O.):-*

(a) Je, kwa kipindi cha miezi 11 maslahi ya askari hao yamerekebishwa vipi?

(b) Je, ni maeneo mangapi kwenye *P.G..O.* yaliyofanyiwa au yatakayofanyiwa marekebisho?

**NAIBU WAZIRI USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mbunge wa Mwanakwerekwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Serikali iliahidi kuboresha maslahi ya Askari Polisi. Katika kuhakikisha maslahi yao yanaboreshwa, Wizara ya Usalama wa Raia iliunda Tume ya wataalam ambayo ilitayarisha mapendekezo ya kuboresha mishahara na posho mbalimbali wanazolipwa askari Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume hiyo imemaliza kazi yake na mapendekezo hayo tayari yaamewasilishwa kwenye mamlaka zinazohusika

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Wizara ya Usalama wa Raia, iliahidi kufanya marekebisho ya kanuni mbalimbali zinazotawala utendaji wa Jeshi la Polisi ili ziweze kukidhi haja na mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kukua kwa demokrasia na utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sio rahisi kutaja maeneo yote yaliyofanyiwa marekebisho, kufutwa na kuingizwa kwa mara ya kwanza katika *P.G.O.* Hata hivyo, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, kimsingi maboresho yaliyofanywa, yamezingatia mabadiliko ya Katiba ya Nchi, kutungwa na kufanyiwa marekebisho kwa

sheria mbalimbali za nchi na za Kimataifa zikiwemo: Kanuni ya Adhabu; Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka wa Makosa ya Jinai; Sheria zinazohusu watoto; Sheria ya Vyama Vingi vya Siasa; Sheria ya Kudhibiti Fedha na Sheria ya Ununuzi wa Vifaa vya Serikali; Matumizi ya Silaha kwa Mujibu wa Kanuni za Kimataifa *(UN Basic Principles on the Use of Force and Fire arms by Law Enforcement Officials, 1990; UN Code of Conduct for Law Enforcement Officials, 1979;* na miongozo mbalimbali iliyotolewa na Serikali, kuhusu namna ya utawala wa Jeshi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Marekebisho ya *PGO* yamekamilika na hivi sasa Jeshi letu la Polisi linaendeshwa kutumia *PGO* hiyo mpya. Napenda pia kuchukua fursa hii, kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na Wabunge wote, kwa michango yao, ambayo ilituwezesha kufanya marekebisho hayo, ambayo yamelenga kuboresha utendaji wa Jeshi la Polisi. Aidha, napenda kuwashukuru, Watendaji wa Wizara, Jeshi la Polisi na Wataalam wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa kufanikisha maboresho hayo ya *PGO*.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na suala la maslahi ya hawa Askari, lakini vile vile kuna tatizo kubwa linalohusiana na makazi kule wanakoishi. Askari wengi hawana nyumba za kuishi na bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna baadhi ya maeneo ameyatembelea, ambayo ni pamoja na Musoma, amekuta maaskari wanaishi kwenye ma-*hall*. *Hall* moja wanaishi Askari zaidi ya watano na wanaweka maturubai wakiwa wanaishi na familia zao.

Sasa sijui Naibu Waziri, anasema nini katika hilo? Ni hatua zipi ambazo zinaweza zikafanyika kwa haraka ili hao maaskari waweze kuishi katika nyumba nzuri?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli lipo tatizo la makazi ya Askari katika Mikoa mbalimbali hapa nchini. Hata hivyo, Serikali kupitia Jeshi la Polisi, imechukua hatua mbalimbali ya kusaidia ujenzi wa nyumba za Askari na kuna Programu Maalum ya Ujenzi wa Nyumba hizo, tumeanza katika Mikoa mingi na tunaendelea nazo na kila mwaka Serikali inapanga Bajeti yake, ikitazama sana kuhusu suala la ujenzi wa nyumba za Polisi. Hata hivyo, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na *NSSF,* nalo linaendelea kuwahakikishia namna bora ya ujenzi wa nyumba za Polisi. Hivi sasa kuna maghorofa 60 yatakayojengwa, kwa kuanzia pale Kurasini na Zanzibar ili kuwahakikishia makazi mema Askari Polisi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu, kuhusu maslahi ya Askari. Kwa hivi sasa kima cha chini cha *Constable* ni shilingi 121,000, ambapo wafanyakazi wengine wa Serikali wanalipwa shilingi 75,000. Pia *Ration* imeongezeka sasa hivi na kufikia shilingi 50,000 kwa mwezi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa bahati mbaya, nimejitahidi kukimbia na maswali hatukuweza kumaliza na wala hatuwezi kusingizia kwamba tulianza na matangazo, maana yake hatukufanya hivyo. Kwa hiyo, muda wa maswali umekwisha na maswali mawili yamebaki. Nina matangazo mengi mpaka mwenyewe nayahofia.

Kwanza kabisa, nilisema wakati tunaingia kwamba, tunaye *High Commissioner* wa Uingereza na amefuatana na *Political Secretary* wake, Bwana John Show. Sasa Balozi amekuja kwa ajili ya kutoa *Briefing,* kwa Ujumbe wa Wabunge, watakaokwenda kuitembelea Uingereza mwezi huu. Wajumbe hao wanatangaziwa kuwa, leo tarehe 7 Februari, 2007, kuanzia saa 1.30 usiku watakuwa na *Briefing* na Balozi katika Ukumbi wa *Veta*. Kwa hiyo, wale wanaofahamu kwamba, watakwenda huko, waende wakashiriki katika *Briefing* hiyo.

Mbele yetu hapa tuna wageni, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini, Mkoani Iringa, naomba wote wa-*raise* mikono. Halafu tuna wageni wa Chama cha Wabunge cha Mapambano Dhidi ya UKIMWI, wamekuja kutembelea *TAPAC.* Naomba wasimame pia. Halafu tuna wanafunzi wa Sekondari ya Mlamya, Kasuru Kigoma, wasimame kama wapo. Halafu pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Diwani Leonard Kiganga. Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, ambao ni Mheshimiwa Gerald Gwaha, Mheshimiwa Michael Haichi na Ndugu Joseph Lwehae.

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, yupo Mwalimu Mwita. Vile vile tunao wageni wa Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, ambaye ni mchoraji maarufu wa mabango mengi makubwa, Ndugu Kisangi. Tunaye pia Meneja Uhusiano wa Benki ya *NMB,* Ndugu Shy-rose Banji.

Sasa nina matangazo ya kazi, nayo ni mengi. Kwanza kabisa, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mnadhimu wa Kambi ya Upinzani, anawatangazia Wabunge wa Kambi ya Upinzani kuwa, kutakuwa na Kikao cha Kambi ya Upinzani leo saa 10.00 jioni, Ukumbi Namba 219, ghorofa ya pili.

Wakati huo huo pia, Chama cha Mapinduzi nacho kinatangaza kwamba, kutakuwa na Kikao leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa. Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, anaomba Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hiyo, wakutane leo saa 5.00 asubuhi katika chumba namba 428. Halafu Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wa Tanzania wa Kupambana na Ukimwi, kwanza nakukaribisha na kukupa pole, kwa msiba wa mama yako. Anawatangazia Wajumbe wake watakutane saa 7.00 mchana, kwenye Ukumbi wa Msekwa. Mtagongana, Ukumbi wa Msekwa una watu, tafuteni kwingine. Halafu Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Katibu wa Kamati ya Wabunge wote wanaotoka Mikoa inayolima zao la Korosho, anaomba Wajumbe wa mikoa hiyo wakutane chumba namba 432 saa 7.00 mchana.

Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Basil P. Mramba, anawakumbusha na kuwakaribisha kwenye Maonesho ya *SIDO,* yatakayofunguliwa leo saa 8.00 mchana kwenye Uwanja wa *Nyerere Square*, Dodoma. Mheshimiwa Jenister J. Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anawataka Wajumbe wa Kamati yake, wakutane katika Ukumbi Namba 133, ghorofa ya kwanza, saa 7.00 mchana, sijui mtafanyaje, Kamati zinakutana? Halafu Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anawatangazia Wajumbe wake, wakutane leo saa 5.00 asubuhi katika chumba namba 231

Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William H. Shellukindo, anaomba Wajumbe wake, wakutane saa 5.00 asubuhi hii katika chumba namba 432, kama vinagongana mtajua wenyewe huko. Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John M. Cheyo, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali na Serikali za Mitaa, wanaotarajia kufanya ziara ya mafunzo katika Bunge la Uingereza, wakutane na Balozi wa Uingereza saa 1.30 jioni kule kwenye Hoteli ya *Veta*, hilo nilishalitangaza mwanzo. Matangazo ni mengi na mta-*sort out* wenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, matangazo yamekwisha. *(Makofi)*

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Hali ya Ulinzi na Usalama Nchini

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii, niweze kuwasilisha Taarifa ya Hali ya Ulinzi na Usalama nchini, kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2006. Kabla sijawasilisha Taarifa hii, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuvusha salama hadi kuuona mwaka 2007. Hivyo, Wizara ya Usalama wa Raia, inawatakia kheri na fanaka katika mwaka huu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wizara ya Usalama wa Raia, napenda kutoa salaam za rambi rambi, kwa Mheshimiwa Spika, kwako wewe Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa msiba mkubwa uliotupata wa kuondokewa na Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti. Mwenyezi Mungu, amlaze mahali pema. *Amen.*

Aidha, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dr. Asha-Rose M. Migiro, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Mheshimiwa Dr. Migiro tulikuwa naye na alishirikiana nasi vema, tunaamini atafanya hivyo pia huko aendako. Nampongeza pia Mheshimiwa Bernard K. Membe, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Hali kadhalika, nampongeza Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na nina imani atatulea vema humu Bungeni. Nampongeza pia Mheshimiwa William M. Ngeleja, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

Vile vile nampongeza Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Wote hawa, ninawaombea afya njema, kheri na fanaka katika kutekeleza majukumu yao mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, hali ya usalama wa nchi yetu katika kipindi hicho, imeendelea kuwa ya amani na utulivu na wananchi wameendelea kutoa ushirikiano mkubwa kwa Jeshi la Polisi, kwa kulipatia taarifa sahihi.

Taarifa hizo ziliwezesha kushughulikia baadhi ya matukio ya uhalifu, kuzuia uhalifu usitokee na hata kuwakamata wahalifu. Katika kipindi hiki cha Oktoba hadi Desemba, 2006, yalikuwepo matukio ya uhalifu, ambayo hata hivyo, hayakuwa makubwa

kiasi cha kuhatarisha amani nchini. Limekuwa ni suala la faraja, kwani jeshi letu limeendelea kumudu, kudhibiti na kujipanga vizuri, kuzuia uhalifu kwa kiwango cha kuridhisha. Naamini sote ni mashahidi wa mafanikio haya. Natoa pongezi kwa Jeshi la Polisi, kwa kazi nzuri ya kudhibiti uhalifu kutokana na ujasiri, umahiri, ubunifu wa mikakati mizuri, kufanya kazi kitaalam *(professionally)* na kuwa na ushirikiano wa karibu na wananchi. Nampongeza Inspekta Jenerali wa Polisi na Makamishna wa Makao Makuu, kwa kazi nzuri ya kuliongoza vema jeshi letu. Nawapongeza Ma-*RPC*, Ma-*OCD* na askari wote kwa ujumla, kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa, kati ya Januari hadi Machi, 2006, wakati Serikali ya Awamu ya Nne inaingia madarakani, matukio makubwa ya jinai yalikuwa 13,798 kwa miezi ya Januari hadi Machi, 2006, ikilinganishwa na matukio 8,130 yaliyoripotiwa katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2006.

Kuna upungufu wa matukio 5,668, sawa na asilimia 41.1. Takwimu hizi zinaonesha kuwa hali ya uhalifu ilivyokuwa nchini katika kipindi cha miezi mitatu ya kwanza ya mwaka 2006, wakati Serikali ya Awamu ya Nne, inaingia madarakani na hali ilivyokuwa katika miezi mitatu ya mwisho ya mwaka 2006. Ni dhahiri kwamba, utulivu na amani, hivi sasa vinatawala kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, makosa makubwa ya jinai yamegawanywa katika aina tatu kuu kama ifuatavyo:-

(a) Makosa Dhidi ya Binadamu. Aina hii ya makosa inajumuisha makosa kama vile mauaji, kubaka, kulawiti, kutupa watoto na wizi wa watoto. Katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2006, jumla ya makosa 2,572 yaliripotiwa Polisi, kulinganisha na makosa 2,744 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2005. Kuna upungufu wa makosa 172, sawa na asilimia 6.3.

(b) Makosa Dhidi ya Mali. Aina hii ya makosa inajumuisha makosa ya wizi, unyang'anyi wa kutumia silaha, unyang'anyi wa kutumia nguvu, uvunjaji wa majumba na kuiba, wizi wa magari, wizi wa pikipiki na wizi wa mifugo. Katika kipindi hiki, yaliripotiwa makosa 3,123, ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2005, ambapo yaliripotiwa makosa 4,022. Kuna upungufu wa makosa 899, sawa na asilimia 22.3. Mfano, makosa ya unyang'anyi wa kutumia silaha, yamepungua kwa asilimia 29. Makosa ya unyang'anyi wa kutumia nguvu, yamepungua kwa asilimia 18.3. Hali kadhalika, makosa ya wizi wa magari, yamepungua kwa asilimia 46 mwaka 2006, ukilinganisha na matukio hayo mwaka 2005.

(c)Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii. Aina hii ya makosa inajumuisha makosa kama vile kupatikana na dawa za kulevya, kupatikana na silaha, kupatikana na pombe haramu, kupokea au kutoa rushwa na kupatikana na nyara za Serikali. Katika kipindi hiki, yaliripotiwa makosa 2,435, ikilinganishwa na makosa 1,389 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2005. Mfano, kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2006, tulifanikiwa kwa asilimia 92.2 kukamata wahalifu waliopatikana na silaha, ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2005. Kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2006, tulifanikiwa kwa asilimia 79, kukamata makosa ya kupatikana na bhangi ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2005. Takwimu hizi zinaonesha kazi kubwa iliyofanywa na Jeshi la Polisi, kutokana na ufanisi wake kuongezeka kwa asilimia

75.3. Ufanisi huu umetokana na Polisi kutoka vituoni mwao na kufanya kazi zao mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ajali za barabarani, katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2006, yaliripotiwa matukio 5,906, ikilinganishwa na matukio 6,048 yaliyoripotiwa katika kipindi hicho mwaka 2005. Kuna upungufu wa asilimia 2.3. Kati ya Oktoba na Desemba, 2006, watu 155 walifariki na watu 843 walijeruhiwa, ikilinganishwa na kipindi cha mwaka 2005, ambapo watu 219 walifariki na wengine 1,018 kujeruhiwa. Kuna upungufu wa asilimia 29.2 kwa watu waliofariki na upungufu wa asilimia 17.2 kwa watu waliojeruhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Usalama Barabarani, bado ni tatizo kubwa linalotukabili. Ajali za barabarani, husababishwa na mambo mbali mbali. Hii ni changamoto iliyo mbele yetu na hivi sasa Wizara yangu, inazipitia upya sheria hizo ili kuziboresha, ziendane na hali halisi ya usafiri ilivyo hivi sasa.

Katika maboresho hayo, ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutazingatia maslahi ya Taifa letu, hususan maisha na matarajio ya wananchi. Hivyo, tutahakikisha kwamba, sheria hiyo ina *common sense* ndani yake na inatekelezeka, hasa katika maeneo yenye matatizo makubwa ya usafiri na wananchi hawana njia mbadala. Kwa mfano, usafiri wa abiria wa kawaida, ambao hutumia baiskeli, pikipiki za kawaida na za miguu mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo ni matukio makubwa yaliyotokea:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 16 Desemba, 2006 saa 12.55 asubuhi katika Uwanja wa Ndege wa Mwanjelwa, Mbeya, ndege ndogo mali ya Kampuni ya *TANZANAIR,* ilipata ajali na kuangukia juu ya paa la nyumba. Ndege hiyo ilikuwa na watu sita. Mtu mmoja alifariki papo hapo. Majeruhi walipata majeraha makubwa ya kuungua moto na kuvunjika sehemu mbalimbali za miili yao. Mali za majeruhi ziliokolewa zikiwemo fedha taslimu Sh.1,288,444, bastola moja aina ya *Chinese* na risasi sita.

Kutokana na ajali hiyo, watu wanne wamefariki, akiwemo Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, aliyekuwa akishughulikia Mambo ya Bunge, Marehemu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti. Mwenyezi Mungu, azidi kuwafariji familia, ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu wote. *Amen.*

Majeruhi wawili, Rubani na Katibu wa Waziri, wanaendelea vizuri. Rubani ameruhusiwa kutoka hospitali na Katibu wa Waziri, bado yuko hospitali, akiendelea na matibabu. Chanzo cha ajali hiyo, kinachunguzwa na wataalam wa *Tanzania Civil Aviation Authority*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 16 Desemba, 2006 saa 3.45 asubuhi katika maeneo ya Vingunguti, Dar es Salaam, majambazi watatu wakiwa na bunduki aina ya *SMG* moja na bastola, walipora shilingi milioni 48.4 za *Mohammed Enterprises,* zilizokuwa zikisindikizwa na Askari Polisi wawili, ambapo Askari Polisi mmoja na Mhasibu wa Kampuni hiyo, waliuawa na wengine kujeruhiwa, wakiwemo wapita njia wawili. Majambazi hayo pia yalipora bunduki moja aina ya *SMG,* ikiwa na risasi 30,

iliyokuwa inatumiwa na Askari waliokuwa wanasindikiza fedha. Watu watano wamekamatwa kuhusiana na tukio hilo na kufikishwa mahakamani na kesi yao inaendelea mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 27 Desemba, 2006 saa 6.00 mchana, maeneo ya Temeke, kwenye *yard* ya kuuza vyuma chakavu, vibarua walipokuwa wakipakia vyuma chakavu kwenye malori ili vipelekwe kiwandani Chang'ombe, bomu moja lililipuka na kumuua mtu mmoja na wengine watano kujeruhiwa vibaya.

Baada ya tukio hilo, iliundwa timu, iliyowashirikisha wajumbe kutoka Jeshi la Polisi, Usalama wa Taifa, JWTZ na Mkemia Mkuu wa Serikali. Timu hii ilipewa majukumu ya kuchunguza vyanzo vya mabomu na kiongozi wa tukio lililotokea na kuishauri Serikali hatua za kuchukua ili tukio kama hilo lisitokee tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 15 Januari, 2007, maeneo ya viwanda saba yalikuwa yamekaguliwa kwa kutumia wataalam wa mabomu kutoka Kikosi cha 302 cha JWTZ, ili kupata picha halisi ya kuzagaa kwa mabomu katika viwanda vya kutengeneza nondo. Uchunguzi huo, ulifanikisha kupatikana kwa mabomu, maganda na vifaa kadhaa, vyenye asili ya milipuko. Watu 14 walihojiwa ili kuisaidia timu kuelewa vyanzo mbali mbali vya mabomu hayo.

Katika mahojiano, ilibainika kuwa, mizigo ya vyuma chakavu iliyotoka Mkoani Tabora, ilikuwa na mabomu. Baadhi ya Wajumbe wa timu ya uchunguzi, walienda Mkoani Tabora, kufanya uchunguzi zaidi. Katika mahojiano na watu mbalimbali Mkoani Tabora, waligundua kuwa, wakusanyaji wadogo wadogo wa vyuma chakavu, hujipenyeza kwa siri, kwenye uwanja wa shabaha wa Shule ya Mafunzo ya Kijeshi Kalunde na kukusanya mabomu, wakidhani ni vyuma chakavu, kisha kuwapelekea madalali wa vyuma chakavu, ambao nao huyanunua na kuyasafirisha kwenye viwanda vya nondo. Uongozi wa shule hiyo ya Kijeshi, umeshauriwa kuwatumia wataalam wa mabomu ili kusafisha eneo hilo. Kazi hii inafanywa na *Brigade* ya Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zaidi zilizochukuliwa kudhibiti hali hiyo ni pamoja na:-

Kuwaelimisha wakusanyaji wa vyuma chakavu, madalali na wenye viwanda namna ya kutambua mabomu ili mara wakiyatambua watoe taarifa Polisi. Wataalam wa mabomu kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi wametembelea viwanda vyote vya nondo Jijini Dar es Salaam na kutoa elimu ya namna ya kuyatambua mabomu ya aina mbali mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar, hali ya ulinzi na usalama ni shwari ambapo hivi sasa Jeshi la Polisi limejitahidi kuimarisha doria kwa Askari wa Upelelezi na Askari wa kawaida. Jeshi la Polisi Zanzibar limefanikiwa kukamata silaha moja aina ya *SMG* pamoja na watuhumiwa 13 akiwemo mwanamke mmoja. Silaha hiyo ilitumika katika matukio kadhaa yaliyotokea eneo la Mwera na kuleta hofu kwa wakazi wa eneo hilo.

Aidha, Jeshi la Polisi limefanikiwa kukamata silaha aina ya *SMG* iliyoibwa katika kituo cha Polisi Mwembe Mchomeke. Watuhumiwa wanne waliohusika na wizi huo

wamekamatwa na kufikishwa Mahakamani. Askari Polisi wawili waliokuwa zamu wakati silaha ilipoibwa walishtakiwa kijeshi na kufukuzwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Ulinzi na Usalama mipakani, hasa katika Mikoa ya Kagera na Kigoma inaendelea kuwa nzuri. Jeshi la Polisi limefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokomeza vitendo vya uhalifu hasa katika Mkoa wa Kagera. Silaha na risasi kadhaa zimekamatwa, zikiwemo silaha zilizotengenezwa kienyeji. Kazi ya Kamanda Venance Tossi alipokuwa Dar es Salaam katika Kikosi cha *FFU* bado inakumbukwa na hivyo hivyo alipokuwa *RPC* Kilimanjaro na kazi hiyo nzuri ndiyo anayoiendeleza Mkoani Kagera kwa ujasiri mkubwa. Kwa upande wa Mkoa wa Kigoma, jumla ya silaha 2,771 zilizokuwa zinamilikiwa isivyo halali zilikamatwa na ziliteketezwa hadharani katika uwanja wa *Lake Tanganyika* tarehe 23 Januari, 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kuupongeza Mkoa wa Kigoma na Shirika la Maendeleo ya Umoja wa Mataifa *UNDP* kwa kutekeleza kwa ufanisi mradi wa kufichua silaha ndogo ndogo na nyepesi Mkoani humo. Aidha, nawapongeza kwa kutoa elimu kuhusu sheria ya kumiliki silaha na taratibu zinazotawala uombaji na hatimaye kuweza kupata kibali cha kumiliki silaha. Elimu kama hii siyo tu inawafumbua macho wananchi wengi, bali pia inawapa fursa ya kufahamu kuwepo kwa sheria ya umilikaji wa silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Usalama wa Raia itajitahidi kuhakikisha kwamba kazi ya kuhakikisha kuwa jamii inajiepusha kabisa na silaha haramu inakuwa endelevu ili kujenga Taifa lenye nguvu Kiuchumi, Kisiasa, Kiutamaduni na Kiulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla hali ya Ulinzi na Usalama nchini ni shwari, japo yapo matukio kadhaa ya hapa na pale. Jeshi la Polisi linaendelea kushirikiana vizuri na wananchi pamoja na vyombo vingine vya dola kudhibiti vitendo vya uhalifu kwa kupanga mbinu na mikakati mbali mbali ya kukabiliana navyo.

Jeshi la Polisi litaendelea kufanya operesheni na misako ya mara kwa mara kudhibiti uhalifu. Jeshi litaendelea pia kuhakiki silaha na kukamata silaha zinazomilikiwa kinyume cha sheria pamoja na kushirikiana na vyombo vingine kuwarudisha wahamiaji haramu kutoka nchi jirani zinazotuzunguka.

Hali kadhalika, operesheni maalum dhidi ya madawa ya kulevya inayoendelea nchi nzima inafanyika kwa mafanikio ya kuridhisha. Baadhi ya watu wamekamatwa na taratibu za kuwafikisha mahakamani zinaendelea. Tukio kubwa la hivi karibuni ni la kukamatwa kwa watu 13 waliokuwa wakisafirisha dawa hizo kutoka Zambia kuja nchini kwa kutumia maiti. Mtandao wao ulifuatiliwa na kwa kiasi kikubwa umevunjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuhitimisha Taarifa hii kwa kutoa shukurani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa juhudi zake kubwa za kutusaidia kutatua matatizo mbali mbali ya Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Namshukuru sana Mwenyekiti Mheshimiwa William J. Kusila - Mbunge wa Bahi (Makamu Mwenyekiti), Mheshimiwa George H. Mkuchika - Mbunge wa Newala na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa uzalendo, utayari na

ushirikiano mkubwa wanaouonyesha kwetu. Kamati nzima iko nasi bega kwa bega kuhakikisha matatizo ya Jeshi la Polisi, hasa ya ufinyu wa Bajeti na ukosefu wa vitendea kazi mbalimbali yanatatuliwa kwa kadri hali itakavyoruhusu. Juhudi wanazochukua ni kubwa na zinastahili pongezi nyingi. Tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine, ninakushukuru kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha Taarifa hii na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kuipokea. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani tumeipokea taarifa hii. Ni muhimu kwetu sisi kama Wawakilishi wa Wananchi kujua Serikali inafanya nini katika eneo la Ulinzi na Usalama.

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali *PAC* 2003/2004

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimearifiwa kwamba Kamati ya Uongozi ilipokaa ilikubaliana kwamba Kamati hizi mbili, Wenyeviti wake wasome, aanze Mwenyekiti wa Kamati za Serikali, atafuatiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya hesabu za Serikali za Mitaa, halafu tutajadili kwa pamoja. Utaratibu wa Kanuni utakapofika mwisho, tutaamulia taarifa moja baada ya nyingine. Kwa hiyo, sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali asome taarifa yake. Mheshimiwa John M. Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa mujibu wa Kifungu 88 (11) ya Kanuni za Bunge Toleo la Mwaka 2004 kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kwa mwaka wa bajeti wa 2003/2004 liijadili na kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kutoa salaam za rambirambi kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwako Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, familia, ndugu, wakazi na Wapigakura wa Tunduru kwa kifo cha Mbunge mwenzetu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu aliyekuwa akishughulikia masuala ya Bunge - Mheshimiwa Juma Jamadin Akukweti, kilichosababishwa na ajali ya ndege. Marehemu atakumbukwa daima kwa uchapakazi na uadilifu wake, kwa moyo wake wa kujituma na kwa uongozi wake wa mfano. Bwana alitoa na Bwana ametwaa. Mapenzi yake yatimizwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba yangu binafsi na ya Wajumbe wa Kamati, tunawapongeza Wabunge wenzetu walioteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, nao ni Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja na Mheshimiwa Gaudense Cassian Kayombo. Tunawatakia mafanikio makubwa katika kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba yangu binafsi na ya Wajumbe wote wa Kamati, naomba kumpongeza Mheshimiwa, Dr. Asha-Rose Migiro, Mbunge, kwa

kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Hii ni heshima kubwa kwa Taifa na Bunge letu na zaidi kwa wanawake wote wa Tanzania. Tunamtakia utumishi uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya Wajumbe wa Kamati yangu uliyoiunda kwa mujibu wa Kifungu 94(1)(2004) cha Kanuni za Bunge ni 13. Naomba Bunge lako Tukufu liwatambue kwa kutaja majina yao kama ifuatavyo:-

Mimi mwenyewe Mheshimiwa, John M. Cheyo - Mwenyekiti, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma A. Fereji, Mheshimiwa Felista A. Bura, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Zubeir A. Maulid, Mheshimiwa Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Pansiano D. Nyami na Katibu wetu Ndugu James J. Warburg.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru Wajumbe wote kwa kazi nzuri waliyoifanya wakati wa vikao vyote vya Kamati ya kufanya uchambuzi wa kina na kutoa michango na maoni mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Kamati ilipokuwa ikichambua na kujadili mafungu (votes) mbalimbali ya Serikali, Mikoa na Idara zinazojitegemea kwa kiwango kikubwa michango yao imesaidia kujenga dhana ya kuwepo nidhamu ya matumizi ya fedha na mali za Serikali kulingana na sheria, taratibu na kanuni zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati katika kutekeleza kazi zake ilikuwa ikiongozwa na Maafisa Waandamizi kutoka Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mhakiki Mkuu wa Mali za Serikali, na Sekretarieti ya Ofisi ya Katibu wa Bunge. Nawashukuru sana kwa mchango wao wa kitalaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka kutumia nafasi hii kumpa pongezi Ndugu yetu Ludovick Utto kwa kuteuliwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali badala ya Ndugu T. M. Kihama ambaye amestaafu. Tunamtakia kazi njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Kamati imefanywa kwa misingi mbalimbali. Msingi wa kwanza ni wa Katiba ya Tanzania Ibara ya 63, nanukuu: “Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekerezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa katiba hii.”

Mheshimiwa Naibu Spika, Moja wa majukumu makuu ya Serikali ni kukusanya kodi na fedha kutoka vyazo mbalimbali na kutumia fedha hizo kama vile Bunge lako Tukufu lilivyoidhinisha katika kikao cha Bajeti. Kazi yetu kama Bunge ni kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Bunge lako Tukufu linatekeleza jukumu hili kwa kutumia Kamati mbalimbali. Kazi ya Kamati ya Hesabu za Serikali ni kukagua mahesabu ya Serikali (financial audit) na utekelzaji wa malengo ya bajeti (performance audit).

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri Waheshimiwa Wabunge wajielekeze kwenye sura ya saba ya Katiba Ibara ya 133 mpaka 144 (Masharti kuhusu Fedha za Jamhuri ya Muungano) na kwa msisitizo mambo yafuatayo:-

Fedha za Serikali haziwezi kutumika bila sheria iliyotungwa na Bunge (Ibara ya 136), hakuna kodi ya aina yoyote itakayotozwa isipokuwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge (Ibara ya 138), majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikeli (Ibara ya 143) ambayo ni pamoja na kuhakisha kwamba fedha zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa matumizi yaliyoidhinishwa na Bunge na angalau mara moja kwa mwaka kukagua mahesabu yote ya Serikali pamoja na Bunge na kupeleka taarifa ya ukaguzi kwa Rais, ambaye anawajibika kuwaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye Kikao cha kwanza kitakachofanyika baada ya Rais kupokea hiyo taarifa na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kikao kilipoanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Katiba katika eneo hili umepewa nguvu ya kisheria katika Sheria ya Fedha (Public Finance Act No.6) kama ilivyorekebisha mwaka 2004. Tunashauri Waheshimiwa Wabunge wajielekeze zaidi kwenye sehemu ya nne hadi ya saba ya sheria hii. Sheria inasisitiza kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anafanya kazi yake ya ukaguzi kwa niaba ya Bunge. Tunanukuu kifungu 31 (1): "The Controller and Auditor General shall on behalf of the National assembly examine, inquire into and audit the accounts submitted to him under section 25 of this Act and perfom any other functions which he is authorized to perform by or under this Act."

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria katika Ibara ya 44 kifungu cha (2) inatoa nguvu ya kisheria kwa yeyote yule atakeyekataa kutoa taarifa au ushirikiano na Bunge hili kupitia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anaweza kufungwa mpaka miaka miwili, kupewa faini ya Shilingi laki tano ama vyote viwili kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la Kamati za Bunge pia linatokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Toleo la 1977 Ibara ya 96(1) kama inavyonukuliwa hapa: "Bunge laweza kuunda Kamati za Bunge la namna mbalimbali kadri litakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake."

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 96 (2) ya Jamhuri ya Muungano inaeleza kuwa: "Kanuni za Bunge zaweza kufafanua muundo na Shughuli za Kamati za Bunge." Hivyo kwa mujibu wa Kifungu hiki, majukumu ya Kamati ya Hesabu za Serikali yameainishwa katika Kanuni za Bunge (2004) Kifungu 94(2):- Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu kuhusu Hesabu za Serikali, kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ya kuondoa matatizo husika ili yasionekane tena katika taarifa zitakazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni zilizotengenezwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha chini ya Sheria ya Fedha (Public Finance Act, 2001 No.6 of 2001) Sehemu ya Pili zimeelezea uwajibikaji wa Maafisa Wahasibu kwa Kamati ya Hesabu za Serikali [(Public Accounts Committee (PAC)] na tunanukuu: "Every Accounting Officer shall be personally and pecuniarily responsible and accountable for the collection and receipt of

all revenue or for all disbursements of expenditure in his vote and shall be answerable to the Public Accounts Committee (PAC)."

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Fedha inamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali (Paymaster General) kuteua Afisa wa Serikali atakayewajika kwa fedha za Serikali katika eneo lake la kazi. Jukumu hili ni binafisi (personal responsibility) na sheria pamoja na kanuni (regulations) zina elekeza kwamba Afisa Mhasibu atawajibika binafsi (personally held responsible Ref. Ibara ya 5 ya Kanuni): "Any Accounting Officer who authorizes or approves the use of public funds or property contrary to the provisions of the Act shall be accountable for any loss arising from that use and shall be required to make good the loss or be surcharged under these Regulations, even if he has ceased to hold that Office. In exercising his duties under these regulations, the Minister shall have power to:

(a) *Upon the recommendation by the Public Accounts Committee, surcharge any accounting officer or any public office as prescribed under the schedule of these regulations;*

*(b) Withdraw the appointment of any accounting officer upon the recommendation by the Paymaster General, where gross negligence in the performance of his duties has been proved by the Controller and Auditor General and confirmed by the Public Accounts Committee (PAC).*

Kwa msingi huu, kila Afisa Mhasibu anawajibika kufika mbele ya Kamati ya Bunge na kutetea utekelezaji wa bajeti ya fungu lake na anaweza kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa pili ni mikataba ya kifedha ya kimataifa. Bajeti ya nchi yetu inategemea mchango wa kutoka nje. Fedha hizi ni misaada kutoka inchi rafiki, misaada na mikopo yenye riba nafuu kutoka kwa mfano Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Benki ya Dunia (WB). Fedha zote hutawaliwa na mikataba inayoitaka Serikali kutumia hizi fedha kwa makusudi na maeneo yaliyokubaliwa na kuidhinishwa na Bunge. Msingi huu unalitaka Bunge lako Tukufu kuwa makini katika kusimamia matumizi ya fedha hizi. Kazi ya Kamati yetu ni kuhakikisha kwamba Serikali inawajibika kwa matumizi ya fedha hizi. Kazi hii ya Bunge kupitia Kamati hii inawapa washiriki wetu katika maendeleo ya nchi yetu (development partners) imani ya uwajibikaji wa fedha za walipa kodi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa iliyowasilishwa na Kamati kwenye meza yako ni muhimu sana katika kuonyesha utekelezaji wa jukumu la Bunge la kuisimamia Serikali kutekeleza jukumu lake la kibajeti. Wadau mbalimbali nchini na nje ya nchi wanategemea ni jinsi gani na kwa ufanisi gani Bunge lako Tukufu linaweza kuisimamia Serikali kibajeti. Taarifa hii itasaidia kuonyesha mapungufu yaliyomo katika mfumo mzima wa utekelezaji wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Kamati tumefanya kazi kwa kuweka mbele utaifa wetu na wananchi wetu na wa nje wanaogharamia matumizi yote ya Serikali kwa kujikamua kikodi au kulipia mikopo mbalimbali. Kwa fedha za walipa kodi kuna itikadi moja tu nayo ni uwajibikaji kwa matumizi ya fedha za Bajeti. Matumaini ya Kamati ni kwamba Bunge litakemea matumizi mabaya na kubariki mapendekezo ya Kamati na pia Bunge litasifu Maafisa Wahasibu pale inapostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu, taarifa inayofuata hapa chini ina sehemu tano zinazojikita; mosi, kwenye masuala ya ujumla; pili, udhaifu wa utunzaji wa nyaraka na athari zake; tatu, taarifa za baadhi ya mafungu yenye masuala yanayostahili kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu; nne, mapendekezo na mwisho hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemeu ya Pili ni masuala ya ujumla kuhusu Bajeti ya Taifa: Sasa naomba kujielekeza kwenye eneo la mahusiano baina ya Serikali na Bunge kuhusiana na taratibu za uandaaji wa Bajeti ya Taifa. Bajeti hutayarishwa na Serikali ambayo huiwasilisha Bungeni kwa ajili ya kupata kibali. Mapungufu makubwa mawili yaliyopo ni: Moja, kutokuwepo ushiriki mpana wa Bunge na wananchi kwa ujumla kuitayarisha bajeti yenyewe ikiwemo misingi, vipaumbele na miongozo yake. Hata inapowasilishwa Bungeni, Bunge huwa haliwezi kubadili chochote. Mamlaka ya Bunge kwa hali hii haipo. Bunge linafanya ukaguzi wa hesabu ambazo halikuwa na uwezo wa kubadilisha chochote. Kamati inapendekeza hali hii irekebishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Bajeti ya Serikali ina pande au sura mbili:- mapato na matumizi. Mapato pia yako ya aina mbili: ya ndani na ya nje. Kamati imegundua kwamba Maafisa Wahasibu huwa wanawajibika sehemu mbili pia kuhusiana na jinsi wanavyotumia fedha zinazotoka sehemu hizi mbili: kwa Bunge na kwa Wafadhili ama Wahisani *(double accountability routes)*. Hali hii sio nzuri hata kidogo kwa kuwa, kwa upande mmoja *TRA* wanaposhindwa kukusanya mapato kama wanavyotarajiwa huwajibishwa lakini sio wafadhili wanaposhindwa kutoa fedha kama walivyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa katika mafungu mengi iliyoyajadili, Fedha za Maendeleo zinazoahidiwa kutolewa na Wahisani, zimekuwa zinatolewa aidha, siyo kwa viwango vilivyoahidiwa au hata kama zinatolewa ni kwa kiwango kidogo na huidhinishwa mwishoni mwa mwaka wa fedha husika au fedha hizo hazitolewi kabisa. Kamati imebaini mapungufu haya yamekuwa yakisababisha mkanganyiko wa Bajeti Kuu ya Serikali inayopitishwa na Bunge na hivyo kuvuruga mipango ya maendeleo iliyotarajiwa kutekelezwa na kusababisha hoja nyingi za ukaguzi.

Kamati inashauri kuwa ingekuwa vyema iwapo kungekuwepo na uwajibikaji wa upande mmoja tu, kwa Bunge (*domestic accountability*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Mhasibu Mkuu wa Serikali, Kamati ilipotembelea Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na kupata taarifa za utendaji wake kazi imegundua mapungufu makubwa ya msingi. Ofisi ya Mdhibiti Mkuu wa Serikali kimsingi na kiutendaji haiko chini ya Wizara ya Fedha.

Ofisi hii inawajibika kutoa taarifa yake moja kwa moja kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia kwa Rais anayempa Waziri wa Fedha kuwasilisha Taarifa hiyo Bungeni. Wajumbe walipatwa na hisia tofauti juu ya uhuru na *Autonomy* ya Ofisi hii na kushauri ni vyema Sheria inayounda chombo hiki ikafanyiwa rejea ili ifanyiwe mapendekezo ya kuifanyia marekebisho yatakayoipa nguvu za kisheria, kiutendaji bila ya kuingiliwa na chombo chochote.

Upungufu mwingine ni uwezo *(capacity)* wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kukagua Taarifa za Hesabu za Serikali na Taasisi zote za Umma. Kutokana na udhaifu huu, Ofisi hii imelazimu kuzipa Taasisi za Umma uwezo wa kisheria kuteua Wakaguzi binafsi kufanya Ukaguzi wa Taarifa za Hesabu za Taasisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 13 Machi 2006 Kamati ilipata fursa ya kutembelea Ofisi ya Mlipaji Mkuu wa Serikali ambapo Wajumbe walitembelea vitengo mbalimbali vya Idara hiyo zikiwemo mitambo ya mtandao wa Uhasibu na mfumo mzima wa malipo ya Serikali inayotumika kwa kuunganishwa kati ya Ofisi ya Mlipaji Mkuu wa Serikali na Wizara zote. Aidha, Wajumbe walipata maelezo juu ya udhibiti na matumizi na ulipaji wa fedha za Serikali kwa mfumo wa mtandao huo ujulikanao kama *Intergrated Financial Management System (IFMS).* Naye Ofisa Mlipaji Mkuu wa Serikali aliwajulisha Wajumbe mikakati mbalimbali inayochukuliwa na Ofisi yake ya jinsi ya kukabiliana na wizi wa fedha za Serikali unaotumika katika mitandao ya teknolojia ya kisasa. Vitengo vilivyotembelewa ni pamoja na Kitengo cha Madeni ya Taifa, Madeni ya Mashirika na Watu binafsi ya Ndani ya Nchi, Mikopo, Malipo ya Hundi na mishahara ya Watumishi wa Serikali na Kitengo cha Pensheni.

Kamati iliagiza yafuatayo kwa Ofisi zote mbili, suala la Ulinzi na Usalama katika Mtandao wa Malipo ya Serikali, vifaa, Majengo ilichukuliwa kwa uzito wa hali ya juu ili kuondokana na mianya inayoweza kupelekea kutendeka vitendo vya wizi, suala la Elimu kwa Watumishi na *Package* ya malipo kama motisha kwa Wafanyakazi izingatiwe ili kuepusha Watumishi kuwa na tamaa ya kujiingiza katika vitendo viovu vya Wizi na kuwajengea maadili mazuri *(integrity)* katika Utendaji wa kazi zao; udhibiti na Ukaguzi wa fedha na mali za Serikali na *performance and physical audit* ufanyike ili kuona matumizi halisi ya fedha za Serikali *(value for money);* Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ahusishwe katika kuhakiki mali hizo, au pale mali hizo zinapouzwa ili kupata thamani kamili ya mali hizi kisheria na Kihasibu katika vitabu vya mahesabu; Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali katika maeneo ya uwezo kiteknolojia iende sambamba na ya Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ili teknolojia inayotumika katika Ofisi ya Malipo iweze kukaguliwa; na uongozi wa Ofisi hizi mbili ni vyema ukafanya vikao na majadiliano ya pamoja ili kupata mwelekeo ni kwa jinsi gani hatua za kuboresha hali ya utendaji zitakavyochukuliwa.

Pia Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu Serikali aratibu mipango ya kujenga uwezo wa kutekeleza majukumu yake itakayoanisha uwezo kifedha na kuainisha matatizo, matazamio ya sasa na kwa siku zijazo *(strategic plan);* Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ipewe mamlaka kamili ya kuajiri watumishi wenye sifa bila kufungwa na nyaraka na taratibu za Idara ya Utumishi Serikalini na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iidhinishiwe mgao wa fedha kupitia fungu 45 wa kutosha kufanya kazi zake. Kwa muda mrefu Ofisi hii imekuwa ikipewa fedha kidogo ikilinganishwa na majukumu yake ya Kikatiba na matokeo yake Ofisi hii imekuwa tegemezi kwa wateja wake inaowakagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokuwa ikijadili Taarifa ya Utendaji na Hesabu za Mafungu ya Mikoa, ilibainika kuwepo kwa *Double Accounting System* katika utoaji wa fedha za maendeleo pale zinapopelekwa moja kwa moja kwenye Halmashauri mbalimbali hapa nchini na baada ya kutumika fedha hizo nyaraka zote Kihasibu hupelekwa kwa Afisa Mhasibu wa Mkoa anayewajibika kuzitolea maelezo *(Account for)*

kwa *PAC* na Afisa Mhasibu wa Halmashauri *(DED)* anawajibika kuzitolea maelezo kwa Hesabu hizo hizo kwa LAAC.

Hali hii imesababishia Maafisa Wahasibu wa Mikoa kutokuwa na maelezo na nyaraka za matumizi ya fedha hizo, hivyo kubaki vitabu kama hoja za ukaguzi na hatimaye kupata Hati zenye dosari za Ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha ulioshia June 30, 2004 kulikuwa na jumla ya malipo ya Shilingi bilioni 58.646 ambayo hayakuwa na nyaraka ama yalikuwa na nyaraka pungufu.

Kutokana na uchambuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, katika taarifa yake Hesabu za mpaka Juni 30, 2004, Kamati ilibaini kuwa malipo yenye thamani ya Shilingi bilioni 5.034 hayakuwa na nyaraka kabisa, ikilinganishwa na malipo ya aina hiyo kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2003 yaliyofikia Shilingi bilioni 49.927. Kati ya hizo, malipo ya Shilingi bilioni 5.963 hayakuwa na nyaraka kabisa. Hali hii inaonyesha kuwa kumekuwa na ongezeko la kulipa malipo bila nyaraka badala ya kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa hesabu zinazoishia June 30, 2004 ulioko katika ukurasa wa 25 hadi 27 kiambatanisho Na.IV ya kitabu cha taarifa yake unaonyesha kuwa, katika malipo yasiyo na nyaraka na yenye nyaraka pungufu ya jumla ya Shilingi bilioni 58.6, Shilingi bilioni 56.97 zinatokana na mafungu ya Wizara na Shilingi bilioni 1.676 ni za mafungu ya Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa nyaraka za malipo kama vile *Payment Voucher*, Risiti, *LPO* na *Invoice* kunaashiria kuwepo kwa malipo yasiyo halali, matumizi mabaya ya fedha za Serikali, wizi na kupingana na kanuni ya sheria za fedha 86(1) inayowataka Maafisa Wahasibu wasitumie fedha za Serikali kulipia huduma au matumizi yoyote bila kuambatanishwa na nyaraka zote muhimu zinazoelezea malipo yanayofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafungu mengi ya Wizara na Mikoa yamekuwa yakipata hati chafu, hati zenye masharti na hati ambazo hazina maoni/maelezo na kutokana na Maafisa wa hesabu kuwa na usimamizi na utunzaji mbaya wa nyaraka za malipo au kufanya malipo makubwa yenye nyaraka pungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia hesabu za mwaka unaoishia June 30, 2004 Kamati ilibaini kuwa matatizo ya kukosa nyaraka zinazohitajika kuhalalisha malipo au kuthaminisha mali kunatokana na mambo yafuatayo:-

- Uzembe wa Maafisa Wahasibu wa kutokutunza nyaraka muhimu za mapato na matumizi na ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha kama nyaraka zote zipo wakati wa ukaguzi;

- Kufanya malipo nje ya nchi kupitia Balozi kwa ajili ya matibabu na malipo ya wanafunzi wanaolipiwa na Serikali bila kurejesha nyaraka zilizotumika kulipia malipo hayo;

- Kukosekana kwa nyaraka za malipo kunatokana pia na wafadhili na miradi wanapokamilisha miradi na kuondoka bila kuacha michanganuo ya gharama za miradi na nyaraka zake;

- Makusanyo ya maduhuli hufanywa bila kutumia risiti za Serikali kitu ambacho ni kinyume na sheria za fedha;

- Maafisa Ugavi kuwa na uwezo mdogo wa kujua umuhimu wa kutunza nyaraka za manunuzi ya vifaa na mali za Serikali; na

- Maafisa Wahasibu walio wengi hawako karibu na Wahasibu Wakuu na Maafisa Ugavi wa mafungu yao katika kuhakikisha kuwa nyaraka zote zinakuwepo wakati wa ukaguzi na baada ya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa malipo na manunuzi yote yameidhinishwa kihalali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuna matatizo yanayojitokeza wakati wa Ukaguzi na kupelekea kuwa na kiwango kikubwa cha hoja za kukosa nyaraka. Matatizo haya ni kama yafuatayo:-

- Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kipindi kilichoishia June 30, 2004 haikuwa na uwezo wa kufanya ukaguzi kwa kutumia kompyuta. Kwa hiyo, baadhi ya nyaraka walizozihitaji ilikuwa siyo rahisi kuzipata. Kwa mfano, hati za usuluhisho wa Benki unaofanywa kwa ujumla na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa kutumia mtandao wa *IFMS*;

- Usuluhishi wa Hesabu *(Bank Reconciliation)* kumekuwa na mkanganyiko wa usomaji au uelewa wa Maafisa Wahasibu kuona mapungufu ya nyaraka zinazohakikiwa kwenye Hesabu za mapato na matumizi kwa kuwa usuluhishi hufanywa na Hazina kwa ujumla bila kuonyesha *Individual Bank Reconciliation.* Hali hii inafanya Afisa Mhasibu asione dosari katika fungu lake husika, hali ambayo inasababisha kuwe na hoja ya upungufu wa nyaraka;

- Uwezo wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali wa kukagua Taasisi zinazotumia kompyuta kutayarisha hesabu zake ni mdogo, kwa hiyo, imepelekewa kujitokeza kwa hoja ya upungufu za nyaraka; na

- Utarabibu uliopo na kupeleka pesa moja moja kwenye Halmashauri na uwajibikaji wa kuwasilisha nyaraka kufanywa na Sekretariati ya Mkoa umeleta ugumu katika utunzaji wa nyaraka za malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo hapo juu yanathibitisha hali na picha halisi isiyoridhisha katika hesabu kwa mafungu yote ya Wizara, Idara, Asasi za Serikali na Mikoa ambayo imeonyeshwa kwa ufasaha na michanganuo ya kina katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka 2003/2004 iliyowasilishwa Bungeni mapema mwaka 2006. Mapungufu ya nyaraka yamepelekea kuwepo kwa dosari nyingi za kihasibu na za kiutendaji katika Serikali zilizosababisha kujitokeza Hoja za Ukaguzi katika Mafungu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mafungu yote yaliyojadiliwa na Kamati, hoja nyingi za ukaguzi zilihusisha dosari zifuatazo:-

- Kuwepo maduhuli yasiyokusanywa *(arrears of revenue)* Shilingi bilioni 20.731;

- Malipo ya mashaka Shilingi bilioni 58.646 na Shilingi bilioni 5.034 bila nyaraka kabisa;

- Malipo yaliyofanywa kwa kutumia ankara kifani *(Profoma Invoices)* Shilingi bilioni 2.581;

- Mali na vifaa kutorekodiwa vitabuni;

- Upotevu wa fedha taslimu, mali na vifaa mbalimbali Shilingi milioni 506, fedha taslimu na Shilingi milioni 32.06 vifaa;

- Kuwepo malimbikizo makubwa ya masurufu na mikopo isiyorejeshwa (Shilingi bilioni 7.851 ambapo Shilingi bilioni 4.348 ni za Wizara tatu);

- Kutofanyika kwa masahihisho ya hesabu za Benki na vitabuni;

- Kudhibiti dhaifu wa ndani katika kufuata taratibu za manunuzi na utunzaji wa mali;

- Vifaa vilivyolipiwa na havikuletwa Shilingi bilioni 13.119;

- Vifaa vilivyonunuliwa bila *Tender Board* Shilingi bilioni 10.231; na

- Vifaa ambavyo havikuwekwa vitabuni Shilingi bilioni 6.039.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mapungufu haya, ni dhahiri wengi wa Maafisa Wahasibu wamekuwa wakikiuka Sheria za Fedha ya mwaka 2004 na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2003/2004 katika jumla ya mafungu *(Appropriated)* yote 81, mafungu 75 yaliyohusu Amana na Maendeleo yalikaguliwa na Wakaguzi. Kati ya mafungu hayo, yapo yaliyopata hati safi za ukaguzi, hati zenye dosari na hati zisizo na maoni kama inavyoonyeshwa hapa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo huu unaonyesha kuwepo na ufanisi kwa baadhi ya mafungu na nia kubwa ni kuyafanya mafungu yote kupata hati safi ya ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mafungu yote yaliyopata hati safi ya ukaguzi, Kamati ilitoa pongezi kwa Maafisa Wahasibu wote husika na kwa mafungu yaliyopata hati yenye dosari na zisizo na maoni, Kamati iliwaagiza Maafisa Wahasibu wote kujitahidi kupata hati safi ya Wakaguzi katika miaka ya mbeleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha, Maafisa Wahasibu wote wanawajibika kuwasilisha hesabu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kila ifikapo tarehe 31 Oktoba ya kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maduhuli yasiyokusanywa *(Arears of Revenue)*. Kamati inasisitiza Maafisa Wahasibu wote waimarishe mikakati ya ukusanyaji maduhuli na kufikia malengo yanayowekwa. Aidha, ni jukumu la Wizara ya Fedha kuwafuatilia Maafisa Wahasibu wote katika kutekeleza jukumu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo yasiyokuwa na nyaraka na yenye nyaraka pungufu *(Unvouched and improperly vouched expenditure)*. Malipo yasiyokuwa na nyaraka na yenye nyaraka pungufu kwa mwaka 2003/2004 yalikuwa Shilingi milioni 58,646 ambapo kati ya hizo Shilingi milioni 5,034 yalikuwa hayana nyaraka kabisa, ikilinganishwa na malipo ya aina hiyo kwa mwaka 2002/2003 yaliyofikia Shilingi bilioni 49.927 na ambapo kadi ya hizo Shilingi bilioni 5.963 na nyaraka zake zilikosekana kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Maafisa Wahasibu wamekuwa hawarekodi na kutunza kumbukumbu za watumishi wao waliokuwa wamechukua mikopo au masurufu kwa ajili ya shughuli za kiofisi. Hali hii inaonyesha ni kwa jinsi gani Maafisa Wahasibu wasivyokuwa makini katika matumizi ya fedha za umma na Sheria ya Fedha inavyotamka. Kamati inashauri Maafisa wote waliohusika na dosari hizi wawajibishwe kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo yaliyofanywa kwa kutumia ankara kifani *(Payment made on Profoma Invoices).* Haya ni malipo yanayofanywa kwa kutumia ankara kifani pasipo kuambatishwa na nyaraka na vielelezo kwa ajili ya malipo hayo. Hivyo katika mwaka 2003/2004 malipo ya aina hii yalikuwa ya jumla ya Shilingi bilioni 2.581.

Mheshimiwa Naibu Spika, Udhibiti dhaifu wa ndani katika manunuzi wa mali/vifaa *(weak controls over procurement of goods/services and poor Assets Management)*. Udhibiti dhaifu katika kufanya manunuzi na kutorekodi vitabuni shughuli za ugavi kumesababisha hasara ya fedha nyingi katika mafungu mbalimbali ya Serikali. Taarifa za Ukaguzi zimeonyesha katika mwaka 2003/2004. Matumizi yenye dosari ya aina hii ni kama ifuatavyo;-

- Jumla ya Shilingi bilioni 13.199 zililipwa na bidhaa kutopokelewa;
- Manunuzi ya mali na huduma yenye thamani ya Shilingi bilioni 10.231 yalifanyika bila kibali cha *Central Tender Board;* na
- Mali na vifaa visivyorekodiwa vitabuni Shilingi bilioni 6.039.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ya udhibiti dhaifu wa ndani katika kufanya manunuzi unafanywa na baadhi ya Maafisa Wahasibu.

- Malipo yaliyofanywa na bidhaa kutopokelewa Shilingi bilioni 13.199;
- Manunuzi yaliyofanywa bila kibali maalum Shilingi bilioni 10.231;
- Mali na vifaa usivyorekodiwa vitabuni, Shilingi bilioni 6.04; na

- Malipo yenye shaka, Shilingi bilioni 2.125 na *US$* 92,948.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa katika baadhi ya mafungu, fedha za Umma zimetumika na kuisababishia Serikali hasara kwa matumizi ya mali au huduma dhaifu isiyolingana na thamani ya fedha zilizotumika. Jumla ya Sh 2.125 billioni na *USD* 92,948 zilitumika kusababisha kuwepo na dosari ya aina hii kwa baadhi ya mafungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za Ukaguzi zilizotokana na mapungufu hayo kwa baadhi ya Maafisa Wahasibu wameweza kuzijibu na baadhi yao kushindwa kuzijibu na hivyo kupelekea kupata hati isiyo safi ya Ukaguzi. Kamati imekemea kwa uzito unaostahili na kutoa karipio kwa kila Afisa Mhasibu kujitahidi kuzuia kujitokeza hoja za Ukaguzi kwa kutekeleza kazi zao kwa kuzingatia Sheria ya Fedha na Manunuzi, Kanuni na taratibu zilizopo. Aidha, Kamati imewaagiza Maafisa Wahasibu wote waimarishe miundo ya Idara zao za Uhasibu, Vitengo na Sehemu za Ukaguzi wa Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mafungu yalikuwa na hoja nyingi za Ukaguzi na Maafisa Wahasibu husika kukamilisha kuzijibu hoja hizo. Hata hivyo, Kamati hairidhiki na hali hii na imetoa angalizo kwa Maafisa Wahasibu wote kuwa umahiri wa kufanyakazi nzuri usiwe wa kujibu hoja, bali kazi nzuri iwe ya kuzuia hoja kwani hali hiyo ndiyo itakayodhihirisha ufanisi mzuri na kwamba fedha za umma zinatumika kama ilivyokusudiwa na wananchi wanafaidika na kodi zao katika kuleta maendeleo yao *(value for money)* na kwamba Sheria zinazosimamia kazi zao zinafuatwa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne ni taarifa za mafungu maalum. Kamati ilipopitia na kujadili taarifa za utendaji na hesabu za mafungu mbalimbali, imechagua mafungu kadhaa na kuyatolea taarifa hapa. Kamati ilibaini baadhi ya mafungu yamekuwa yakikabiliwa na hoja sugu za ukaguzi ambazo baadhi zimekuwepo vitabuni kwa muda mrefu na zinahitaji kuchukuliwa hatua mahsusi katika kuzipatia ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu 22, Hesabu za Taifa *(National Accounts)*: Kamati yangu imegundua kuwa kuna upungufu wa ufanisi kuhusiana na uendeshaji wa Mfuko Mkuu wa Serikali *(Consolidated Fund Service),Miscellaneous Deposit Accounts, Public Debt and General Services*. Baadhi ya mapungufu haya ni pamoja na yafuatayo:-

- Hazina ilitoa fedha zaidi *(excess votes)* kwenye baadhi ya mafungu kuliko ilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha Shilingi bilioni 31.4;

- Kamati inamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinatolewa kama zilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kama sheria inavyotaka;
- Kuwepo makusanyo duni ya fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa mfano, Serikali ilikusanya/ilipata jumla ya Shilingi bilioni 648.6 mpaka tarehe 30 June, 2004 ikilinganishwa na makadirio ya Shilingi trilioni 1.198 ambayo ni pungufu kwa Shilingi bilioni 549.2, ambayo ni asilimia 45.85 tu ya fedha zilizoidhinishwa na Serikali. Kamati inaona hali hii sio nzuri hata kidogo upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hii ina maana

kwamba zaidi ya nusu ya miradi ya maendeleo iliyopangwa haikutekelezwa;

- Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 Serikali, chini ya mpango wa *Revenue Retention Scheme*, makusanyo halisi yalikuwa Sh 78.5 bilioni kutoka kwenye Wizara na Idara mbalimbali. Kati ya kiasi hiki, jumla ya Shilingi bilioni 46.49 zilirudishwa kwenye Wizara na Idara husika na Hazina na kiasi kilichobaki (Shilingi bilioni 32.0) kilihamishiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali;

- Kamati imebaini kuwa kuna baadhi mafungu yaliyobakiza fedha chini ya utaratibu huu zaidi ya viwango vilivyoruhusiwa (kinyume na kanuni za *retention*) hadi kufikia ziada ya Shilingi bilioni 13.04. Udhibiti wa kiasi ambacho Wizara na Idara zinakusanya na hatimaye kubakisha kwa matumizi yao ni mdogo. Hali hii husababisha Wizara na Idara kubakisha fedha nyingi ambazo hutumika kinyume na bajeti iliyoidhinishwa. Kamati ina maoni kuwa, Hazina waweke utaratibu usioweza kuyumbishwa na kuwa na ufuatiliaji ili hali hii isijirudie;

Udhaifu mkubwa na unaojirudia mwaka baada ya mwingine wa Hazina kutokufanya usuluhishi wa kibenki kwa muda na kwa umakini katika akaunti mbalimbali za Serikali. Kuna baadhi ya akaunti ambazo usuluhishi wake haujakamilishwa toka mwaka 2000. Tukianza na Mfuko Mkuu wa Serikali *(CSF),* taarifa ya usuluhishi wa kibenki hadi tarehe 31 Desemba, 2004, ulikuwa na fedha ambazo hazijasuluhishwa tokea mwaka 2000/2001;

- Kulikuwepo tatizo la usuluhishi katika mahesabu ya akaunti za matumizi ya kawaida kwa Mafungu 19 mbalimbali yenye tofauti ya Shilingi milioni 81.1;

- Akaunti ya Amana imekuwa na tatizo la kutokuwa sahihi katika mwaka wa 2003/04. Salio lilitakiwa liwe Shilingi bilioni 15.27 badala ya kile kilichoandikwa cha Shilingi bilioni 13.6. Cheki zilizochacha zenye kiasi cha Shilingi bilioni 1.67 hazikuwa zimeingizwa kitabuni;

- Kulikuwepo pia tatizo la usuluhishi katika mahesabu ya akaunti za maendeleo kwa Mafungu 21 mbalimbali. Kamati inaitaka Hazina ifanye juhudi kubwa *(as a matter of urgency)* katika kurekebisha kasoro hizi;

- Hesabu za Mfuko wa barabara zinaonyesha kwamba mapato jumla yalikuwa Shilingi bilioni 67.9 mpaka tarehe 30 Juni, 2004. Kati ya hizi, Shilingi bilioni 44.1 zilipelekwa Wizara ya Ujenzi, Shilingi bilioni 18.9 zilipelekwa *PORALG* na Shilingi bilioni 4.87 zilihamishiwa kwenye Mfuko Mkuu kinyume na sheria. Kamati haikuridhishwa na maelezo ya Serikali, kwa nini Shilingi bilioni 4.87 hazikupelekwa kwa watumiaji, yaani Wizara ya Ujenzi na *PORALG* kama sheria inavyotaka. Kamati inaamini kuwa fedha hizi zingetolewa kama inavyotakiwa, barabara nyingi, hasa za Vijijini zingeboreshwa. Kamati inaagiza Hazina isitumie

fedha hizi kwa matumizi mengine na hizi fedha siku za usoni, izipeleke zinakotakiwa;

- Serikali iliongeza deni kwa Taifa kwa Shilingi bilioni 689.7 ikilinganishwa na mwaka uliopita kutoka Shilingi trilioni 5.87 hadi Shilingi trilioni 6.56;

- Katika mwaka wa fedha 2003/2004 Serikali haikuweza kulipa jumla ya Shilingi bilioni 323.28 kama miadi iliyoiva *(unpaid callable commitments)* kwenye mashirika mbalimbali ya kimataifa. Kamati ina maoni kuwa kutolipa miadi hii kwa wakati ni kutokuonyesha uungwana wetu kama Taifa. Serikali iwe inajitahidi kadiri inavyowezekana kutimiza wajibu wetu wa kimataifa na hasa kwa miaka ijayo, ikizingatiwa kuwa nchi yetu imetoa Naibu katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa;

- Serikali pia haikuweza kutayarisha na kuwasilisha kwa ukaguzi taarifa juu ya mwenendo na ushughulikiaji wa *Treasury Bills, Government Bonds and other Securities of the Government* kwa mwaka 2003/04 ambazo ni muhimu katika kuiwezesha Serikali kuziba pengo la fedha inazohitaji kudhibiti ujazo wa fedha katika uchumi. Serikali kushindwa kufanya kazi hii ni udhaifu ambao uliikosesha Kamati na Bunge lako Tukufu fursa ya kuishauri Serikali juu ya vigezo na viashiria hivi vya uchumi. Kamati inaitaka Hazina kutayarisha na kuwasilisha taarifa hizi (zinazoshughulikiwa na Benki Kuu) kwa wakati kwa ajili ya ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 47 - Wizara ya Miundombinu: Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimebainisha kuwepo hoja ya Ukaguzi iliyotawala sana katika Mjadala wa Taarifa za Utendaji na Hesabu za Fungu 47 ambapo iligundulika kuwa Wakala wa Majengo ya Serikali ilinunua nyumba mbili kwa bei ya Sh. 410,000,000/=.

Aidha, katika maelezo yake, Mkaguzi Mkuu amehoji ununuzi wa nyumba hizo na kisha kuziuza, haukuwepo kwenye mipango na malengo ya Wakala kwa mwaka husika, pia ni kinyume na malengo, sera na mtazamo wa kuanzishwa kwa Wakala wa Nyumba za Serikali. Aidha, Mkaguzi ametaka kujua bei iliyotumika kuwakopesha wanunuzi wa nyumba hizo ili kufuatilia urejeshaji wa mkopo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu hoja hiyo, maelezo ya ziada yanatolewa jinsi nyumba hizo zilivyouzwa kwamba utekelezaji wa Uamuzi wa Serikali wa kuzinunua nyumba hizo ulifanywa miezi ya Julai na Agosti, 2004. Kwa kuwa baada ya nyumba hizo kununuliwa na kuwa chini ya Wakala zilikuwa ni nyumba rasmi za Serikali, nyumba hizo zilikuwa *allocated* kwa matumizi ya Viongozi wa Serikali kama taratibu zinavyohitaji.

Aidha, kwa kuwa pia kwa mujibu wa maamuzi ya Serikali kupitia Waraka wa Baraza la Mawaziri Na.7 wa mwaka 2001 nyumba hizi (ambazo sasa zilikwishaingia katika *pool* ya nyumba za Serikali) siyo kati ya nyumba ambazo zimezuiwa kuuzwa kwa watumishi, viongozi waliopangiwa nyumba hizo waliuziwa kwa kuzingatia taratibu zilizotumika kuuza nyumba nyingine zote za Serikali kwa Watumishi.

Mojawapo ya maelekezo ya Serikali katika utekelezaji wa zoezi la kuuzia Watumishi nyumba ni kuwa, kwa vile kipato cha watumishi wa Serikali ni kidogo na kwamba hawana uwezo wa kununua nyumba hizo kwa *market value,* utaratibu mahsusi na wa makusudi wa kuwawezesha kununua nyumba hizo utumike. Hivyo, utaratibu uliotumika kuthaminisha nyumba zote za Serikali zilizouzwa kwa watumishi ni kwa kuzifanyia uthamini wa *depreciated replacement cost* nyumba hizo, bila kujumuisha thamani ya ardhi ya eneo husika. Kwa kutumia utaratibu huu, nyumba husika ziliuzwa kama ifuatavyo:-

- Nyumba Na.106: Sh. 56,640,500/= *Uganda Avenue*, *Oysterbay;*
- Nyumba Na. 474: Sh. 66,460,5000/= *Mindu Street* - Upanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watumishi waliouziwa nyumba hizi wamekwishamaliza kulipa mikopo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati baada ya kutafakari hoja hii, ilistushwa na ukweli kwamba fedha za Serikali zilichukuliwa, zikanunua nyumba kwa bei ya juu halafu wakauziwa Watumishi wa Serikali. Kamati ilitembelea nyumba hizi na kubaini kuwa nyumba Na.106 ni nzuri na nyumba Na. 474 ni kama gofu.

Kamati iliwahoji wahusika wote kuhusu mlolongo wa maamuzi ya kuwauzia watumishi wa Serikali kwa mtindo huu ambao ni nje ya utaratibu wa Waraka Na.7 ulioagiza nyumba za Serikali wauziwe watumishi na sio kununua nyumba kwa bei ya juu na kuziuza kwa bei ya chini.

Kamati ilimuagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kufuatilia jambo hili ili kujiridhisha pamoja na kuhakiki malipo ya nyumba hizo.

Kamati imeelezwa kwa barua kumbukumbu Namba MM/010 ya tarehe 31 Januari, 2007 kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwamba wamepata vielelezo vyote kuhusiana na mauzo ya nyumba hizo na hoja ya ukaguzi imefungwa. Kamati inashauri kuanzia sasa Serikali isitishe utaratibu wa kununua nyumba na kuuzia watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 58 - Wizara ya Nishati na Madini: Katika taarifa yake kwa mwaka 2003/2004 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali alitoa hoja kwamba uwezo wa kupata mapato kutokana na Wizara hii haukuwa umekadiriwa sawasawa *(Aya ya 415.1, uk.337: Revenue collection performance).* Vyanzo vya mapato vya Wizara hii ni pamoja na mrahaba kutoka mauzo ya madini kama vile dhahabu, almasi, *tanzanite* na mengineyo. Kamati, kama alivyohoji Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, inaamini kabisa uwezo *(revenue potential)* wa kupata mapato mengi ya Serikali kutokana na Wizara hii kwamba ni mkubwa sana na kwa msingi huu Kamati iliamua kujiridhisha kama kweli Wizara hii inapata mapato yote inayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vikao vilivyofanyika Dar es Salaam na Dodoma, Kamati ilibaini matizo yanayosababisha sekta hii kutokupata mapato ya Serikali kutoka Sekta ya Madini kwa kiwango kikubwa kufuatana na uwezo na

mategemeo ya Taifa.  Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana chanzo cha kukosa mapato kutoka Sekta ya Madini ni pamoja na sababu zifuatazo:-

- Sheria ya madini inayotoa fursa kwa migodi ku-*depreciate* gharama ya mitambo *(Capital Investment Costs)* kwa mwaka mmoja tu wa kwanza wa shughuli za uchimbaji madini, inatoa pia fursa ya kuongeza asilimia 15 kwa bakaa ya gharama ya mitambo *(additional depreciation allowance on unredeemed investment)* na gharama kubwa za uendeshaji migodi *(High Operations Costs)*. Gharama hizi zisipoangaliwa kwa makini zinapunguza kiwango cha kodi ambayo ingetozwa kwenye faida;

- Kufuatana na taarifa za Wizara ya Fedha na *TRA* pamekuwa na hasara kubwa ambazo zimekuwa *declared* na Makampuni ya migodi. Kwa mujibu wa taarifa hizi, hasara kwa njia hii inakadiriwa kufikia bilioni 1.04 *USD* au Shilingi trilioni 1.358;

- Matatizo mengine ni pamoja na udhaifu katika Wizara ya Nishati na Madini kutunza nyaraka za mapato ya mrahaba. Udhaifu huu unaweza kuleteleza kupoteza mapato mengi; na

- Gharama ya huduma za Ukaguzi ambayo ni asilimia 1.9 ya thamani ya dhahabu itakayouzwa nje na itakayokuwa imekaguliwa, malipo haya yanaonekana kuwa makubwa, hasa ikizingatiwa kwamba mrahaba ni asilimia 3%.

Mheshimiwa Naibu Spika Serikali iko katika zoezi la majadiliano na wenye migodi wakubwa kwa lengo la kuhakikisha kwamba Tanzania inapata faida inayostahili kutokana na madini ambayo ni maliasili yake.  Kamati inayoshughulikia majadilino hayo inaongozwa na Wizara ya Nishati na Madini.

Kamati, kufuatana na maelezo ya Serikali, imeona kwamba Serikali imechukua hatua madhubuti za kuhakisha kwamba Sekta hii ya madini inachukua nafasi inayotegemewa na Taifa ya kuwa namba moja katika kuiletea Serikali mapato. Tunampongeza Rais kwa kulipa jambo hili kipaumbele.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa mpaka mwaka 2005 kumekuwa na hasara inayokadiriwa ya *USD* 1.045 bilioni, yaani Shilingi trilioni 1.358 sawa na robo ya Bajeti ya Taifa mwaka 2006/2007. Kamati inaishauri Serikali iongeze ubunifu na mikakati itakayoliwezesha Taifa kupata mapato yanayostahili kutoka Sekta ya Madini. Mapendekezo ya Kamati kuisadia Serikali katika jukumu hili yanatolewa kama ifuatavyo:-

Mapendekezo kuhusiana na mapato yatokanayo na Sekta ya Madini:-

- Kuna umuhimu kwa Serikali kufanya kila jitihada kuhakikisha kwamba kuna mazingira ya maelewano (*harmony*) katika Sekta nzima ya Madini ili kujenga *confidence* ya wawekezaji na wananchi;

- Serikali ichukue hatua za haraka kuhusiana na ujenzi (uwepo) wa miundombinu itakayowezesha uchimbaji wa madini kuokoa fedha nyingi zinazotumika hivi sasa kwa kutumia miundombinu mbadala. Mfano ni umeme, reli, barabara na kadhaliaka;

- Serikali ichukue hatua za makusudi kuifanya Sekta ya Madini kuwa chanzo madhubuti cha mapato ya Serikali, kama vile *corporation tax*, mrahaba na kadhalika;
  - Sheria ya Madini iangaliwe upya kwa kuangalia uwezekano wa kurekebisha kasoro zinazosababisha Sekta hii kutokuchangia mapato yanayostahili kwa Taifa Kama vile *deprecition policy 15% capital allowance*, fedha ya kurekebisha uharibifu wa mazingira;

  - Serikali kupitia *TRA* ichunguze suala la hasara iliyowasilishwa na makampuni ya migodi kwa lengo la kuipunguza;

  - Serikali iimarishe kitengo cha nyaraka *(documentation)* katika Wizara ya Madini, Wizara ya Fedha na Benki Kuu ili iwe msingi wa kudhibiti mwenendo mzima wa shughuli za Sekta ya Madini, ikiwemo takwimu za uuzaji madini nje uweze ukaimarika. Tumegundua kwamba hakuna utaratibu mzuri ambao unasaidia sehemu hiyo; na

  - Kuna umuhimu wa kuendelea na ukaguzi wa madini ili kuendelea kulinda maslahi ya Taifa katika sekta hii muhimu, kwa bei nafuu. Kwa hili Kamati inashauri Serikali izungumze na Mkaguzi wa sasa ili gharama ya ukaguzi ipunguzwe iwe ya kiwango maalum *(fixed),* badala ya asilimia kama ilivyo kwa sasa hivi. Sababu ni kwamba dhahabu inapanda kama vile mafuta.

Kwa hiyo, kama ni asilimia mtu anaweza kupata faida ni kwa dhahabu kupanda na bila kufanya kazi ya ziada. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha utaratibu huu na jambo muhimu ni kuimarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia imetolea maoni juu ya Wizara ya Afya ambao msisitizo hapa ni kwamba jengo la Muhimbili la Watoto limaziwe. Tunamwomba Waziri kama ni fedha aje aombe hapa ili kuhakikisha kwamba hilo jengo linakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumetolea maoni Mahakama ambayo tunasema kesi nyingi sana zinazoleta kasoro katika ukaguzi zimelala Mahakamani, basi itafutiwe njia ya kumalizia hili jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fungu la 68 ambalo ni Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hapa inaomba pawepo na Bajeti ya kutosha ili matatizo ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu, mikopo iweze ikapunguzwa. Pia kuna haja ya kuangalia jambo la udahili ili lisiwe tu kwa daraja la kushinda, lakini liweze kuoana ni fani gani mtu ameshinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumetolea maoni Wizara ya Mambo ya Ndani, hapa tunasisitiza yule Afisa Mhasibu mzembe ambaye amepoteza kesi angechukuliwa. Halafu

kuna Zanzibar ambalo kuna fedha zaidi ya Shilingi milioni Sh.190,382,897.00 na zenyewe zipelekwe kwenye Tume ya Pamoja. Pia tumetolea maoni Mkoa wa Kigoma, pia tumetolea maoni Wizara ya Mambo ya Nje ambayo hapa tunataka Chuo cha Demokrasia kiweze kuangaliwa ili kiweze kukaguliwa. Pia tumetolea hoja kwa Balozi zetu ambazo ziko nje ambapo watu wanatumia fedha zile ambazo wanazozikusanya badala ya kuzirudisha kwanza halafu wanapata gawio. Wengine wanatumia risiti ambazo siyo za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nijielekeze katika sehemu ya tatu ambayo ni mapendekezo ya jumla na kwa kuwa hii ripoti yetu tumeiweka ndani ya komputa, tutamwomba *Director* ainukuu yote hata kama hatujaweza kusema mapendekezo yote kwa sababu ya muda ambao tumepewa. Lakini mapendekezo ya ujumla Bunge lishirikishwe katika makubaliano ya msingi ya Bajeti na miongozo yake na hapa. *I think* mwezi wa Aprili Bunge litashirikishwa, Maafisa Wahasibu wa mafungu mbalimbali wawajibike kwa Bunge kama tulivyosema.

Halafu tunasema *perfomarnce* ya fedha ya maendeleo ni ndogo, tunaomba basi zile fedha ambazo hazipo uhakika zisiwekwe kwenye bajeti kwa sababu zinaleta hoja za ukaguzi. Kuna udhaifu mkubwa wa utunzaji wa nyaraka unaosababisha hesabu za Serikali kuwa na dosari kedekede. Kwa hiyo, jambo hili tunaomba liangaliwe. Tumeshazungumza jambo la *RAS* na *DED* ambapo pia hapa liangaliwe ili uwajibikaji uwe bayana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo kuhusiana na mafungu mbalimbali, tunashauri kwamba Fungu 22 liangaliwe kwa makini zaidi ili dosari ambazo zimewekwa mle ziweze zikaondolewa. Serikali itenge fedha za kutosha kumalizia jengo ambalo tumeshasema la Wodi ya Watoto katika Hospitali ya Taifa Muhimbili linalojengwa tokea mwaka 1988.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia tumeelezea mambo ya Mkoa wa Kigoma yule Afisa Mhasibu ambaye hajaweza kueleza juu ya maduhuli yake milioni 139 achukuliwe hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mapendekezo lukuki ambayo tumeweza kuweka humu ndani. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wajielekeze katika ripoti ambayo tayari tumeshaigawa. Kwa mfano Balozi wa Lilongwe, achukuliwe hatua ambaye yeye amechukua dola 100,001 mpaka leo hajaweza kurudisha masurufu.

Mwisho, Kamati inatoa pongezi kwa Maafisa Wahasibu wote waliopata hati safi za ukaguzi na inawahimiza Maafisa Wahasibu wote waliopata hati zenye dosari kwa kukazia zaidi kuzuia hoja kujitokeza kuliko kuzijibu hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa pongezi kwako na zaidi kwa Spika, kwa kutoa muda wa Bunge lako kujadili na kuamua juu ya mapendekezo ya Kamati. Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali na taarifa ya Mdhiti na Mkaguzi Mkuu, haijajadiliwa ndani ya Bunge hili kwa muda mrefu na hili linaleta hisia kwamba Bunge halijali hesabu za matumizi na mapato ya Serikali. Udhaifu huu unaathiri dhana ya uwajibikaji wa Serikali kwa Bunge.

Kamati inashukuru Ofisi yako kwa kuiwezesha Kamati kuweza kuhudhuria na kushiriki katika mafunzo mbalimbali. Pia kuweza kwenda *South Africa* na kushiriki katika Umoja wa *PAC, (SADC OPAC)* ambao sasa Tanzania ilichaguliwa kuwa Katibu.

Pia Kamati inamshukuru sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri anaiyofanya kukagua mahesabu na kuwasilisha Taarifa kwa wakati unaotakiwa siku ya kujadili Taarifa za kale zimepitwa na wakati kwani tunapowasilisha taarifa hii, Kamati tayari imeshaanza kujadili taarifa ya mwaka 2004/2005. Mwezi wa Aprili utakapowasilisha maoni yetu tayari tutapokea taarifa ya 2005/2006. Hii ni hatua nzuri sana. Tunashukuru sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaomba ikihitaji siku zaidi ili kukamilisha kazi hizi ipewe na Kamati iongezewe uwezo wa Kikatibu na kwa sababu Kamati imepata mafunzo mengi sana, basi kugeuzageuza pia inaturudisha nyuma. Kwa hiyo, Kamati iliyopo iweze kuendelea kwa kipindi chote cha Bunge.

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, tunatoa shukrani maalum kwa Idara ya *Hansard,* kwa kazi nzuri, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na sisi, Benki Kuu na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano waliotupa.

Mwisho, tunawaonya Maafisa Wahasibu ambao hawahudhurii kwenye vikao vya *PAC,* ni kosa la jinai na wanaweza wakafungwa mpaka miaka miwili na kupewa adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa**

**MHE. MGANA I. MSINDAI – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa juu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, iliyowasilishwa Bungeni mwezi Machi, 2006 kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Halmashauri za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutekeleza Kanuni ya 88(11) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004, naomba uniruhusu nitumie nafasi hii kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati yangu kuelezea masikitiko yetu makubwa kutokana na msiba uliolikumba Taifa letu kufuatia kifo cha Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru na Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu, aliyekuwa akishughulikia mambo ya Bunge, pamoja na Maafisa wetu waliofariki kufuatia ajali ya ndege iliyotokea Mjini Mbeya tarehe 14/12/2006. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze mahala pema Peponi roho za Marehemu. *Amin.*

Aidha, tunampongeza Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro kufuatia kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa; Mheshimiwa Bernard Membe, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri wa Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Mheshimiwa Dr. Batlida Burian kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, nafasi iliyokuwa inashikiliwa na Marehemu. Pia niwapongeze Manaibu Waziri,

Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Kayombo kwa kuteuliwa kwao kushika nafasi katika Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati hii yametajwa kwenye Kanuni ya 103 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na mwaka wa taarifa hii Kamati ilifanya kazi zake katika namna kuu mbili kama ifuatavyo:- Awamu ya kwanza, ilihusisha Kujadili Hesabu zilizokaguliwa za Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji. Kazi hiyo, ilifanyika kwa Halmashauri zote 118 na kazi hii ilifanyika Dar es Salaam na Dodoma.

Awamu ya pili, ilihusisha Kamati kwenda moja kwa moja katika kukagua miradi iliyotekelezwa katika ngazi ya Halmashauri, kwa kutumia fedha za umma ikiwa ni pamoja na nguvu za wananchi katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 katika Mikoa ya Dar es Salaam,Tanga Dodoma, Kigoma, Rukwa, Tabora, Mwanza Mara, Kagera na Shinyanga.

Kamati ilipata fursa ya kuhudhuria semina tatu. Moja iliyoandaliwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali ambayo ilihusisha (*LAAC*) na*(PAC).* Kamati ya pili, iliandaliwa na Idara ya Maboresho ya Serikali za Mitaa *(Local Government Reform).* Semina hii ilifanyika Dodoma ikihusisha *(LAAC)* na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Semina hii ilifanyika tarehe 16 na17 Juni, 2006. Hapa niwashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda na Mheshimiwa Naibu Celina Kompani kwa sababu walishiriki semina hizi toka mwanzo mpaka mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa taarifa zilizowasilishwa na Halmashauri mbalimbali mbele ya Kamati ulizingatia mambo makuu yafuatayo:- Taarifa ya Wilaya, Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Kawaida, Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa fedha za maendeleo pia hapa ilihusisha mifuko mbalimbali kama vile fedha za barabara, fedha za *Basket Fund,* fedha za *MMEM*, fedha za Wafadhili mbalimbali na fedha za *TASAF*. Majibu ya hoja za ukaguzi na majibu ya hoja za Kamati ya *LAAC* yaliyowasilishwa kwa kwenye vikao vya nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeendelea kuwashirikisha Wenyeviti wa Halmashauri ili wanaporudi Majimboni wakawaeleze Madiwani wenzao mambo yaliyotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utendaji wa kazi katika Halmashauri zetu kwa sasa umekuwa bora zaidi kuliko vipindi vilivyopitwa ingawa katika Halmashauri bado wako watumishi wachache ambao wanaharibu sifa nzuri na mazuri yanayofanywa katika Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ambalo Kamati imeliona ni la mwelekeo mzuri, ni ufungaji wa Hesabu za Halmashauri na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa wakati. Kwa mfano, kati ya Halmashauri zote nchini, ni Halmashauri sita tu (6) zilizochelewesha hesabu zake kwa hesabu za Januari-Juni 2004. Kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Halmashauri zote zimewasilisha hesabu zake. Kamati imegundua kuwa baadhi ya Halmashauri ambazo watumishi wake wamekaa muda mrefu bila kuhamishwa, wamejijengea tabia ya kufanya kazi kwa mazoea na sio kwa taratibu ama miiko maalum ya kazi zao, au uwezo wao wa kuwa wabunifu umefikia kikomo katika maeneo hayo, au wamejenga mazingira ya kuhodhi madaraka kuzidi Viongozi wao kiasi cha kutokuwa na

ushirikiano wa kutosha. Tumegundua pia kuwa ni tatizo kubwa sana kwa Mtendaji kukaa kwenye kituo kimoja kwa muda mrefu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa napenda nitoe pongezi na shukrani kubwa kwa Waziri Mkuu mwenyewe pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – *TAMISEMI* - Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa kukubali ushauri tulioutoa wakati tunaendelea na vikao vya Kamati na kuchukua hatua za haraka na kutekeleza ushauri huo kwa kuangalia upya Watendaji wote wa Halmashauri kwa kuanza kujaza nafasi zilizokuwa wazi, kuwathibitisha watumishi wenye sifa waliokuwa wanakaimu kwa muda mrefu na kuwahamisha Watendaji waliokaa kwenye Vituo vya kazi kwa muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema Awali, Halmashauri zinatakiwa kuwasilisha mahesabu na michanganuo ya miradi iliyo bayana na sahihi. Endapo Kamati inagundua kuwa Watendaji hawawezi kutolea maelezo ya kina taarifa zao wanazoziwakilisha, maana yake ama wanaidaganya Kamati au wana nia ya kuficha ukweli. Katika hatua hii, Kamati inalazimika kuchukua hatua kulingana na taratibu. Kwa mfano kutoa adhabu ya tozo ya asilimia 15 kwa wale waliosababisha uzembe au kuwarudisha wakaandike hesabu upya au vyote kwa pamoja.

Kwa Hesabu za Januari-Juni 2004 Kamati ilitoa adhabu ya hii kwa baadhi ya wakuu wa Idara katika Halmashauri ya Moshi, Tunduru, Makete, Mufindi, Dodoma, Kondoa, Ileje na Manispaa za Sumbawanga, Mbeya na Shinyanga kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Halmashauri ambazo zilirudishwa kwenye Kamati kwa sababu ya kutopitisha taarifa ya hesabu zake kwenye vikao halali vya Halmashauri yaani Kamati ya Fedha na Uongozi na Baraza la Madiwani, kabla ya kuzileta kwenye Kamati yetu. Halmashauri hizo ni Manispaa ya Singida, Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Halmashauri ya Bukoba Mjini. Wakati Halmashauri ya Wilaya ya Ileje ilirudishwa kwenye Kamati kwa sababu Watendaji walishindwa kutoa majibu ya kuridhisha. Aidha, Halmashauri ya Manispaa ya Arusha, ilirudishwa tena kwenye Kamati kwa sababu Kati ya Wakuu wa Idara 10 waliotakiwa kufika mbele ya Kamati nane hawakufika badala yake wakatuma Makaimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfuko wa Akina Mama na Vijana, yako maelekezo na maagizo yaliyotolewa na Serikali kwamba Halmashauri zote nchini zitenge kutoka katika mapato yake asilimia 10 kwa mwaka 2000 na asilimia tano kwa mwaka 2003 ili fedha hizo zitumike kukopesha vikundi vya Akina Mama na Vijana. Lengo kubwa la agizo lililokuwa ni kutunisha mfuko wa kukopesha walengwa, lakini pia kujenga uwezo wa Halmashauri zenyewe kuwazesha wananchi wao kujikomboa na umaskini. Maagizo haya yametekelezwa kwa kiwango kidogo sana, hakuna Halmashauri iliyoitosheleza Kamati katika hii na hivyo agizo halijatekelezwa kikamilifu. Kamati inashauri kwamba, sasa wakati umefika Halmashauri zilazimishwe kutekeleza agizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia ilitoa maelekezo kuwa Halmashauri itenge asilimia 15 au zaidi kutegemeana na uwezo wake kwenye vyanzo vya mapato ya ndani na yote yanayoingizwa kwenye Akaunti Na.1 na fedha hizo zipelekwe kwenye Vijiji kwa

ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Vijiji hivyo. Tunavyofahamu, fedha hizo ni nje na matumizi ya kawaida ya Halmashauri katika kufuatilia, kusimamia na kuchangia miradi hiyo kama Halmashauri. Kamati imegundua kuwa katika Halmashauri zote zilizohojiwa, nyingi hazitengi fedha kutoka kwenye fidia wanayoipata kutoka Hazina. Badala yake wameendelea kutumia fedha hizo kwa shughuli nyingine za Halmashauri kinyume na maagizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ambalo Kamati imeliona ni tafsiri tofauti ya maelekezo hayo, ndicho chanzo cha Halmashauri nyingi kukiuka agizo la Serikali. Katika hali hii, Kamati inashauri ufafanuzi na maelekezo ya kina sasa yatolewe upya ili kila Halmashauri iwe na tafsiri na utekelezaji unaofanana. Hapa hatusiti kuzipongeza Halmashauri zilizotekeleza Agizo hilo ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Manispaa ya Ilala, Jiji la Mbeya na Halmashauri ya Wilaya Kyela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia, ilibaini kuwa lipo tatizo katika Halmashauri zote la ulipaji wa mishahara kwa Watendaji wa Vijiji. Mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji mpaka sasa kuna jumla ya Watendaji 40, ambayo bado hawajawahi kulipwa mishahara yao kwa zaidi ya miaka mitatu sasa. Sababu ya Watendaji hao kutolipwa ni kwamba majina yao hayakuingizwa kwenye orodha ya malipo kutoka Hazina *(payroll)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waraka wa Serikali unaohusu ajira ya watumishi, unawataka watumishi wote wanaoajiriwa Serikalini kuwa na kiwango cha Elimu ya Sekondari na uliweka muda maalum kwa waajiriwa wote ambao wako chini ya kiwango hicho, kuwa wamepata elimu hiyo ifikapo Juni, 2007, vinginevyo wataondolewa kazini. Baadhi ya Watendaji hawa ni miongoni mwa waathirika wa Waraka huu.

Kwa msingi huo, Kamati imekuwa inahoji ni hatua gani au kama kuna mipango yoyote katika Halmashauri zao kuendeleza Watendaji hao. Imebainika kuwa Halmashauri nyingi hazina programu maalum ya kuendeleza Watumishi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema tukafahamu msimamo wa Serikali kuhusu ulipwaji wa malimbikizo ya madeni ya mishahara na utaratibu wa kuwaendeleza watumishi hawa, Halmashauri kuweka programu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la jumla lilikuwa ni Makisio ya Mapato kwa kila Halmashauri nchini. Asilimia 96 ya Halmashauri zetu haziwezi kujiendesha endapo Serikali itaacha kuzipatia fedha. Siyo tu kwamba haziwezi kujitegemea kwa sababu ya ukusanyaji kidogo wa mapato, bali pia mipango yao hafifu ya kutambua vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Halmashauri nyingi zilifanya makisio ya chini na kukusanya chini ya makisio hayo. Kamati inashauri kuwa Halmashauri ziwe makini katika kufuatilia makusanyo na makisio yao lakini pia kuwa wabunifu katika kutafuta vyanzo ambavyo havitakuwa kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hesabu za Januari 2004 Kati ya Halmashauri 118 Halmashauri 21 zilipata hati chafu. Kwa mwaka 2004/2005 ni Halmashauri nne tu ambazo zilipata hati chafu nazo ni Misungwi, Wilaya ya Mtwara, Wilaya ya Handeni,

Halmashauri ya Mji wa Mtwara, Mikindani, hizi ndiyo zilizopata hati chafu. Hata hivyo dhamira ya Kamati kufikia mwaka wa fedha 2007/2008 pasiwepo Halmashauri yenye kupata hati chafu, hasa kwa kuzibana Halmashauri hizo kwa njia ya kuzikagua vitabuni na zaidi kuzikagua moja kwa moja katika miradi wanayotekeleza *(value for money). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Halmashauri nyingi kuwa na hati safi, lakini haimaanishi kuwa Halmashauri hizo zinafanya vizuri ikilinganishwa na hali halisi ya utekelezaji wa miradi yao. Hii imegundulika baada ya kutembelea Halmashauri kwenye Mikoa 11 kukagua *value for money* kwamba katika baadhi ya maeneo Halmashauri zimefanya vibaya, fedha zimetumika vibaya, hali ya vitabu na hali halisi havilingani. Ubadhirifu umekuwa mkubwa kwa mfano, Manispaa za Dodoma, Tanga na Halmashauri za Wilaya ya Korogwe, Mpanda na Kigoma Vijijini.

Wakati wa uchambuzi wa hesabu za Halmashauri Kamati ilichunguza kwa undani mwenendo wa mapato ya Halmashauri ili kuona na kushauri ni kwa namna gani Halmashauri zinaweza kuongeza mapato yao na hivyo kuwa na uwezo wa kutekeleza malengo yaliyowekwa na wananchi wa Halmashauri hizo. Kamati imefanya hivyo kwa kuwa inaamini kuwa Halmashauri zenye mapato ya kutosha ndiyo inayoweza kuwahudumia wananchi wake kwa kuchangia kwenye miradi iliyoibuliwa na wananchi wenyewe. Kamati ilibaini kuwa malengo na makusanyo ya mwaka yanapachikwa tu, hayafanyiwi uchambuzi kwa kuzingatia takwimu na vyanzo halisi vya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo bado lina matatizo sana ni masurufu na karadha. Kiasi kikubwa cha makusanyo ya Halmashauri kiko mikononi mwa watumishi, hali inayoonyesha kuwa utunzaji wa kumbukumbu katika Halmashauri nyingi ni mbovu na hivyo uwezekano wa hizo fedha kupotea ni mkubwa. Muda mrefu unapita bila Halmashauri kuchukua hatua za kukata fedha hizo toka kwa wadaiwa. Kwa mujibu wa Kanuni, masurufu yanatakiwa yarejeshwe sio zaidi ya siku 14 tangu mtumishi kutekeleza wajibu alioombea hizo pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu unaonyesha kuwa, wananchi ni wepesi sana kuchangia kwenye miradi inayobuniwa na wao wenyewe pamoja na kujitolea kwenye miradi mbalimbali inayobuniwa na Serikali endapo watahamasishwa kikamilifu. Haya yanajionyesha kwenye miradi ya *MMEM, MMES* na *TASAF*.

Mheshimiwai Naibu Spika, Kamati inapenda kuwapongeza sana Watanzania katika Halmashauri mbalimbali kwa kukubali kwao kutoa michango pale inapohitajika. Hata hivyo Kamati imebaini kuwa nguvu na michango ya wananchi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo havithaminishwi kupata urari wake kifedha. Hivyo, kutowatia moyo wananchi. *(Makofi)*

Lakini kutothaminishwa kwa nguvu hizo kunaweza kuhusishwa na ubadhirifu wa fedha zinazotolewa na Serikali au kwamba zinatumika lakini kwa kiasi kidogo sana huku mzigo mkubwa wa utekelezaji ukiachiwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa walifanya ziara kwenye Halmashauri za Mikoa 11 katika kipindi tofauti hadi kufikia

Januari mwaka huu. Hali halisi ya utekelezaji wa miradi iliyotembelewa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika zoezi la kukagua *Value for Money* Kamati ilishindwa kujiridhisha na utengenezaji wa barabara, kwa kuwa barabara nyingi zimeharibiwa na mvua. Miradi ya barabara ambayo Kamati haikuridhishwa na jinsi ilivyokuwa imetengenezwa, Miradi hiyo kama tulivyoionyesha kwenye taarifa yetu haikuwa imejengwa kwa utaalam uliokusudiwa kwa sababu hapakuonyesha dalili za kujengwa *culverts* na *drainage system* na kushindiliwa vizuri, matokeo yake wakati mvua zinanyesha, barabara hizo zote zilisombwa na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanikiwa kutembelea miradi inayohusu Shule za Msingi na za Sekondari. Kwa miradi ya madarasa na nyumba za Walimu, Kamati haikuridhishwa na ujenzi wa madarasa na nyumba za Walimu katika maeneo mengi hasa kwenye Shule za Msingi. Hiyo ilitokana na kwamba zipo aina mbili za ramani za madarasa zinazotolewa na Serikali kupitia mpango wa *MMEM.* Halmashauri nyingi hazikuzingatia vipimo halisi vya ramani hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo la jumla kwa Wakurugenzi wote limekuwa kwamba Shule zitakazojengwa sasa zizingatie mchoro mpya wa *MMEM* uliotolewa na Wizara. Zipo baadhi ya Shule za Msingi ambazo wanafunzi wanaendelea kukaa chini, yaani hawana madawati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano michache ni Shule ya Msingi Jamhuri katika Manispaa ya Tabora na Shule ya Msingi ya Mtakuja katika Manispaa ya Musoma. Mazingira kama haya sio rafiki kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la kutofuata miongozo ya kitaifa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, hivyo kufanya miradi mingine kukosa fedha za kukamilisha au kutelekezwa chini ya viwango vilivyokusudiwa. Kamati iligundua kuwa nyumba nyingi za Walimu zilizotolewa taarifa kuwa zimekamilika na Walimu wakiwa wanaishi humo, hazikuwa zimekamilishwa kwa kuzingatia ramani. Nyumba nyingi za Walimu zina jengo la kulala tu bila kuwa na choo, jiko, bafu na stoo kama ilivyo katika ramani.

Aidha, katika Halmashauri nyingi madarasa mengi yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi yamebakia kuwa maboma. Halmashauri zimeshindwa kuyakamilisha madarasa hayo kwa kupelekewa mbao, mabati na milango. Kitendo hiki kinawakatisha tamaa wananchi kuendelea kuchangia miradi mingine ya maendeleo. Kote Kamati ilikopita imekutana na matatizo kama hayo niliyoyaeleza. Kwanza majengo yote, Kamati imeagiza yakamilishwe kwa fedha za *OC* zinazopelekwa kwenye Halmashauri na pili majengo yote yatakayojengwa kuanzia sasa yazingatie ramani zinazotolewa na hasa nyumba za Walimu zitakazojengwa sasa ziwe na vyumba vitatu vya kulala na vyoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya afya ilihusu ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, ukarabati na ujenzi wa wodi mbalimbali na *x-ray* katika Hospitali za Wilaya kwa kutumia fedha kutoka *Busket Fund* na *TASAF,* nguvu za wananchi na fedha toka vyanzo vya Halmashauri na Wahisani mbalimbali pamoja na miradi mingine ya afya kutekelezwa kwa ufanisi. Iko baadhi ya miradi iliyotekelezwa kwa kiwango cha chini

huku ikitumia fedha nyingi sana na mingine kutofuata utaratibu wa ujenzi wake. Miradi hii tumeionyesha kwenye taarifa yetu, lakini niseme tu kwamba Mikoa ya Kigoma, Tabora, Shinyanga, Mara na Mwanza imeathirika sana na tatizo hili. Aidha, Kamati ilipokea matatizo makubwa yanayoikumba miradi hii ya Sekta ya Afya. Moja ikiwa ni upungufu wa watumishi. Upo upungufu mkubwa wa watumishi hasa katika Zahanati na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili imewaagiza Maafisa Tawala wa Mikoa kuhakikisha wanalifikisha Wizarani ili lipatiwe ufumbuzi. Pamoja na uhaba wa wafanyakazi, lipo tatizo la ulipaji wa mishahara katika baadhi ya hospitali za Wilaya hususan katika Hospitali teule za Wilaya kama vile Nyakahanga, Wilaya ya Karagwe. Rubya Wilaya ya Muleba. Mugumu, Wilaya ya Serengeti ambazo awali zilikuwa zinamilikiwa na wamisionari. *(Makofi)*

Watumishi wa hospitali hizi wamekuwa wakipokea mishahara yao toka Serikali Kuu tangu zilipoteuliwa kuwa Hospitali za Wilaya. Kuanzia mwezi Julai mwaka 2006 watumishi wale wengi hawajapata nyongeza ya mishahara kama ilivyorekebishwa na Serikali pamoja na kwamba ndani ya watumishi hao wapo ambao wamepokea nyongeza hiyo. Pia ilijitokeza suala la ukosefu wa dawa na vitendea kazi kutoka *MSD*. Waganga wote wa Wilaya zilizotembelewa wamethibitisha kuwa karibu nusu ya dawa zinazohitajika kwenye Vituo vya Afya hazipatikani *MSD*. Wakati huo huo hawaruhusiwi kuzinunua dawa hizo mahali pengine na hata kama zitapatikana mahali walipo. Kamati imeliona hili ni tatizo kubwa na inapendekeza kuwa pesa zinazotolewa *MSD* zipunguzwe ili asilimia 30 zipelekwe kwenye Halmashauri moja kwa moja zitumike kununua dawa zile ambazo *MSD* inashindwa kuwapatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko miradi ya kuigwa katika Sekta hii ya Afya. Mradi wa Ghala za Madawa iliyojengwa Karagwe. Mradi huo umegharimiwa na Serikali na Ufalme wa Ubelgiji na Serikali ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli umejengwa vizuri sana na ikijengwa maeneo mengi hili tatizo la madawa litapungua sana. *(Makofi)*

Tegemeo la mradi ni kukabiliana na tatizo la upungufu wa madawa muhimu kwa kuanzishwa kwa mfuko wa madawa utakaojiendesha, kuimarisha Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii, ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya, kuimarisha mawasilano kati ya vituo vya kutoa huduma za afya kwa maana ya simu ya upepo na vitendea kazi vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi tuliyopitia tulikuta mapungufu ikiwepo miradi ya elimu, miradi ya kilimo na miradi ya maji. Kwa mfano, tulikwenda Mombo, tukakuta Shule nzima haina choo hata kimoja. Kwa hiyo, wanafunzi wake walikuwa wanajisaidia vichakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu wa kuimarisha Vitengo vya Ukaguzi na kuwaendeleza watumishi kielimu, pia mgawanyo wa fedha za *MMEM* bado unaleta tatizo. Tulikwenda maeneo mengine tukakuta fedha za *MMEM* na *MES* haziendi kwa shule husika, bali zinakaa Hazina Ndogo. Kwa hiyo, kuwafanya watumishi, walimu wahusika wapate shida ya kwenda kuzipata hizo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nikushukuru sana wewe, nimshukuru Mheshimiwa Spika, niwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu walioiwezesha Kamati hii kufanya kazi nzuri ya kuigwa, nao ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Ali Haji Ali, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Samwel M. Chitalilo, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mheshimiwa Laus O. Mhina, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Halima O. Kimbau, Makamu wa Mwenyekiti na mimi mwenyewe Mwenyekiti. *(Makofi)*

Vile vile nawashukuru sana Makatibu wetu, Ndugu Dickson Bisile na Ndugu John Joel kwa kazi nzuri waliyoifanya kuisaidia Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Nawashukuru sana kwa hoja hiyo.

Waheshimiwa Wabunge walioomba kuzungumza mpaka sasa ni 25. Kwa hiyo, naanza kumwita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista J. Mhagama na Mheshimiwa Mwanri ajiandaye. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa nafasi. Pili, niwashukuru, niwapongeze Wenyeviti wa Kamati zote mbili za Hesabu za Serikali, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na Kamati zao kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuweza kutuwasilishia hafla hii kwenye Bunge. Nafikiri sasa tutakubaliana na Wabunge kwamba umefika wakati taarifa zote za Kamati ziweze kufika kwa wakati ili tusiwe tunajadili mambo ya nyuma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ningependa kusema mambo ya jumla kwanza. Ukipitia taarifa zote mbili, utakuta kwamba kuna mambo ya msingi ambayo yangetaka kuzingatiwa na Serikali kwa jumla. La kwanza ni kwamba Serikali hairuhusiwi kutumia bila ya idhini ya Bunge. Ukiangalia Taarifa ya *PAC* utakuta kwamba kuna *access vote* hapa ya 31 bilioni ambayo imetumiwa bila ya idhini ya Bunge. Nasema, kama Serikali Kuu inaanza kuvunja Sheria na Katiba ya Nchi, basi na Serikali za Mitaa na wengine wataendelea kuvunja sheria hizo.

Kwa hiyo, la kwanza nafikiri ni kusimama katika misingi yetu ya Sheria za Fedha na Katiba yetu inavyoturuhu katika suala zima la mapato na matumizi ya nchi. Hili lilikuwa la kwanza la jumla. La pili la jumla ni kwamba ukisoma Taarifa ya *PAC* utakuta kwamba kuna deni kubwa sana la Serikali na Serikali kila siku inaendelea kukopa. Nafikiri Waziri wa Fedha angetusaidia. Sasa kuna ongezeko kubwa la makusanyo ya mapato. Tulipoanzia mpaka sasa hivi tuko kwenye bilioni 230 kwa mwezi. Vile vile

kuna kasi kubwa ya nchi mbalimbali na mashirika mbalimbali kutufutia madeni. Inakuwaje, deni la Taifa linaendelea kuongezeka? Tunahitaji maelezo ya kina kwa hili kwamba huku kuna mapato yanaongezeka, huku unafutiwa madeni, lakini bado deni la Taifa linaendelea kuongezeka. Nafikiri hapa kunahitaji maelezo ya kina tuweze kuelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la tatu la jumla ni kwamba, ukiangalia *PAC report* aliyoiwasilisha utakuta kuna pesa zaidi ya Shilingi trilioni *1.3* ambazo zingeweza zikawa ni mapato ya Serikali. Ukichukulia fedha ambazo zimekuwa hazikukusanywa kutokana na nyaraka mbovu au nyaraka pungufu *about 58 billion,* ukichukulia hiyo, tayari ile asilimia 39 ya *budget deficit* ambayo tunayo imekuwa *covered already.* Kwa hiyo, hakuna sababu ya Serikali kwenda kumpigia mtu magoti kwa sababu mapato yaliyoko katika nchi yanatosheleza kabisa kama yangeweza kusimamiwa vizuri. Hili nalo tutahitaji kupata maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ya jumla, ningependa kusema kwenye *Vote* ya 58 ya Madini. Taarifa ya *PAC* inaonyesha kwamba ukurasa wa 38 Wizara ya Nishati na Madini kifungu cha 58. Kuna mapato ambayo yangeweza kupatikana. Lakini kwa sababu tu ya uzembe wa kutokutunza nyaraka, kwa sababu tu ya kutokufuata sheria ya Madini yenyewe ambayo tumeipitisha katika Bunge hili, pamoja na mapungufu yake tumeweza kukosa shilingi trilioni 1.3.

Sasa nasema hii ni hatari sana hapa hakutaji Sheria mpya, wala hakutaji kitu chochote, ni kufuata Sheria iliyopo hivi sasa. Hakuna nyaraka katika Wizara ya Madini za kuweza kukusanya mapato yetu. Hakuna *document* za kutosha Benki Kuu za kuweza kufuatilia mapato yetu. Siyo hiyo tu, hata Sheria inayosema kwamba makampuni yote ya madini lazima kumbukumbu zake ziwekwe Tanzania na hawaweki Tanzania wanaziweka nje ya nchi na Serikali imeshindwa kusimamia hilo. *(Makofi)*

Sasa tunakuja hapa tunasema Miundombinu, hatuna pesa. Pesa tunazo, tatizo ni *management of our resources,* hili ndiyo tatizo la msingi lililopo. Mimi ninachokiomba kwa Mheshimiwa Waziri atusaidie. Kwanza ile ripoti ya Alex Stuat iko wapi? Kwa sababu taarifa tulizonazo kwamba ripoti hii imeelezea haya mapungufu yote, ya ndani, ya kwetu sisi ya kuweka kumbukumbu sahihi kwenye Wizara, ya kusimamia Sheria kwamba hawa watu *document* zao zote ziwekwe ndani ya nchi, yako katika *Alex Stuat Report.* Lakini bado Serikali imekuwa bubu haisemi chochote pamoja na kwamba tunatoa mrahaba, tunatoa asilimia 1.9 ya mapato ya mrahaba ya asilimia tatu ambayo Mwenyekiti hapa amesema ni kubwa sana, tunaitoa na tumeipigia sana hapa Bungeni, lakini bado taarifa yake mpaka leo haijapatikana. Tungependa vile vile Serikali itueleze, Taarifa hii imefikia wapi? Tunalipa karibu dola milioni 65 mpaka utakapomalizika mkataba, lakini taarifa yake bado hatujaiona na tungependa tuione na tujue maudhui yake hiyo taarifa inasema nini katika suala zima la kusimamia Sekta hii ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la matumizi mabaya ya Serikali. Ukisoma taarifa ya *PAC* kuna *access vote* ambazo zimetumika bila ya idhini ya Bunge. Jambo la kusikitisha ni kwamba Wizara ya Fedha ambayo ndiyo Wizara Mama ina-*lead.* Ndiyo msimamizi mkuu na wakati mwingi katika Bunge hili tunaambiwa tatizo kubwa ni uwezo wa Wahasibu wetu uko chini. Ukiangalia matatizo yaliyoko kwenye Wizara

ambako ndiko kwenye *qualified people* ni makubwa zaidi kuliko yaliyoko kwenye Halmashauri ambako kuna watu ambao hawana uwezo. *(Makofi)*

Sasa tatizo hapa ni nini? Ni uwezo wa watu? Ni uaminifu au ni usimamizi mzuri. Ma-*Accounting Officer experience* tulionayo na wewe unayo *experience* hii, wakiona *PAC* kesho inakutana, ndiyo watu wanahangaika kuangalia ma-*audit report.* Lakini katika kipindi cha mwaka mzima wanatumia, wanafuja, hawana habari. Siku wakiona ratiba ya *PAC* iko pale au ya *LAAC* ndiyo watu wanaanza kuhangaika. Lakini Sheria inawabana kabisa ma-*Accounting Officer* kwamba lazima wawachukulie watu walioko chini yao na wao wachukuliwe hatua. Mimi naomba sasa Mawaziri kwa kweli nawaomba Mawaziri wawasilimie ma-*Accounting Officer* wafanye kazi ya *routine* ya kuhakikisha matumizi na mapato ya Wizara zao. Kuna mapato mengi hayakusanywi, tumeona katika ripoti hapa. Kuna matumizi ya ovyo. Lakini kwa sababu ma-*Accounting Officer* wanatumia, hawana habari, mpaka kesho wakisikia *PAC* ndiyo mtu anatafuta *auditor* yuko wapi? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, utumiaji wa *Internal Auditors,* taarifa zote hizi mbaya zinazotokea, kama *Internal Auditors* wangefanya kazi yao vizuri basi kungekuwa na upungufu mkubwa wa upotevu wa nyaraka na upotevu wa fedha unaotokea hivi sasa. Kwa hiyo, bado hatujazitumia rasilimali, *human recource* tulizonazo ndani ya Wizara zetu kikamilifu kuhakikisha mapungufu haya ambayo yapo ndani ya Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Bunge lako Tukufu liazimie kabisa katika taarifa hizi mbili, wale wote waliovunja Sheria ya Fedha, wale wote waliovunja Sheria ya Manunuzi, basi Bunge hili liazimie wachukuliwe hatua mara moja kwa mujibu wa Sheria. Hilo ningeomba liwe ni azimio la kwanza la kufanya. Lakini la pili, badala ya kungoja mpaka *PAC* ifike, ni vizuri na Mawaziri na wao tukaazimia kabisa kama wanawasimamia hawa *Principal Secretaries* angalau kuwe na *routine* ya vikao ya kuhakikisha, basi kuna *check and balance* katika haya mambo ya matumizi na mapato ya Serikali. Vinginevyo tutaendelea na utaratibu huu na tutaendelea na kuwa na *deficit* kwenye bajeti bila ya sababu ya msingi. *(Makofi)*

Nasema sababu ya mapato ya Serikali kuwa hayatoshi haipo, ukichukua mapato kwenye madini, ukichukua mapato kwenye rasilimali za maliasili zinatosha kabisa kutukidhia mahitaji yetu. Lakini Sheria haifuatwi. Lakini baya zaidi, ni kwamba, Sheria ya Madini ya mwaka 1988 inasema wazi kwamba Makampuni yote yaliyoko Tanzania yanatakiwa nyaraka zake ziwekwe Tanzania. Sheria kabisa tumepitisha hapa Bungeni. Wala haina kasoro Sheria hii. Sasa tuelezwe hapa Bungeni, Serikali imeshindwa nini kuisimamia Sheria hii ili kuyabana Makampuni haya kuweka kumbukumbu zake hata ikafikia mahali, *auditor* aliyechaguliwa kufanya hayo, hawawezi kupata kumbukumbu kwa sababu tu haziko ndani ya nchi. Hili tutataka maelezo ya kina kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, tungependa vile vile kupata kauli ya Serikali. Migodi ya dhahabu iko mingi, ni kwa nini *MEREMETA* haikukaguliwa hadi leo? Hili nalo tutataka maelezo ya kina. Tumesoma taarifa mbalimbali, *MEREMETA* mpaka leo haijakaguliwa na hakuna maelezo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naungana na wenzangu kuwapongeza Wenyeviti na ninaunga mkono hoja hizi. Ninaomba masuala hayo yajibiwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja zilizoletwa mbele yetu na Wenyeviti wa Kamati kwa niaba ya Kamati zao. Lakini kwa mujibu wa Kanuni na taratibu zinazoendesha Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sina budi kusema kwamba, kwa kuwa leo ni mara yangu ya kwanza kuchangia kwenye Bunge hili, nirejee kusema kwamba tunapongeza sana yale yaliyotokea katika hizi siku mbili tatu, kwa maana ya uteuzi wa Dr. Asha-Rose Migiro na uteuzi wa Waheshimiwa Manaibu Mawaziri lakini na Mawaziri. Ninasema hivyo na hasa nikimpongeza ndugu yangu Gaudence Kayombo, Mbunge ambaye tunatoka katika Mkoa mmoja. Lakini na wale wengine vile vile nawapongeza sana. Lakini ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Ngeleja na wale wengine vile vile nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapokea pole zote ambazo zimekuwa zikitolewa kwenye msiba mkubwa uliotukuta wa Mheshimiwa ndugu yetu Juma Jamaldin Akukweti, Mbunge mwenzetu kutoka Mkoa wa Ruvuma. Lakini kama nilivyosema mara ya mwanzo kwamba tunawashukuru Wabunge, Serikali na Bunge kwa kushirikiana nasi katika msiba ule mzito uliotupata. Utaratibu huu tunaofanya sisi Wabunge kuchangia hoja ambazo zimekuwa zikijadiliwa na Wabunge wenzetu kwenye Kamati mbalimbali, ni utaratibu muafaka kabisa. Ninafahamu kwamba ni utaratibu ambao uko katika Kanuni zetu za Bunge za kuendesha shughuli mbalimbali ndani ya Bunge ili kutupa nafasi sisi Wabunge kuishauri Serikali yetu katika masuala mbalimbali ambayo tunaona kwamba yatasaidia sana kuleta na kuharakisha kasi ya maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme taarifa hizi mbili za Wenyeviti zinahusu suala zima la mwenendo na utaratibu wa matumizi ya fedha katika nchi yetu ya Tanzania. Nchi yetu imekuwa katika mfumo wa kurejesha madaraka makubwa kutoka kwenye Serikali Kuu kwenda kwenye Serikali za Mitaa kwa maana ya kwamba *from the centralizaton to the decentralization process.*

Kwa maana hiyo, sasa hivi Serikali za Mitaa zinapewa jukumu zito zaidi ya kusimamia maendeleo ya wananchi wa Tanzania na kwenye Serikali za Mitaa sasa ndiko ambako kunatakiwa nguvu yote ya kiutekelezaji ya kiusimamizi na ya kiutendaji ipelekwe kule kwenye Serikali za Mitaa. Ninafurahishwa sana na maamuzi yaliyopitishwa na Bunge, lakini maamuzi pia yaliyopitishwa na Serikali katika kipindi kile ambacho tuliona kuna umuhimu wa kufuta kodi ambazo zilikuwa na kero kwa wananchi kwa maana ya kwamba kuiachia Serikali Kuu mamlaka ya kukusanya kodi ili kuweza kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi kule katika Serikali za Mitaa ambako ndiko nguvu kubwa ya hoja ya maendeleo kimsingi inakochukua nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo lilitekelezwa vizuri sana bila wasiwasi wowote. Lakini ufanisi wa kazi sasa katika Serikali za Mitaa ndiko tatizo liliko kubwa kubwa sana. Vyanzo laini vya kukusanya mapato katika Serikali za Mitaa vimefutwa. Kumebakiwa vyanzo vigumu sana ambavyo haviwezi kusaidia Serikali za Mitaa kuweza

kujipatia fedha kupitia vyanzo vyake ili kuendesha miradi ya wananchi. Lakini naipongeza Serikali, bado imekuwa ikisimama imara kuhakikisha kwamba Serikali Kuu kupitia bajeti zinazopitishwa ndani ya Bunge na taratibu za matumizi ya fedha inapeleka fedha kule katika Serikali za Mitaa ili shughuli ziweze kuendelea na kufanyika kama zinavyotakikana.

Lakini ninaomba niseme kwamba katika mpango na mfumo mzima wa *Revenue Retention Scheme* kitu hiki ambacho tunakuja kukigundua, yako makusanyo ambayo yanakusanywa kupitia Wizara, lakini tunakuja kugundua kwamba mwishoni mwa siku yako mafungu ambayo fedha zake zinarudishwa Hazina na mwaka wa fedha umekwisha bila kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho kinasababisha kukwama kwa shughuli nyingi za maendeleo kadri ya utaratibu uliopangwa na kupitishwa na Bajeti yetu ndani ya Bunge letu Tukufu la Tanzania. Hii inajionyesha kwa mfano ripoti ya Mwenyekiti wa *PAC* ukurasa wa 31, unaona pale makusanyo duni ya fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hilo lilikuwa ni tatizo lingine mojawapo ambalo wenzetu pale kwenye Kamati waliliona. Unaona kabisa kwamba jinsi fedha zilivyokusanywa na jinsi zilivyoshindwa kufikia malengo ambayo tumejipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mikubwa ya maendeleo inafanyika kule kwa wananchi ambako nimesema kwenye *Local Authorities* kule ndiko tunaendesha miradi ya ujenzi wa barabara, kule ndiyo tunaendesha miradi ya kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wananchi, kule ndiko tunaendesha shughuli zote za kilimo na mipango yote ya kilimo ili kuboresha maisha ya Watanzania ili Watanzania wawe na maisha bora. Sasa nilikuwa naomba sana tumwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameanza kazi vizuri. Anaonyesha ushirikiano wa kutosha na kwa kweli mimi nasema huyu mama ni rasilimali kubwa sana katika nchi yetu. Ninaamini kabisa na ninafikiri hata leo ameamua kubaki makusudi humu ndani ili aweze kuelewa mwenendo mzima wa taratibu hizi na matatizo yanayoweza kukabili Sekta ya Fedha katika nchi yetu. Sasa ninamwomba mama atusaidie katika mambo yafuatayo:-

Kwanza kabisa, tunamwomba Mheshimiwa Mama yetu Zakia Meghji - Waziri wa Fedha atusaidie fedha zinapopitishwa kulingana na mafungu yanayotakiwa kwenda hasa kwenye maeneo yetu ya Serikali za Mitaa kwa maana ya Halmashauri yetu yafike kwa wakati. Fedha zile zifike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na tatizo kubwa kwamba, fedha inayopangwa kwa ajili ya mradi wa maendeleo unaotakiwa kuanza mwezi wa Agosti, fedha ile inatufikia mwezi Desemba. Mwaka unapokwisha, fedha iliyotumika ni robo tu ya kiasi cha asilimia ya fedha nzima ambayo iliyotakiwa kutufikia. Kwa hiyo, tunajikuta tunabaki kwenye njia panda. Hatuelewi mradi ule utakamilika vipi kulingana na asilimia 100 ya fedha iliyopangwa katika mradi husika na ilishapitishwa katika Bunge letu. Mheshimiwa Waziri wa Fedha akitusaidia katika hilo ninaamini kabisa matatizo yetu ya kiutendaji kwenye *Local Government* yatakuwa yamepungua kwa kiasi kikubwa.

Lakini lingine la pili, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atusaidie kusimamia mpango mzima wa *Revenue Retention Scheme* na huo ndio utakaosaidia kabisa kuhakikisha kwamba hakuna mlundikano wa fedha ambazo hazina matumizi, hazipelekwi katika matumizi ambayo yalikusudiwa kufanywa. Hapo tutaweza kwenda vizuri. Lakini haya mambo mengine ya kiutendaji ambayo pia yamekuwa ni sababu nyingine zinazopelekea kutokufanyika shughuli za kimaendeleo vizuri, nadhani Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie kuyaangalia. Kwa mfano, ni nia njema tu iko ya kuhakikisha kwamba Serikali za Mitaa, Halmashauri inayopata hati chafu haiwezi ku-*qualify* kupewa ruzuku ya maendeleo.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hili nadhani tulitazame vizuri kwa namna fulani. Wananchi hawakuhusika katika kusababisha hati chafu ipatikane ndani ya Halmashauri yao. Lakini wale wananchi ndio wanaokuja kubeba *burden* ya kutokupewa ruzuku ya maendeleo na kuwafanya wananchi wale wakose kupiga hatua za kimaendeleo kwa kosa la Watendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine niseme si kosa la watendaji, kwa maana ipi? Inawezekana katika Halmashauri ile, hawana mtaalamu wa fedha, ama mtalaam aliyepo anakaimu na ile sio nafasi yake. Kwa hiyo, utakuta Halmashauri inapata shida kubwa sana, matokeo yake wananyimwa ruzuku ya maendeleo, wanaoumia ni wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika kipengele hicho pia ningemwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, lakini wakisaidiana na Waziri wetu wa TAMISEMI, wajaribu kuangalia tuhakikishe kwamba, wataalam wa fedha wanakuwepo kwenye Halmashauri zetu kadri inavyotakiwa. *Internal Auditors* wafanye kazi zao kwa kadri inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ametuambia wanachotaka ni kusaidia, kuhakikisha kwamba, utaratibu wa mapato na matumizi unafuatwa vizuri, ili kuzifanya Halmashauri zote ziweze kuwa na hati safi, kwa maana ya utendaji mzuri upande wa fedha na kuweza kuwasaidia wananchi, kufikia maendeleo yanayotakiwa, lakini wanahitaji sana nguvu za Serikali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naomba niliseme hilo, lakini niendelee kusema, bado tuna matatizo makubwa ya mfumo mzima wa kuwalipa watendaji wetu wa vijijini na hasa watendaji wetu wa kata. Tukae chini katika bajeti inayokuja, ikiwezekana tuharakishe kuwaingiza kwenye *payroll* watendaji wa kata na walipwe na Serikali Kuu, ni mzigo mkubwa sana kwenye Serikali zetu za mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, nilikuwa na hayo machache tu ya kuchangia na naipongeza Serikali, kwa shughuli inayofanya, kuendeleza maendeleo katika nchi yetu. Ahsante sana, naunga mkono hoja zote mbili. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika taarifa hizi mbili, ambazo zimetolewa na Wenyeviti wetu. Napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, kwa taarifa nzuri ambayo ameitoa na napenda kumpongeza pia Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ambayo mimi ni Mjumbe wake.

Kabla sijaendelea, naomba nichukue nafasi hii, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, kutoa pole sana kwa ndugu zetu, familia ya Marehemu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti. Sisi wananchi wa Siha, tumepokea kwa masikitiko makubwa sana taarifa hizi, tuliendelea kutoa salamu zetu, lakini kwa vile nataka ziingie katika *Hansard,* napenda kusema hapa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha na kwa kweli naamini kabisa kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi, tumepoteza kada muhimu na napenda kusema pole sana kwa jamaa na familia.

Napenda pia kuungana na Wabunge wenzangu, kuwapongeza wale wenzetu wote, ambao wamepata nyadhifa mbalimbali. Kwanza kabisa, napenda kumpongeza dada yetu mpendwa, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose M. Migiro, ambaye amekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Najua tumempelekea *message,* kwangu mimi nataka niseme tu kwamba, hii ni pongezi pia kwa akina mama wote wa Tanzania. Inaonesha kwamba, akina mama wakipewa nafasi, wanaweza wakafanya vizuri na Mheshimiwa Naibu Spika, wewe mwenyewe ni shahidi kwanza, umekaa pale tunaona unavyoendesha shughuli za Bunge vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo, humu ndani wako wengi, naweza nikawataja kwa majina lakini sasa kwa vile ni wengi, itakuwa tabu. Tunaona kabisa waziwazi kwamba, akina mama wakipata fursa, wanaweza wakafanya vizuri. *You can not imagine* kwamba, leo tunazungumza habari ya Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mtanzania, mwana mama, kwa hiyo, tuchukue changamoto, tuendelee kufanya hivyo na tunampongeza sana. *(Makofi)*

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian, kwa nafasi aliyoipata, Mheshimiwa Benard K. Membe, Mheshimiwa William M. Ngeleja na Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo. Nawapongeza sana wote, tunawatakia kila la heri na fanaka. Ninachoweza kusema, mimi kama Mbunge mwenzenu, nitatoa kila aina ya ushirikiano takaotakiwa kuutoa, ili kuweza kuleta mafanikio makubwa katika nchi yetu.

Baada ya hayo, niseme haya ambayo tumekuwa tunayazungumza hapa, mengine mengi yameshazungumzwa. *Politics* ni *reflection* ya *economics* na *economics* ni *reflection* ya *politics*, wapo watu wengine wanafikiri kwamba, unaweza ukatenganisha, ukasema unajua bwana haya ni mambo ya siasa yanaletwa hapa. Hakuna kitu cha namna hiyo, ukigawa soda hapa, unawapa watu wanakunywa, halafu mmoja akikosa akilalamika, *that is politics,* mbona mnagawana soda wote ninyi huku mimi sipati. Kwa hiyo, hapa lazima tuelewane vizuri. Yako madarasa ya MMEM na MMES, yanaonekana kwamba, unajua haya ni mambo ya kisiasa tu, hakuna habari ya kisiasa, *always the economic base* ina-*determine the super structure,* unachosema hapo juu, kama hapa chini hapana msingi ni kazi bure. Lazima tuweke hiyo *analysis* hapa, tuelewane vizuri, huu utaratibu ulioletwa na Serikali, ambao tunautumia hapa Bungeni wa kutoka kule tuliko na kwenda Shinyanga, Mwanza na Kilimanjaro, kwenda kuangalia namna hela ambazo tumezipitisha hapa zinavyotumika ni utaratibu mzuri, tuendelee nao. *(Makofi)*

Tunakuja hapa tunang'ang'ania kuwa, bajeti ni mpango wa Serikali, unaoonesha jinsi fedha zitakavyopatikana na namna zitakavyotumika. Tanzania ni nchi maskini, haiwezi ku-*afford* hapa kupitisha hela nyingi kiasi hicho, unaipeleka kule halafu huifuatilii, ni kitu kimoja, kusema haya ndiyo mapato ya Serikali tuliyopangia na hela zilizotumika ni hizi. Pia ni kitu kingine kabisa, kwenda kuangalia kama kweli haya

mabati yamenunuliwa au kwenda kuangalia kama nyumba za walimu zimejengwa na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu utaratibu ni vizuri tukauendeleza, *actually* Bunge linafanya kazi zake kupitia Kamati, hatuwezi kwenda wote sisi kuangalia wanyamapori, tukatoka wote tukaenda kwenye Halmashauri, utaratibu huu tunatakiwa ndio tuupiganie. Ndio unaosimamia Serikali na ndio kazi ya Mbunge kuisimamia Serikali. Hizi taarifa zilizotolewa hapa ni nzuri, tumezisikia. *(Makofi)*

Sasa mimi nataka niende mbele zaidi, hali ikoje kwenye *field*? Mimi *personally* nimekwenda Mara na Shinyanga, tumefika kule tumekuta hela zinakwenda na hili ni suala la *policy.* Serikali imeweka *policy* nzuri, Chama Tawala kimeweka *policy* nzuri, tunataka watu wetu wapate maji safi na salama tunakwenda kuangalia, tunataka watu wetu wasome, tunakwenda kuangalia. Nataka nichukue hili eneo la elimu, ambalo Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, tumekwenda kule tukakuta kwenye Halmashauri ile ile, hela zinazotoka TAMISEMI zimekwenda, zinazotoka Halmashauri zimekwenda, zinatokana na msaada, *SIDA* wamesaidia pale zimekwenda zinazotokana na wananchi wamechangia pale zimekwenda pale.

**NAIBU SPIKA:** Zilikwenda maana yake zimeliwa?

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Kwa maana ya kwamba, zimekwenda katika Halmashauri inayohusika, sio kwamba zimeliwa, nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika. Ukimwuliza mwalimu kwenye shule ya sekondari wewe ulipokea hela za MMES shilingi ngapi, atakwambia shilingi milioni saba, ukimwuliza kama amepata msaada wa wananchi, atasema ndiyo wananchi walikuja hapa walisomba mawe na mchanga, kazi imefanyika vizuri. Unamwuliza ulifanyaje, anasema tulisimamia tulikwenda vizuri, madarasa yake mazuri yamenyooka, yana *louvers* na kila kitu safi. Mnahama mnakwenda shule ya pili, kijiji kile kile, mnakuta madarasa ya ajabu ajabu, unajiuliza haya madarasa ameyapata wapi na hii ramani ameipata wapi! Ukiuliza maswali, watu walikuwa wakali mle Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka nikasema labda tunavuka mpaka, tunakuwa wakali kwa sababu ni kazi yetu sisi kusimamia matumizi ya Serikali. Unamwuliza mmefanya nini hapa, anasema sisi tumepewa hizi hela, unaanza na Halmashauri yenyewe, mwulize Mkurugenzi ambaye ndiye amepewa dhamana kubwa pale ya kusimamia, anakwambia unajua sisi tumeambiwa fedha zikishaingia kwenye shule za sekondari, zinahusika zaidi na *Headmistress* au *Headmaster* au Mwenyekiti wa shule yule aliyeko pale. Unamwuliza *engineer*, huu ukuta wewe uli-*satisfy* kwamba, utoke hapa kwenda hatua hii? Anakwambia sisi hatuhusiki, tumeiachia Kamati ile ya shule iko pale. Nataka niseme hapa kuna tatizo, lazima tujenge mfumo wa usimamizi. *(Makofi)*

Haiwezekani hela za Serikali, zitoke kwenye *centre,* ziende kwenye Halmashauri, pale kuna *DED* amekaa, anayetakiwa kusimamia hela zilizokwenda pale shuleni, anasema aliiachia Kamati ya Shule ifanye. *That is wrong,* Halmashauri zetu zionekane kabisa waziwazi, eti Mkurugenzi anakwambia, unajua mimi nilimwachia Mwenyekiti wa shule pale, pamoja na *Headmistress* au *Headmaster,* ndio afanye kazi ile, *that is wrong*. Hatukusema hivyo, ni kweli kwamba, hela zinatoka hapa zinakwenda moja kwa moja mpaka kwenye shule ya sekondari, kwenye akaunti yao pale. Lakini hii haikumaanisha

kwamba, Mkurugenzi na Madiwani, hawatasimamia shughuli pale na hapa nataka nijibu jambo moja, kuna hii habari inayozungumzwa ya kusema, unajua tunaiadhibu Halmashauri, kwa sababu haikupata hati safi. Nataka nieleze *it is my opinion,* Serikali inachotaka kufanya pale ni kusema, Halmashauri inaundwa na Baraza la Madiwani, ndio wasimamizi wakuu wa mapato yanayoingia pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuambie, mahali popote penye Halmashauri, Madiwani wamesimama kidete kusimamia hela, watapata hati safi. Serikali inachofanya ni kuzuia ile ili mwaka mmoja mkikosa, yale mapato yameingia pale, muwatie mbiringa mbiringa Mkurugenzi na Wakuu wa Idara, msimamie mhakikishe kwamba, hela zinakwenda pale. Mkisema hapa tu wewe bwana pale sio matatizo ya wananchi na wananchi hawakukosea kitu chochote kwa hiyo, peleka hela pale, zitaendelea kutafunwa, Tanzania itarudi nyuma. Ifike mahali tuiadhibu Halmashauri, hatukupi hela kwa sababu hukusimamia hela za Serikali ambazo zilipelekwa pale, *that is the bottom line.* Unaiweka hapo, unasema bwana sisi hatupeleki pale. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya miaka miwili, utaona hati safi zinatokea hapo kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Hai itajua kwamba, mimi nikifanya makosa hapa hela zikitumika vibaya, hatutapata hela tena kutoka Serikalini. Lazima tuliangalie hivyo, baada ya hapo nchi hii itasonga mbele, itakwenda haraka, hatuwezi kila siku kusema Tanzania ni nchi maskini, Tanzania iko nyuma, halafu tunafikiri ni sifa. Sasa Tanzania ni ya wakulima wadogo wadogo, utafikiri ni sifa. Sisi tunataka twende mbele, tuwe na wakulima, tuwe na watu waliopiga hatua kiteknolojia, ndio tunataka kusema huwezi kila siku kutuambia sisi tuko nyuma kimaendeleo unafikiri ni sifa, sisi ni maskini bwana, watu wetu ni wanyonge bwana, tunafikiri ni sifa.

Nitamaliza tu Mheshimiwa Naibu Spika, usiwe na wasiwasi, nataka tu tuiweke vizuri hapa. *(Makofi)*

Sera za Chama cha Mapinduzi, zinataka kumtoa Mtanzania hapa alipo na kumsukuma mbele aonekane ana maendeleo. Ndio mpango wake huo, kuwavusha watu kuona kwamba, wanasoma madarasa mazuri, watoto wetu wanasoma vizuri na wanaishi maisha mazuri. Kwenye hili, nataka niweke mambo yafuatayo vizuri na hii inahusu Serikali, ambapo imedhamilia kusomesha watoto wetu, asilimia 50 ya wanaomaliza darasa la saba, waende shule za sekondari, ndio mpango ulioko hapa. Wale waliofaulu darasa la saba walau asilimia 75, wapate nafasi ya kwenda *secondary schools.* Mpango wa Serikali unasema, watoto asilimia 50, Zanzibar wao wamesema ni wote, hapa kwetu Bara wanasema asilimia 50, waliomaliza darasa la saba wapate nafasi ya kwenda *secondary schools* na katika hao asilimia 50, kama ninakosea, Mawaziri watakaposimama watatusaidia, maana yake naona Waziri ananiangalia.

Asilimia 75 waende *secondary schools,* ili wale ambao wamefaulu, iko tofauti kati ya wale wanaomaliza darasa la saba wakafaulu na wale waliofaulu asilimia 75 waweze kwenda sekondari. Hapa nataka nizungumze, tukienda kwa utaratibu huu hata ukichukua *millenium goals,* hata ukichukua masuala ya dira, ukaenda kwa utaratibu huu, siku itafika hatujamaliza hiyo idadi, hatutaweza,. Ukishaamua kwamba unataka kuwasomesha watoto wako, wasomeshe kama mwendawazimu, yaani unafika mahali unasema mimi sisikilizi la mtu. Nitakupa pale Namibia, wakati Sam Nujoma, ana *endeavour*, ile *endeavour note* yake kwa huyu Rais mwingine, nimelisahau jina lake,

huyu aliyeingia, wakati anaingia pale alikuta wanatumia asilimia 30 kwa ajili ya kutoa elimu kwa watoto wao. Wakati anamwachia mwenzake alimwambia, nakuomba utakapoingia hakikisha asilimia 50, inatumika kwa ajili ya kutoa elimu. Tunazungumza habari ya urithi, ukitaka kuendeleza watoto wetu hapa, wape elimu; maji yatakuja na kila kitu kitakuja. *(Makofi)*

Nataka kusema pale kwangu Siha, kuna Shule ya Sekondari ya Siha, *form one* mpaka *form six*, inaendeshwa na KKKT. Shule ile kama ina nafasi pale na bahati nzuri, Naibu Waziri wa Elimu yuko hapa, Waziri wa Fedha yuko hapa ananisikia, kama wana nafasi pale, wewe usikae unasema hii shule unajua ni ya *private* kwa hiyo, mimi siwezi kupeleka watoto wangu pale. Kama ruzuku ya kumsomesha mtoto mmoja ni shilingi laki mbili, peleka fedha hizo pale Shule ya Sekondari ya Siha ya *private,* somesha watoto wako pale. Kama wewe unazo shilingi laki mbili zako unataka kusomesha watoto, kuna mtu ana *private secondary school* na wewe sasa hivi huna mahali pa kuwapeleka watoto, chukua hela wapeleke pale. Kwa kuanzia, haya mawazo yanaweza yakapuuzwa, lakini kama kweli tumedhamiria kwamba, tunataka kuongeza idadi ya wasomi, ukishamaliza shule hizi tunazosema, chukua watoto warudishe katika hizi za kwako za Serikali uwapeleke pale, tumia hiyo Mheshimiwa Zakia Meghji.

Wamefanya wenzetu, Cuba wamefanya hivyo na dunia imefanya hivyo, usikae tu unang'ang'ania mpaka ujenge zako tu, fika mahali ufanye maamuzi, sema mimi watoto hawa kama ningekuwa na shule, wote ningewapeleka. Sasa sina, lakini ninazo shule za *seminary*, waislamu wamejenga shule zao pale, wana nafasi, mimi nitawapelekea ruzuku ya Serikali, niwasomeshe watoto wangu pale. Nitakapojenga shule zangu hizi zikikamilika, watoto wale watakuwa wamemaliza wamekwenda. Kama tunafanya hivyo kwa *private universities,* tunapeleka ruzuku; *what is wrong with* kupeleka kwenye shule za sekondari? Kama tulikuwa tunapeleka kule; *what is wrong* leo kupeleka pale? *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na karibu tena Bungeni. Mimi nitachangia machache, kuhusu taarifa za Kamati hizi mbili. Kwanza, ninawapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati hizi, kwa kazi nzuri, ambayo imefanyika na ambayo inatuonesha wapi tulipo katika kusimamia shughuli za Serikali. Jana nilisema utaratibu huu wa kupokea taarifa ni mzuri na leo naendelea kuamini baada ya kusoma hizi taarifa ya kwamba, huu ndio utaratibu wa kufanya kazi katika Bunge.

Napenda niseme yafuatayo, ukisoma taarifa zote mbili, zinaonesha mapungufu makubwa tuliyonayo, katika kusimamia kazi za Serikali, kwa wale ambao wamepewa dhamana hizo, pote pameoneshwa matumizi mabaya ya pesa. Pesa kidogo tulizonazo na sio za Serikali Kuu ni za Watanzania, Serikali Kuu haina pesa, hizi pesa ni kodi za wananchi wa Tanzania, hawa wakulima, wavuvi, wafugaji wanapokusanya kusanya, ndipo tunapopata hizi pesa ambazo tunazileta hapa ndani ya Bunge, pamoja na pesa chache zinazoletwa na wafadhili au wale ambao wanasaidiana na sisi katika kujenga Taifa hili.

Kwa hiyo, tunapozungumza Kamati hizi mbili, zinataka kutuonesha jinsi ambavyo katika maeneo yaliyo mengi, pesa hizi za Watanzania hazikutumika vizuri. Lakini pia nilitaka kuonesha ya kwamba, pamoja na mipango ya maboresho, kwa sababu katika mkoa wetu wa Mwanza kila siku ukienda, *DED* hayupo kaenda kwenye maboresho, lakini ukisoma mahesabu yanazidi kuharibika kuliko kuboreshwa. *(Makofi)*

Pamoja na mipango ya maboresho, bado tunazidi kudidimia, kwa hiyo, ninachotaka kuchangia ni kwamba, je, wakati haujafika wa kuchukua hatua? Nadhani nikisema mengi, nitarudia yale yale yaliyo kwenye Kamati, pendekezo langu ni moja, tunayo sheria ya kwamba, Kamati kama hivi zikishafikisha hapa tukazungumza na wametoa mapendekezo na hatukuyakataa, tumekubaliana nayo, tupate taarifa katika kikao kinachofuata, namna ambavyo hayo tuliyokubaliana yametekelezwa. *(Makofi)*

Tusipokwenda hivyo, tutarudi huko nyuma ambapo tutazungumza mpaka jasho litatutoka. Mimi hapa nimeshazungumza juu ya ubovu wa ma-*DED*, ama waweka fedha, anatoka Ukerewe anapelekwa Misungwi, huko ndio kabisa wanapata hati chafu. Misungwi wamepata hati chafu, lakini aliyetuchafua sisi, ndio huyo kaenda kuchafua Misungwi, kwa hiyo, watu wa Misungwi wamenyimwa, wamefungiwa kila kitu, kama tulivyofungiwa sisi. Sasa swali ndio hilo, naomba nisaidiwe, hatima ya maamuzi ya Bunge yanafikia wapi katika utekelezaji wa Serikali na kwa maana hiyo, napendekeza tukubaliane yaliyopendekezwa na hizi Kamati mbili, yatekelezwe na tupate taarifa hapa Bungeni, jinsi yalivyotekelezwa, hapo tutapiga hatua. *(Makofi)*

Napenda tu niongeze lingine, *value for money*, thamani ya kazi kulingana na pesa tulizowekeza mle, hata hii ya mvua, mimi nimekuwa karibu na nyumbani kwetu, kuna daraja lilijengwa kabla sijazaliwa, halijachukuliwa na mvua, lakini barabara zilizojengwa wakati niko Mbunge ndani ya Bunge hili, zote zimekwenda ziwani! Sasa najiuliza; *what is value for money*, ama ile *cement* ya miaka ya nyuma kabla sijazaliwa, ilikuwa ina nguvu? Mimi nafikiria hapo inaonesha wazi, kwa mfano, ukiangalia madaraja mengi haya yaliyojengwa kwenye reli ya kati, yanazaidi ya miaka 70, mbona hayabebwi kama daraja lile la barabara ya kwenda Tanga? Kwa hiyo, tusije tukapata visingizio vya mvua, kwa kazi mbaya iliyofanywa, halafu tukaipitisha, ndio *value for money*. Tumesomea shuleni, mimi shule ya msingi niliyosomea leo ukienda pale, utafikiri imejengwa mwaka jana, sasa hiyo ndiyo *value for money*, ukuta uwe ni ukuta, msingi wa nyumba uwe ni msingi wa nyumba na kama ni zahanati iwe ni zahanati. Mimi nadhani hii wenzetu wametuonesha mahali pa kwenda, sasa nani anachukua hatua?

Sisi tunataka kuchanganya mambo mawili, wakati mwingine Wabunge tunapelekwa hata kufanya kazi ambazo sio zetu, kila mara tunasema Wabunge wafanye hivi, mimi nadhani hii ndio kazi yetu ya kusimamia wale tunaowalipa na wale ambao wamesomeshwa na taifa hili, hizo kazi wazifanye, sisi ni wasimamizi. Hatuwezi tukawa akina bwana kilimo, hatuwezi tukawa madaktari, hatuwezi tutachafua taifa hili kwa kuchanganya wajibu. Sisi wajibu wetu ni huu wa kusimamia na kwa hiyo, kama nilivyosema mwanzo, tuletewe taarifa kama hatua zimechukuliwa, baada ya mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hizi, ama sivyo tutakuwa *roughing stocks.* Wananchi wanatusikiliza, tunazungumza kwa jaziba kuhusu haya mambo, halafu baadaye mafaili haya yanapelekwa kwenye nyaraka *and that is the end of it*. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwa kweli ituletee taarifa.

Kuna masuala ya ruzuku na mengine; je, hatujafika wakati wa *transparency,* tujue namna ya kuzigawa pesa za taifa katika maeneo mbalimbali na iwe wazi, kwa sababu kompyuta ina uzuri wake, lakini pia ina ubaya wake. Kompyuta ubaya wake hasa kwenye mahesabu, mtu akiwa anaichezea kwa *cut and paste,* hawezi kufikiri tena mwaka huu ni bajeti, analeta *page* ile ya mwaka jana, anaongeza anachezea, zile hesabu anaziweka pale. Mantiki na uchambuzi wa nini, tunapaswa kufanya, kwa sababu *value for money* pia inatokana na jinsi ulivyofanya uchambuzi wa nini unachotaka kufanya, ukajiuliza nahitaji watumishi wa aina gani, waweze kuimudu hiyo kazi, nahitaji pesa kiasi gani niweze kugharamia hiyo kazi nitakayoifanya na nitahitaji malighafi ya kiasi gani, kuifanya hiyo kazi. Wakati mwingine *value for money,* haiji kwa sababu umepeleka pesa, mtaalamu hukupeleka, umepeleka mtaalamu hakuna pesa au hakuna malighafi.

Kwa hiyo, vyote hivi vitatu visipokaa pamoja, unajikuta ya kwamba, huna *value for money*, mtumishi yuko kakaa tu au *infrastructure* imewekwa hakuna pesa za kuweza kuitumia ile *infrastructure* na hii lazima tuiweke, tuzuie mahesabu ya bajeti ambayo yanakuja kwa kubambikizwa ndani ya kompyuta, halafu yanajumlishwa yanakuwa sahihi, kumbe hayana mantiki ndani yake ya kuweza kusukuma maendeleo ambayo tunayahitaji. Hili ni suala ambalo nadhani, lazima tuliangalie kwa makini na hasa wakati wa bajeti, nadhani Wabunge tutakuwa tunalichambua zaidi na tumekuwa tukifanya uchambuzi wa makini zaidi. Kwa hiyo, hata hizi pesa za *capital development,* unaposema unapeleka wilaya fulani na nyingine unainyima, umetumia mantiki gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda pia nisisitize jambo moja, ambalo ni zuri, hivi ukishakiuka kanuni ya utumishi, adhabu yake ni nini? Kanuni za utumishi zinakiukwa kila siku na kanuni za hesabu, adhabu yake ni nini? Mimi najua ukikiuka kanuni ya fedha ni kufungwa, kama umekula hata senti moja ya Serikali, unafungwa na watu waliwahi kufungwa. Hivi siku hizi kwa nini tunasema magereza yamejaa, kwa nini hakuna nafasi ya hao wanaokula pesa za Serikali? Kama ni hivyo, tujenge magereza *specifically* kwa wanaokula pesa za Serikali, kuna watu mle ndani ya magereza wameiba kuku, mtu anaiba mamilioni ya Serikali yuko nje ya gereza! Mimi ningependa tubadilishane, huyu wa kuku tumwondoshe, tumwingize huyu aliyechukua mamilioni ya pesa za Watanzania, wala sio za Serikali, ni za Watanzania. *(Makofi)*

Mimi napenda hiyo turudi pale, sasa tuorodheshe, nimetafuta kila Kamati, sikuona mahali ambapo wameonesha orodha ya majina ya watu waliokula pesa, kwani hamkuwaona huko mlikopita? Tunapoenda kwenye *transparency,* mtuambie majina, sio kwamba tumekuta nyaraka zimepotea na nini, mtasema mwalimu fulani kala, *DED* fulani kala na hivyo tuje tufanye uamuzi, sisi ndio tunaopitisha pesa na sisi ndio tunaowalipa mshahara. Sasa haya mambo tunaenda tunazunguka, mpaka tunafika mahali watu wanatuona kama na sisi hatuelewi labda.

Sasa mimi napenda kusema, orodha kama ni siri, iwe siri, lakini ifike mahali, fulani kala kiasi fulani, fulani kaanza kurejesha kiasi fulani, hakuna. Kwa hiyo, napendekeza kwa Kamati hizi, wakati wa mafumbo umekwisha, kama tunaenda kwa mafumbo, hatutalikomboa taifa hili, yaani humu kila mtu ni mafumbo tu, mwisho unaona hivi nikitaka kusema fulani afungwe, namsema nani. Kwa hiyo, *next time,* Mwenyekiti wa *PAC* na Mwenyekiti wa *LAAC,* mtuletee majina na hatua zilizochukuliwa ili tuweze kuamua mambo ya maana, sio tunakaa tunalilia pesa na kumbe pesa zimeshaliwa na watu halafu magereza tunasema yamefurika, kumbe yamejaa wale walioiba kuku. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, orodha yetu ni kubwa sana, bado wachangiaji ishirini na tatu, hao sijawajumlisha Mawaziri ambao watatakiwa kuja kujaribu kujibu hoja kidogo, wala sijawajumlisha watoa hoja wenyewe. Kwa hiyo, orodha yetu ni kubwa, tutaangalia mchana tutasemaje. Kwa hiyo, tukirudi hapa watakaoanza ni Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Omar S. Kwangw' na wengine.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge, mpaka mchana saa kumi na moja.

*(Saa 07:00 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasimamisha Shughuli za Bunge mchana huu, nilikuwa nimesema mchangiaji wetu wa kwanza, atakuwa Mheshimiwa George Malima Lubeleje, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa na Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', ajiandae.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja zilizoko mbele yetu; Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali na Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali na Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kwa taarifa zao nzuri. Kwa hiyo, naziunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naanza na suala zima la ukaguzi wa mahesabu na miradi katika Halmashauri zetu. Kwa bahati nzuri nimewahi kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya kwa muda wa miaka 15, kwa hiyo, nina uzoefu mzuri sana wa shughuli za Halmashauri za Wilaya. Zamani *PAC* ndiyo ilikuwa inafanya kazi zote mbili, kukagua Hesabu za Serikali za Mitaa, pamoja na za Serikali Kuu, lakini baadaye waliona kwamba, kazi hiyo ni nzito na ni kubwa, Kamati moja haiwezi. Ndiyo maana Bunge likaamua kwamba, sasa tuwe na Kamati ya kukagua Hesabu za Serikali na Kamati ya kukagua Hesabu za Serikali za Mitaa. Lakini Kamati hizi zinafanya kazi nzuri na bila Kamati hizi, mimi nina hakika, fedha za Serikali zingetumika vibaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie suala zima la Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Halmashauri za Wilaya, zina miradi na zinapewa fedha nyingi za miradi mbalimbali na wengi wanatekeleza miradi vizuri. Ni Halmashauri chache, ambazo kwa kweli utekelezaji wake siyo mzuri. Kuna dhana potofu, ambayo imejengeka kwamba, Halmashauri zote zinatumia fedha vibaya, si kweli. Halmashauri nyingi zinajitahidi kutumia fedha vizuri na zinatumika kwa makusudi yaliyokusudiwa kwenye miradi ya maendeleo. Ni Halmashauri chache tu, ambazo kwa kweli hazifuati ile

Sheria ya *Financial Memorandum,* pamoja na *the Public Financial Act,* lakini Halmashauri nyingi zinafuata taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ina utaratibu wa kukagua mahesabu, pamoja na miradi katika Halmashauri zote za Wilaya, Halmashauri za Miji, Manispaa, pamoja na za Majiji. Kabla ya kuanza kwa ukaguzi wa hesabu hizi, Halmashauri nyingi zilikuwa zinapata hati chafu. Mimi ninakumbuka katika miaka ya 1990, hali ya mahesabu ya Halmashauri za Wilaya ilikuwa mbaya sana. Fedha zilikuwa zinatumika na zilikuwa hazina mwenyewe. Lakini baada ya kuundwa Kamati hii ya Hesabu za Serikali za Mitaa na kuanza kukagua mahesabu, pamoja na miradi mbalimbali na kufuatilia kila Halmashauri, hivi sasa tunaridhika kwamba, Halmashauri nyingi zinatekeleza majukumu yake vizuri na wanafuata sheria katika matumizi ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba kwamba, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, iendelee kukagua hesabu za Halmashauri za Wilaya, pamoja na kufuatilia miradi mbalimbali. Hii itasaidia Halmashauri nyingi kufanya vizuri na kupata hati safi. Sasa hivi ni Halmashauri chache tu, ndizo zinapata hati chafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri zetu, Halmashauri ya Wilaya ni Madiwani pamoja na watendaji. Sasa lipo tatizo, kuna Mheshimiwa Mbunge mwenzangu asubuhi hii amelizungumzia kwamba, unafanyika ubadhirifu katika Halmashauri, lakini badala ya kuchukuliwa hatua yule mtu aliyehusika, Halmashauri ya Wilaya, inanyimwa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano hai kwamba, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, kwenye bajeti ya mwaka 2006/2007, tumenyimwa fedha shilingi milioni 500, eti kwa sababu taarifa hazikuandaliwa vizuri, kwa sababu sijui kulikuwa na ubadhirifu, lakini wale wote waliofanya ubadhirifu, hawakuchukuliwa hatua. Wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa, walikosa shilingi milioni 500, eti kwa sababu kuna watu wachache, waliotumia vibaya zile fedha!

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi milioni 500, zingesaidia miradi mingi sana katika Wilaya yetu ya Mpwapwa. Tuna matatizo ya maji katika Wilaya ya Mpwapwa na ni matatizo makubwa sana. Hivi sasa wananchi wanapata tabu sana, maji hayatoshi. Lakini vilevile, fedha hizo zingesaidia miradi ya barabara na zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbaya zaidi, unapotokea ubadhirifu na unagundulika na Kamati ya Hesabu ya Serikali za Mitaa, tayari imeshakagua na kutoa taarifa Serikalini kwamba, katika Halmashauri fulani, tumegundua kuna ubadhirifu na waliohusika wapo wanatajwa. Basi ni vizuri Serikali iwe inachukua hatua haraka, badala ya kuwahamisha watendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anaharibu Kongwa, anaharibu labda Bariadi, anaharibu Kiomboi, Iramba, analetwa Mpwapwa au anapelekwa Karatu. Wakati umefika sasa mtu akiharibu, basi achukuliwe hatua hata kama ni kusimamishwa kazi, lakini suala la kumhamisha inakuwa si zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawapa adhabu wananchi bila sababu. Kwa sababu Mpwapwa, *Accounting Officer* aliyehusika yupo, Wahasibu waliohusika wapo, lakini

mnanyimwa shilingi milioni 500, unawapa adhabu wananchi. Siyo Mpwapwa tu ni Halmashauri nyingi, kwa mfano, katika Mkoa wa Dodoma ni Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa tu ndiyo walipata fedha, lakini wengi hatukupata karibu Halmashauri zote za Mkoa wa Dodoma, lakini waliofanya ubadhirifu huo wapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, kuzinyima fedha Halmashauri za Wilaya eti kwa sababu Mtendaji amesababisha ubadhirifu au Mtendaji ametumia vibaya fedha, kwa kweli hatuwatendei haki wananchi wa nchi hii. Wapewe fedha, wahusika wachukuliwe hatua, hata kama ni kusimamishwa kazi wasimamishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba, Halmashauri ni Madiwani, pamoja na Watendaji, ndiyo wanaosimamia mapato na matumizi. Kamati ya Fedha ndiyo inayosimamia mapato na matumizi katika Halmashauri, lakini tulishakubaliana na Serikali ilishaahidi kwamba, baada ya uchaguzi, Madiwani wapewe mafunzo angalau ya muda mfupi tu, waweze kuelewa majukumu yao na waelewe mipaka yao ya kazi. Lakini sijui hilo kama limekwishafanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukawa tunawalaumu sana Madiwani kwamba, hawasimamii mapato na matumizi, lakini tunawalaumu Madiwani; je, tumewapa mafunzo angalau ya muda mfupi? Sasa tunaanza mwaka wa pili, tangu tumefanya uchaguzi mwaka 2005, kwa hiyo, naishauri Serikali mafunzo kwa Madiwani yatolewe ili waweze kujua majukumu yao, wana majukumu mazito na makubwa ya kusimamia mapato na matumizi. Kazi ya Watendaji wale ni utekelezaji tu, lakini Madiwani wawe *policy makers*, kazi yao ni kutoa maamuzi ya kisera. Ndiyo maana kuna Halmashauri nyingine, unakuta hata mahusiano kati ya Madiwani na Watendaji siyo mazuri, kwa sababu inawezekana Madiwani hawajui mipaka yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali, wakati umefika sasa, semina au mafunzo ya muda mfupi yatolewe kwa Madiwani kwa nchi nzima ili waweze kujua mipaka yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ndiyo ulikuwa huo. Lakini napenda nirudie tena, Kamati hizi mbili ni muhimu sana na ninaomba Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, wanapopeleka mapendekezo Serikalini kwamba, kuna ubadhirifu kwenye eneo lolote lile, basi Serikali ichukue hatua haraka sana, badala ya kusubiri tuanze sisi Wabunge tena kulumbana na Serikali bila sababu. Fedha hizo ni za Serikali na ni fedha za walipa kodi, lazima zitumike vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti tunaomba fedha nyingi zipelekwe vijijini. Fedha zinabaki Wizarani, najua Wizara ina majukumu mengi, lakini miradi ya maendeleo mingi iko vijijini, kule ndiko tunakojenga shule, tunakojenga zahanati, barabara na huduma zote za kiuchumi na kijamii. Kwa hiyo, nashauri katika bajeti ijayo, fedha nyingi zielekezwe vijijini kuboresha miundombinu ili kurahisisha mawasiliano, pamoja na huduma mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na ninarudia tena kusema kuwa, ninaunga mkono hoja hizi mbili kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, nichangie kidogo katika hoja zilizoko mbele yetu. Lakini awali ya yote, naungana na wenzangu katika kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati hizi mbili, kwa taarifa nzuri na takwimu nyingi nzuri za kutosha na za kutupa mwanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa kuanzia, nichangie hoja iliyoko katika ukurasa wa 36 inaenda mpaka ukurasa wa 38, inayohusu fungu la 47. Katika fungu hili, nimesoma kwa makini, lakini kwa uchungu mkubwa, pia kwa sababu kama taarifa hii ni sahihi ilivyoandikwa hapo, basi kuna Ugonjwa wa Kansa umeingia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni jana tu niliuliza swali kuhusu nyumba za Serikali katika swali namba 36, nadhani Waheshimiwa Wabunge, watakumbuka jibu la Serikali kuhusu hoja hiyo. Sasa siku moja tu baada ya jibu lile, leo tunapata taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali, iliyothibitishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na iliyothibitishwa na Serikali, inayoonesha madudu katika nyumba mbili. Ni nyumba iliyo katika *Plot* Namba 106, *Upanga Avenue Oysterbay* na *Plo*t ya pili ni Namba 474 iko sehemu inayoitwa *Mindu Street,* Upanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama taarifa hii ni sahihi na nitaomba Serikali inithibitishie baadaye, hapo kumetokea mambo mawili. Kwanza, nyumba isiyo ya Serikali imenunuliwa na Serikali, lakini baadaye ikauzwa tena kwa viongozi wa Serikali au kwa watumishi wa Serikali. Lakini kilichofanyika hapa ni kitu ambacho ni vema Watanzania wote wakakielewa ili tunapopiga kelele kwamba, kuna madudu katika uuzaji wa hizo nyumba za Serikali, waweze kuelewa ni kitu gani kimetokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu tulizonazo hapa, zinaonesha kwamba, nyumba hiyo ilinunuliwa na Serikali kabla haijauzwa kwa shilingi milioni 220. Shilingi milioni 220, kwa watu wa vijiji wasioelewa hayo mahesabu marefu ni sawa na zahanati nne zilizokamilika. Lakini nyumba hiyo ikauzwa na Serikali kwa utaratibu huo ambao si wa tenda ya wazi na kama nita-*quote* maneno ya Naibu Waziri wa Miundombinu, jana aliita *single sourcing,* ambapo *single sourcing* nayo ina utaratibu wa kisheria, lakini haukuwa kweli. Sasa kwa kuwa sikuwa na namna ya kumjibu Naibu Waziri, natumia nafasi hii pia kumjibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba hiyo ilinunuliwa kwa shilingi milioni 220, ikauzwa kwa mtumishi wa Serikali kwa shilingi 56,640,500 na wanatumia lugha hapo ya ajabu; wanasema nyumba hizo zimeuzwa kwa watumishi hawa, kwa kuwa mishahara ya watumishi wa Serikali ni midogo na kwamba, hawana uwezo wa kununua nyumba hizo kwa *market value*. Utaratibu mahsusi na wa makusudi wa kuwawezesha kununua nyumba hizo utumike. Kwa hiyo, nyumba inanunuliwa na Serikali kwa shilingi milioni 220 na inauzwa kwa mtumishi wa Serikali na hapa inavyoonekana, mtumishi huyo ni kigogo, anayesemekana hana uwezo wa kununua nyumba hiyo kwa *market value*. Kwa hiyo, anainunua nyumba hiyo kwa bei ya kutupa, shilingi milioni 56, ambayo ni sawa na zahanati mmoja. Wanaendelea mbele wanasema, wameuza nyumba hiyo bila kuangalia bei halisi ya eneo iliyopo hiyo nyumba, nimesema iko *Uganda Avenue Oysterbay. Oysterbay* kwa wale wanaojua thamani ya ardhi, eneo peke yake ni mamilioni ya hela.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba ya pili, ni nyumba namba 474, yenyewe ilinunuliwa kabla ya kukabidhiwa kwa huyo mtumishi wa Serikali kwa shilingi milioni 190, lakini ikauzwa kwa mtumishi wa Serikali kwa shilingi 66,460,500, bei ya kutupa. Naibu Waziri, jana wakati ananijibu alisema kwamba, yeye ndiye mtaalam wa *procurement* na kwa sababu ni mtaalam, anajua *single source*. Lakini Serikali imetoa jibu hapa kwamba, kuna Waraka Namba 7 wa Baraza la Mawaziri wa mwaka 2001, nyumba hizo zimeuzwa kinyume na maelekezo ya Waraka wa Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisipoteze muda, ninataka kujua kutoka Serikalini, wakati Naibu Waziri alipojibu swali ndani ya Bunge hili, alikuwa anatania, alikuwa anafanya mchezo, alikuwa anapotosha Bunge, alikuwa hajui kwamba, kuna nyumba zimeuzwa kwa bei ya namna hiyo au alikuwa hajui kwamba Mheshimiwa Mbunge anapouliza swali, ana taarifa naye ya nyumba za aina hiyo na Naibu Waziri alitaka kuzificha? Nitapenda kupata taarifa ya kweli kwamba, Ibara ya 63 katika nchi hii, imewekwa kwa utani au ni ya kweli? Kama ni ya kweli; je, inatumika namna gani kuisimamia Serikali, wakati Mawaziri hawatoi majibu sahihi kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama taarifa hii ni sahihi ...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo Mwongozo wa Naibu Spika. Kanuni gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (BUNGE):** Kanuni namba 55.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Mbunge, atueleze hizo nyumba anazozungumzia, ambazo zimeuzwa kinyume na Waraka wa Baraza Mawaziri, atuthibitishie hilo na atupe ufafanuzi.

**NAIBU SPIKA:** Katika hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya *Public Accounts Committee,* amesema kwamba, kuna nyumba zilinunuliwa kwa bei hizo zilizotajwa na kuuzwa kwa bei ndogo zilizotajwa, iko ndani ya taarifa yenyewe. Kwa hiyo, naondoa kuhusu utaratibu, endelee Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuhusu nyumba zilizouzwa kwa watumishi wa Serikali, lakini jambo ambalo nilikuwa naliulizia hapa ni suala la kwenda kinyume na Waraka wa Baraza la Mawaziri. Nilitaka kupata ufafanuzi huo, atuthibitishe kwamba, jambo lililofanyika lilikuwa ni kinyume na Waraka wa Baraza za Mawaziri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, sipendi kutumia muda kwa hili, kwa sababu linafahamika, kwa hiyo, naomba tuendelee. Hili linafahamika. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaomba dakika zangu zilizotumika zilindwe na bahati nzuri taarifa ninazotumia ziko

kwenye kitabu, huenda hata Mheshimiwa Waziri, labda hajaangalia kitabu hicho. Namwomba arejee ukurasa wa 37 atapata taarifa aliyokuwa anaiomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa namalizia katika hoja hii kusema kwamba, iwapo taarifa hizi ni za kweli, hii ni dhambi kwa sisi Watanzania kwamba, nyumba ya Serikali inaweza ikanunuliwa kwa bei hiyo na ikauzwa kwa bei ndogo kwa mtumishi wa Serikali.

Sasa ili nijue kama kweli uzito huu ninaosema ni wa kweli, napenda Serikali inihakikishie na Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, anipe taarifa sahihi. Napenda kujua watumishi hao kwa sababu jana Naibu Waziri wa Miundombinu, alisema hawezi kunipa majina kwa kuwa ni mengi na mimi niliridhika kwamba, majina 7,000 kwa kweli ni mengi, lakini majina mawili siyo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, pamoja na Serikali, tupate majina ya watu wawili hao, waliouziwa hizo nyumba, tujue na vyeo vyao tuweze kujua kama kweli hao ni watumishi ambao hawajui *market value*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, nangependa niseme sasa kwamba, kwa kuwa hili limejulikana, pamoja na kwamba, kuna Kamati iliyoundwa na Serikali, jambo hili limekwishafika Bungeni. Kama Azimio la Kamati halitoshi, Kamati imesema kwamba, hili liishie hapo. Napenda kusema, Bunge hili likubali nyumba hizo zirejeshwe Serikalini au hela tofauti ambayo haikulipwa ile iliyonunua nyumba, kwanza zile fedha zirejeshwe Serikalini, ni jasho la Watanzania, zinapaswa kurejeshwa au mhusika alipe kiwango kamili kama zilivyotumika katika kununua hizo nyumba. Ile nyumba ya shilingi milioni 220 na aongezee tofauti ya shilingi milioni 56 alizolipa na bahati nzuri walizilipa zote. Kwa hiyo, hao wanaonekana ni watu wenye uwezo, kama walilipa fedha zote kwa mara moja, mimi naamini hao si watu kama mimi na wewe Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii kwa kuwa jana nyumba zilielezwa kwamba ni nyingi na haiwezi kuletwa taarifa na kuna Kamati iliyoundwa na Serikali, ambayo iko chini ya Mheshimiwa B. H. Nyundo na ni Kamati ya Serikali.

Ninaomba sasa kwa kuwa hizi nyumba mbili tumejua kuna uchafu na katika nyumba nyingine ambazo sisi pia tuna taarifa kwamba, zimeuzwa kwa mtindo huo huo na kwa kuwa Serikali haikutaka kunipa majibu, tunaomba taarifa ya Kamati hii iwe taarifa ya Bunge na iwasilishwe kwenye Bunge lako Tukufu katika Kikao chake cha mwezi Aprili, 2007, ili tuweze kupata taarifa sahihi ya jinsi mali hii ya Watanzania ilivyotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhambi kwa sisi Bunge, kuachia mali za wananchi zinatumika kwa mtindo huu, pamoja na kwamba, Serikali haikutaka kutoa jibu kwa kuwa imeunda Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, napenda pia nichangie kidogo katika mambo yanayohusu Wizara ya Nishati na Madini, fungu la 58 na kwenye kitabu chetu ipo kwenye ukurasa wa 39.

Naomba nimkumbushe yeyote atakayependa, ninazungumzia taarifa za Kamati, ambazo zimeandikwa na ziko mbele yetu. Kwa hiyo, kila mmoja kabla hajatoa *point of order,* naomba asome kwanza *pages* hizo, nimetoa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *page* hiyo, jambo linalotisha ni taarifa inayosema kwamba, kufuatana na taarifa za Wizara ya Fedha na *TRA*, pamekuwa na hasara kubwa ambazo zimekuwa *declared* na Kampuni ya Migodi, kwa mujibu wa taarifa. Hasara ya shilingi bilioni 1.3. Sasa mimi hii taarifa ya shilingi bilioni 1.3 kwa rekodi iliyoko, wenzangu wamekwisha zungumzia na mimi sitaki kuizungumzia sana, lakini nataka kuzungumzia kwa *angle* tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ni taarifa ya jinsi Serikali inavyokosa *documents proper* kutoka kwa makampuni yetu ya migodi na jinsi makampuni haya yanavyoandika taarifa zake na ku-*under declare* jinsi walivyopata faida au harasa na hizi ndizo ukizijumlisha zinaleta hiyo *total* ya shilingi bilioni 1.3.

Mheshhimiwa Naibu Spika, kitu kinachonishtua ni *under declaration,* ambayo inatolewa hapa na nina taarifa ambazo katika uchunguzi wangu, inaonekana hawa watu hawa-*collaborate* hata na yule tuliyemchagua, tunayemlipa asilimia 1.9 ya thamani ya dhahabu yetu, ametoa taarifa Serikalini, lakini bado wale wahusika wanashindwa ku-*collaborate* na kutoa ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa *za under declaration,* zimepelekwa Serikalini. Taarifa hizi kama mimi mahesabu yangu na utafiti wangu unavyoonesha, kuna kampuni hapa ime-*under declare* kwa thamani ya shilingi milioni 589, ime-*declare* ina hasara ya shilingi milioni 760.3, lakini uchunguzi umegundua shilingi milioni 589, kwa hiyo, wame-*under declare* kwa zaidi ya shilingi milioni 170.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unaweza kwenda kwa makampuni yote na nina taarifa za makampuni karibu matano. Serikali ambayo ina meno, Serikali ambayo imemuweka mkaguzi, inashindwaje kupata fedha hizi kwa mtu huyu, kiasi kwamba tungepata shilingi bilioni 1.3, leo sisi tusingehitaji kwenda kwa mfadhili yeyote kukopa hela, tungetumia fedha zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Serikali, inipe taarifa sahihi kwamba, hao watu siku zote tumesema wametukalia shingoni, hawatii sheria zetu, hawaitii hata Serikali, wanatafuna kwa kiwango kikubwa fedha zetu kwa njia wanazotumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejibu tu kirahisi hapa Bungeni mara nyingi kwamba, tuna wakaguzi wetu kule, lakini wakaguzi wamefanya kazi yao, fedha hizi zimeshindakana kurudi. Ninapenda kupata taarifa kamili, Serikali sasa inafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri, mwaka 2006 alijaribu kutoa hata *deadline,* lakini bado hawajafanya kazi. Kutokana na muda uliobakia, kuna makampuni yamekataa kutoa taarifa, kati ya makampuni hayo ni Kampuni ya MEREMETA, yule mthamani wetu Bwana Alex Stuart, ameshindwa kupata rekodi kwa sababu MEREMETA hawapeleki taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, MEREMETA ni kampuni ya Serikali, leo tunafahamu imejibiwa ndani ya Bunge, MEREMETA haipo tena. Tunafahamu kule MEREMETA, hata machimbo yamefungwa, lakini hatujakusanya chochote. MEREMETA ni kampuni ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nipate jibu la Serikali, hii kazi ambayo imeshindikana, kwa sababu hawa-*collaborate*, hata huyo wa kwetu wa Serikali anashindikana, hata sisi wenyewe tunashindwa kupeleka; kuna nini hapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tukifika mahali tukasema kuna wingu la rushwa, kwa sababu sisi wenyewe wa Serikali ndiyo wahusika wa MEREMETA; hapa nani atakataa? Tunapenda wingu hilo liondolewe, Serikali itupe taarifa sahihi, kwa nini MEREMETA haikutoa taarifa kwa yule wala haiku-*collaborate* kwa yule mtu ambaye alifanya ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka ningependa kuhoji pia suala lililoko chini ya kifungu cha *Environmental Budget* katika madini. Kwa mkataba uliopo, migodi yote inatakiwa kuchangia kwenye mfuko wa kulinda mazingira na walitakiwa kuweka fedha kwenye mfuko huo ili siku wanapoondoka, tusibakiwe sisi Watanzania na mashimo.

Katika mfuko huo, kwa hesabu ya yule mtafiti, kama hesabu zetu ni sahihi, leo tulitakiwa kuwa na *dollar* za Kimarekani milioni 50. Tunataka kuiuliza Serikali, taarifa hii wamepelekewa na Alex Stuart, hela hizo ziko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itupe taarifa, hizo fedha ambazo Alex Stuart tunayemlipa kwa asilimia 1.9 ya thamani ya dhahabu iliyouzwa, hizo fedha ziko wapi? Zilitakiwa kuwekwa kwenye *ESCRO Account,* lakini hatujapata taarifa, hiyo *ESCRO Account* iko mahali gani? Haya ni mambo ya msingi na tusingependa kuyaachia hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa katika Taarifa ya Kamati wanatuambia kuna Makampuni haya ya madini, kuna *missing documents,* kuna taarifa ambazo hazijawasilishwa zinasemekana zimepotea au hazipo au hazionekani zipatazo 6,762 na kwa mahesabu ya haraka haraka yanakisiwa kuwa na thamani ya dola za Kimarekani 250,399,040. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu yeyote anayefuatilia utaratibu wa mahesabu kwenye Halmashauri kitabu kimoja cha *HW5* kikipotea aliyekipoteza anakamatwa, anapelekwa lupango. Hizi ni fedha za Serikali *USD* milioni 250 zina thamani karibu shilingi bilioni 32 hazijulikani. Wahusika wameachiwa, Serikali imekaa kimya. Ndiyo Serikali hii hii inayowakamata wale wadogo leo inawaachia wakubwa, inaeleza nini Bunge hili kwamba mabilioni 32 Serikali imekaa lakini wadogo wanakamatwa wanapelekwa lupango labda kwa ajili ya kitabu kimoja cha shilingi 50 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ningependa nipate ufafanuzi, kwenye kitabu hiki wanasema Mfuko wa Barabara fedha zilizotengwa zaidi ya shilingi bilioni nne zilizotakiwa kupelekwa Halmashauri na Ujenzi hazijapelekwa. Kule kwenye Halmashauri tunaambiwa kwamba uki-*allocate* fedha, ukihamisha mahali pengine unaadhibiwa. Tunaomba kuuliza Waziri wa Fedha ambako hizi fedha hazikupelekwa

ametumia kwa kazi nyingine na yeye anaadhibiwa adhabu gani? Hatuwezi kuwaadhibu kule kwenye Halmashauri tukaacha kujiadhibu sisi Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kupata majibu mimi pamoja na kwamba taarifa ni nzuri lakini nitasita kumuunga mkono.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia taarifa ya Kamati hizi mbili. *(Makofi)*

Kabla sijafanya hivyo naomba kwa niaba ya wananchi wa Babati niungane na Wabunge wenzangu katika kutoa rambirambi kwa kifo cha aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Bunge Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti na Mwenyezi Mungu ailaze roho yake pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Mataifa. Vile vile naomba niwapongeze Mawaziri walioteuliwa, Mheshimiwa Bernard Membe kuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, lakini na vile vile Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia mambo ya Bunge. Vile vile naomba niwapongeze Mheshimiwa William Ngeleja, Mbunge wa Sengerema kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Gaudence Kayombo kuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pongezi hizo lakini vile vile niungane na wenzangu katika kuwapongeza hawa Wenyeviti wawili, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mwenyekiti wa *PAC* na Mheshimiwa Mgana Msindai, Mwenyekiti wa *LAAC.* Kwa kweli kwa taarifa nzuri sana ambazo kwa kweli ziko mbele yetu ni taarifa ambazo nimeona zina takwimu nyingi za kutosha na kwa kweli zimejielekeza vizuri, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za Kamati za Bunge ni muhimu sana, ukitaka kujua picha halisi ya utendaji wa Serikali mahali pa kuzipata ni kupitia taarifa za Kamati za Bunge. Picha halisi ya Serikali ndiyo tunaiona. Kwa hiyo, Taarifa za Kamati za Bunge ni muhimu sana na mimi napendekeza kwamba kwa kuwa Bunge linakaa mara nne kwa mwaka na kwa kuwa vile vile Kamati za Bunge kila kabla ya Mkutano wa Bunge zinapata kikao cha wiki mbili, haiwezekani Taarifa za Kamati zikatolewa tu mara moja kwa mwaka au tena kwa bahati kama hii ya siku mbili tatu za mwisho wa Bunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, napendekeza kwamba Kamati ziko sikumbuki vizuri lakini 15 tuseme. Kila wakati wa kikao cha Bunge Kamati tano zinaweza zikatoa taarifa na hivyo tutakuwa na Taarifa za Kamati katika kila kikao cha Bunge ukiacha kikao cha bajeti. Kwa hiyo, ni muhimu sana au itengwe wiki ya Taarifa za Kamati, vinginevyo hatutaisimamia Serikali vizuri kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kile kifungu cha 63 kwamba kazi ya Bunge ni kuishauri na kuisimamia. Sasa ni lazima basi kazi hizi ambazo tunazifanya kwa kusimamia tuzione na zijadiliwe na kila Mbunge na wananchi wazipate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mengi yamesemwa basi itabidi kutafuta yale mengine ambayo kwa kweli hayakusemwa sana na kujaribu kwa kweli kujielekeza kwenye mambo ambayo hayakuzungumzwa sana. La kwanza ni suala la mgao wa fedha. Katika suala la mgao wa fedha ninachoona sasa hivi fedha zinachelewa sana. Kwa sababu sasa hivi fedha zimegaiwa, tumeshamaliza robo ya pili lakini ukiona magazeti juzi juzi ndipo mgao wa fedha kwenda kwenye Halmashauri ndio umetokea. Mimi kabla sijaondoka jimboni kwangu kwenda kwenye Kamati za Bunge katikati ya mwezi Januari, 2007 nilikuwa najaribu kumwuliza Mkurugenzi wangu kama mgao wa fedha umefika, ulikuwa haujafika. Tuko robo ya pili imekwisha karibu tunaanza robo ya tatu, sasa robo ya pili inaanza Novemba, Desemba na Januari imeshakwisha, leo tuko Februari ndizo fedha za robo ile ya pili ndizo zinatoka. Sasa athari yake ni kubwa sana. Kwanza miradi inachelewa sana kukamilishwa, lakini pili fedha zinapofika gharama zinapanda na zinabadilika. Kwa hiyo, bajeti nzima makisio yote yanavurungwa na hali hiyo.

Lakini vile vile watendaji wetu wanapata matatizo, inabidi Wakurugenzi wakafanye majadiliano labda na wafanyabiashara au wenye vifaa, waende wakafanye mapatano ambayo yanaleta mianya mingi hapo, unaweza ukapata mwanya wa rushwa vile vile kwa sababu inabidi Mkurugenzi aende akafanya mazungumzo na wafanyabiashara na kadhalika ili aweze kusogeza zile kazi ambazo amepewa.

Vile vile hali hii inawadhalilisha na viongozi wengine. Kwa mfano hata Wakuu wa Wilaya usipompelekea fedha kwa muda unaotakiwa atafanya nini. Tunawadhalilisha wanakwenda kupiga magoti mahali ambapo pengine haikuwa lazima ili apate mafuta aende akafanye shughuli za Serikali ambazo ni muhimu. Kwa hiyo, tunaomba sana Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba fedha ziwe zinatolewa katika kila robo kama inavyotakiwa. Kwa hiyo, nilitaka kwanza nisisitize hilo. Vile vile hata watumishi. Malalamiko mengi yanakuja kuhusu watumishi. Kwanza wakati fedha hazipo hawafanyi kazi, zikichelewa na wengine madai yao nayo yanachelewa. Kwa hiyo, nataka nisisitize hilo kwamba kwa kweli fedha ziwe zinapelekwa kwa wahusika kwa muda unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linalohusiana na mgao wa fedha ni suala la Serikali kupeleka fedha mwishoni mwa robo ya mwisho kabisa karibu na mwezi wa tano pale Juni ndiyo Serikali inapeleka fedha. Sasa zinapelekwa nyingi kweli wakati ule. Wakati ule ndio watendaji wa Serikali ndivyo wanavyobabaika. Fedha zinatumika visivyo na ndiyo mwanya wa ubadhirifu unatokea pale. Kwa sababu fedha zimepelekwa nyingi kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, matumizi yanatafutwa badala ya kwenda sasa kwenye ile miradi matumizi yanatafutwa na hata wengine wanashindwa kutumia fedha inabidi kwa taratibu lazima zirudi Wizara ya Fedha, zirudi Hazina. Kwa hiyo, mtindo wa kupeleka fedha nyingi mwisho wa mwaka ingekuwa vizuri waachwe fedha zifuate taratibu za kawaida za kupeleka fedha katika kila robo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nilidhani ni vizuri ningeliongelea kidogo ni suala la zabuni *(tender),* katika ngazi za Halmashauri ya Wilaya na Miji, tuliondoa Waheshimiwa Madiwani. Nadhani lengo la kuwaondoa Waheshimiwa Madiwani ni kuepuka mwanya wa kutokea rushwa na vile vile pengine upendeleo. Lakini sasa tumefanya nini? Mwenyekiti wa *Tender* nadhani ni Mtendaji Mkuu wa Halmashauri na wataalamu wake, afadhali hata Madiwani walipokuwepo siri ilikuwa inaweza kutoka kwamba siku ya pili unaweza ukajua hawa wamehongana kiasi gani au

mtu fulani amefanya nini. Sasa hivi siri ndiyo haitoki kwa sababu Mtendaji Mkuu, wale walioko chini yake ni watumishi wake unatazamia waseme nini, wakatae *tender* ipi. Watatoa *tender* ambayo yeye anaitaka na hawatasema hiyo siri kwa sababu ni watumishi wa chini yake.

Kwa hiyo, kuwaondoa Madiwani hatujafanya kitu bado Serikali ifikirie kwamba tufanye nini katika eneo hilo. Labda tutafute Bodi ya Tenda sasa ambayo itakuwa na mchanganyiko wa maeneo yote za sekta zote pengine itasaidia. Sijui tunakwepa nini? Diwani ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata anakalia kikao cha Serikali yenye maamuzi. Sijui kwa nini tuliwaondoa. Mimi sioni ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baya zaidi ni kwamba Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya anakwenda kusaini mikataba ambayo imekwishapitishwa baada ya tenda na kazi kuanza. Mwenyekiti wa Halmashauri ndiyo anakwenda anasaini halafu baadaye taarifa zinapelekwa kwenye Kamati. Kwa hiyo Kamati ya Fedha kwenye Halmashauri zetu kwa kweli ni mihuri tu. Tenda zimeshatolewa, kazi zimeshaanza Mwenyekiti wa Halmashauri anakwenda kuanguka pale anaweka mkono maana yake nini? Mimi sijui kwa nini Wenyeviti wanakubali jambo hilo. Sijui kwa nini wanakubali. Hili ni tatizo kubwa kwa sababu hatajua kwamba ni nini kimefanyika, yeye anakuja kusaini tu sasa tunarudi ile enzi ya Carl Peters jamani. Hebu tuache hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani ni vizuri vile vile nizungumzie suala la mapato ya Halmashauri yanayotokana na viwanja. Halmashauri kwenye miji zinachukua maeneo kwa ajili ya kuwapa watu na kujenga, lakini jambo linaloonekana ni kwamba viwanja vya watu ambao wamekaa miaka mingi katika eneo hilo vinachukuliwa. Kwa mfano, mtu anaweza kuwa na eka moja, labda nitoe mfano wa Babati ambao naufahamu vizuri. Mwananchi anaweza kuwa na eka zake mbili au moja karibu na mji hapo na kwa sababu sasa kuna mji basi sheria zinataka viwanja vipimwe akipewa mtu pale kiwanja kimoja thamani ya ardhi ya eka moja kwa Halmashauri ya Mji wa Babati ni shilingi 248,000. Lakini Halmashauri ya Wilaya inaweza ikatoa kwenye kiwanja hicho baada ya kumfikia huyo mwananchi inaweza ikatoa viwanja hata vinne tena vikubwa tu.

Lakini na Halmashauri yenyewe ikaja ikawapa viwanja watu wengine kwa fedha nyingi sana mara tano au hata mara kumi. Sasa huyu ambaye kwa kweli huyu ambaye kwa kweli amekaa pale na maisha yake shilingi 248,000 miaka yote alikuwa anasubiri ardhi, anasomeshea watoto wake ndiyo chakula chake unampa 248,000. Lakini wewe mwenyewe Serikali unakwenda tena kutoa kiwanja hicho kwa mtu mwingine ambaye anaweza kujenga ghorofa pale au nini kwa zaidi ya shilingi milioni moja au mbili au tatu.

Kwa hiyo, naona jambo hili sio sahihi hata kidogo, ni vizuri kwenye zile sheria ambazo zinakuja za ardhi na mambo ya mipango miji jambo hili likaainishwa vizuri, thamani ya ardhi ijulikane vizuri ili wananchi wetu tusiwapore haki yao kwa kweli. Ni kinyume kabisa kumwondoa mtu kwa kiwango ambacho anapaswa alipwe ili aweze kukidhi mahitaji yake halafu unamlipa kwa kiwango kidogo, kwa kweli si jambo zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine sasa niende kwenye suala la *PAC* naona muda umekwisha lakini malipo wanayoonesha haya ya bilioni 58.6 ambayo yanasemekana aidha, yana nyaraka pungufu au bila nyaraka. Fedha ambazo zinazoonekana pale kwa vifaa vilivyolipiwa ambavyo havikuletwa, vilivyonunuliwa bila ya *tender,* vifaa ambavyo

vimepunguzwa zabuni. Uzalendo uko wapi kwa watumishi wetu. Tatizo hapa ni uzalendo lazima tuwafundishe watumishi wetu wawe wazalendo wa nchi hii. Serikali katika kipindi kilichotajwa imeshindwa kukusanya maduhuli karibu ya bilioni 20.7. Fedha hizi zingepatikana zingesaidia tatizo hata la sasa ambapo Serikali inapata taabu sana katika kupunguza walau makali ya asilimia 40 ya wanafunzi ambao wanatakiwa walipe kwenye Bodi ya Mikopo. Wala hata Mheshimiwa Rais asingekuwa na matatizo makubwa. Fedha nyingi hazikusanywi na taarifa inaonyesha hapa asilimia karibu nusu ya makusanyo yalikuwa kama asilimia 45.85 ina maana zaidi ya nusu ya miradi ilikuwa haitekelezwi katika kipindi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata wanafunzi wanapoandamana wa Vyuo Vikuu wanatoa meseji, wanao ujumbe kwamba hatufanyi kazi zetu vizuri, tukifanya kazi zetu vizuri hata wao watasoma vizuri, watapata unafuu pamoja na sera ya elimu ya juu ya uchangiaji wanaweza kupata nafuu. Kwa hiyo, nilidhani kwamba Serikali itafute sasa utaratibu wa kuhakikisha kwamba kwa kweli kama ni makusanyo ya mapato basi tukusanye mapato walau zaidi ya asilimia 90. Haya matatizo mengine mengine yaliyo kwenye sekta ya elimu kwa kweli yapungue.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kule mkoani tuna kitu kinaitwa *RCC,* Kamati ya Ushauri ya Mkoa. Kamati hizi tunaomba kuwe na ratiba maalum ili na sisi Wabunge tuweze kushiriki vizuri. Lakini unakuta kila mkoa unaamua unavyotaka tu mwingine analeta mwezi wa sita, mwingine mwezi wa nne na mwingine mwezi wa nane, jambo hili halina uratibu. Tunaomba Ofisi ya Waziri Mkuu iratibu jambo hili na ioanishe ratiba kwa kila mkoa, ioanishe na ratiba ya Bunge ili na Wabunge tuweze kushiriki kule tuweze kutoa mawazo yetu, hii ni pamoja na vikao vya Halmashauri za Wilaya ikiwa ni pamoja na *Full Councils* pamoja na Kamati zile za Fedha na Mipango, kuwe na uratibu na ratiba ipangwe vizuri. Ndiyo maana tuna Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inashughulika na uratibu wa shughuli zote. Tunaomba jambo hili kwa kweli liweze kufanyika litatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda umekwisha naunga sana mkono taarifa hizi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi nami nichangie hoja mbili zilizo mbili zilizo mbele yetu. Kama ilivyo ada napenda kwa niaba ya jimbo langu la Busanda na wananchi wa Geita kwa ujumla kutoa pole kwa familia ya Mbunge mwenzetu ambaye alituacha hivi karibuni pamoja na wenzake katika tatizo walilolipata la ajali ya ndege. Napenda niseme pole sana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe nafasi kumpongeza dada yetu Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kwa nafasi aliyoipata. Hiyo imedhihirisha wazi kwamba akinamama wanaweza na uwezo wao kwa kweli ni mkubwa sana. Nadhani wananchi wangu hasa akinamama waliopo kwenye jimbo langu wakati anateuliwa tulikuwa kwenye mkutano nikawaambia ikabidi waweke bidii, inawezekana. Niwapongeze pia ndugu zetu nikimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumwonyesha Mheshimiwa Rais akawaona hawa na akawapa nafasi Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Batilda Burian na Mheshimiwa Berbard Membe. *(Makofi)*

Napenda pia niwapongeze na kuwashukuru Wenyeviti waliotoa taarifa zao. Kwa kweli zilikuwa nzuri na kuwa zinasisimua. Nami niungane na Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Omar Kwaangw', kwa kweli limekuwa ni tatizo kubwa, Taarifa za Kamati hazitolewi, sasa nafasi hii inaonyesha umuhimu wa taarifa hizi na wakati huu nadhani wataalamu wetu ni vizuri wawe makini kuangalia kwamba yanayoongelewa yanaelekeza bajeti iende namna gani. *(Makofi)*

Mimi ningeshauri kama ingewezekana kipindi cha wiki mbili za mwezi huu wa kwanza na wa pili ni vizuri kama tungezitumia kwa taarifa tu na watalaam wakawa wanakuja kila taarifa inapotolewa waweze kujikosoa. Bila ya kuelezana hatuwezi kufika na hakuna sababu ya kuwa na Kamati kama haziwezi kutolewa taarifa watu wakazifanyia kazi. Sasa hivi tunawatia suruba Waheshimiwa Mawaziri hata hoja nyingine kufikiri yote yaliyosemwa hapa nadhani labda niwapongeze tu Mawaziri wana vichwa vikali lakini huenda mengine wanayaacha. Taarifa za Kamati ni muhimu naomba Mheshimiwa Naibu Spika na uongozi wetu, Kamati ya Uongozi wajitahidi kuhakikisha kwamba hili suala la kupokea Taarifa za Kamati linafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati napitia makabrasha na wakati nasikiliza taarifa ya *PAC* nimefarijika sana kuona kwamba wamegusa karibu maeneo mengi. Mimi natoka maeneo ya migodi, maeneo ya madini. Nimefurahi kusikia kwamba wanataja sheria ile ya madini ina matatizo. Tumeomba ni muda mrefu na iliwahi kuundwa Tume mwaka 2003 mpaka 2004 kuhusu suala la madini. Hii sheria ina vipengele ambavyo vinamgandamiza mwananchi na sijui ni kwa nini Serikali inaona kigugumizi kuileta ikatengenezwa upya. Sheria inamfanya mwananchi ambaye anakaa mahali panapochimba madini kama ni wachimbaji wakubwa aonekane yeye si chochote na si lolote inasema ni kwa *co-existences* lakini bado inampa nafasi mwekezaji au mchimbaji au mtafuta madini kuwa na kauli juu ya ardhi. Nitatoa mfano Rwamgasi wa Geita kuna wawekezaji ambao wako kule wanafanya ugunduzi lakini wanaweka masharti kwamba mwananchi asiweke vitu vya kudumu au vya maendeleo. Sasa wako pale kwa shida hata kama anachimba choo yuko kule ndani anachukuliwa hatua. Mtu kama anafanya uchunguzi kwa nini wachimbaji wadogo wasifanye shughuli wao wenyewe wakawa wanaendelea wakawa wanachimba badala yake akianza kazi basi wakamwachia. Kamati imebaini kwamba kunatakiwa kuwekwe miundombinu sehemu za migodi.

Ndugu zangu Botswana wanapataje wao gawio la asilimia 50. Wao kwanza Serikali inaweka miundombinu, inaweka umeme, inaweka barabara, inaweka maji. Sasa mwekezaji anapokuja ndipo Serikali inamwambia sasa sisi tumeshakuwekea vitu hivyo. Lakini bahati mbaya sisi sehemu ambako kuna migodi ndiyo sehemu ambazo zina matatizo zaidi. Kamati imebaini kwamba mahusiano sio mazuri kwenye maeneo yenye machimbo ya madini, ni kweli, hali ni mbaya sana. Ni matatizo sana wananchi hawaelewi kwa sababu hawapo. Kwanza wamechukua ardhi sehemu kubwa, wanachukua eneo kubwa karibu nusu ya Wilaya au Tarafa mbili, tatu. Sasa wanakuwa na uwezo wa kuamua lolote pale na bahati mbaya wawekezaji sheria inawaruhusu kutoa kauli yoyote au kutoa maamuzi juu ya ardhi. Sasa mimi napenda niiulize Serikali je, kama wakisema sisi tuna fedha, tunataka wananchi hawa wahame, Serikali itasemaje juu ya hili. Kwa sababu sheria kama imewekwa ilivyo ina maana *Geita Gold Mine (GGM)* wanaanza kutoa fidia kwa Wilaya ya Geita wananchi wa Geita tukakimbia tunakokwenda. Je, *GGM* akiamua kutoa fidia kwa wananchi wa Tanzania tutakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inabidi kuangalia sana sheria hii. Mimi nilikuwa naomba sheria hii ije, inawapa kiburi. Halafu lingine ambalo naona katika makusanyo. Kamati imegundua kwamba Serikali haina uwezo wa kutunza nyaraka lakini vile vile haina uwezo wa kufuatilia. Mimi nilikuwa kule Tume ya Madini, *capacity* ya kufuatilia ni ahadi gani imetolewa na hawa wawekezaji. Kwa mfano mazingira tukuchukue mfano Geita, Kamati naiomba itembelee Mgodi wa Geita iangalie kuna chochote au kuna mti umepandwa pale. Lakini kwenye sheria inatakiwa watunze mazingira waweke katika hali nzuri na waweke fedha kwa ajili ya baadaye watakapoondoka. Ni kweli kwa mfano kesho wakiondoka watakaobaki wanaumia ni wananchi wa Geita. Hata wanavyoviahidi havitekelezeki. Halmashauri wameahidi migodi yote inachelewa wamekubali kutoa dola laki mbili kwenye kila Halmashauri. Migodi yote angalau imetoa lakini mgodi wa Geita haujatoa. Bajeti iliyopita niliuliza hapa Waziri akasema watatoa mpaka leo hawajatoa. Jamani hiki kiburi wanakitoa wapi, hawajatoa. Waziri anazungumza ambaye amechaguliwa na Rais wanamdhalilisha Rais na Waziri, akasema kiburi chao kitawatoka. Tukakutana nao *Dodoma Hotel* wakaniambia bwana wewe umetuaibisha sisi tuko kwenye mpango wa kutoa mpaka leo hawajatoa hizo fedha. Mimi naomba Waziri atusaidie hawa watu kiburi ni cha nini kuna nini ndani. *(Makofi)*

Kwenye Halmashauri tulikuwa tukivutana nao kuweza kuchangia angalau maendeleo. Wakaahidi kutoa dola milioni 150, mara ya kwanza, mara ya pili wakaacha. Tukawaambia wajenge Sekondari, wamejenga Sekondari ni miaka minne sasa ya milioni 150 hayajaisha madarasa manne mpaka leo, shule za wakulima zinakwenda lakini ile shule ndiyo ina matatizo. Sasa nasema hebu sheria hii iletwe tuiangalie tuweze kuangalia wananchi wanafaidika vipi. Sasa hivi kuna mgogoro hivi ninavyozungumza Ruwamgasa hawaongei *East Africa AGO* hawaongei na wananchi wakikutana wanafukuzana na bahati mbaya kulitokea *incidents* wakati wananchi wanachimba walikwenda *East Africa* wakafukia wananchi wawili baadaye walipotoka wakaenda wakawekwa ndani nashukuru Serikali ilienda ikawatoa. Lakini hayo sio mahusiano. Tulilalamika sana katika kipindi kilichopita bahati mbaya kiongozi alisimama akasema msiwasumbue. Nadhani nimshukuru sana Rais wetu sasa hivi alivyoingia akasema mimi nilikuwa nimeamua kunyamaza sasa hivi nazungumza kwa sababu ya nguvu aliyoingia nayo Rais akatuunga mkono katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imegusa vile vile baadhi ya Wizara. Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia amezungumzia suala la *division one.* Nashukuru kwamba linafanyiwa kazi kwa watu na suala la mikopo. Lakini napenda nitoe tu angalizo moja kwamba bado kuna tatizo kwenye suala la mikopo hasa kwenye *mini testing* kugundua ni nani anayestahili kulipiwa. Kwa sababu kama mtalipia *division one* unaweza ukajikuta wale waliosoma *Saint Augustine, Saint Joseph* au nini ndio unaowalipia. Lakini waliosoma shule za *Saint Government* na *Saint Kata* hizi tunazozijenga hawamo. Basi inahitaji kuangalia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hapa ni uaminifu wa vijana na sisi wenyewe wazazi sijui lakini nadhani hata watoto wa Wabunge wanalipiwa. Kwa hiyo, inabidi tuangalie tunapoweka kidole hivi tujiweke na sisi wenyewe. Inabidi waweke sheria kuhakikisha kwamba wanaolengwa ni wale wale. Mimi nadhani mgogoro usingekuwa asilimia 40. Asilimia 40 kama inaweza kupatikana waongezwe wengine na vile vile hata wanaosoma *private* hata wanaosoma nje wanasema wanaosoma nje analipa dola fedha za Kitanzania milioni mbili na huyo anasoma *Saint Augustine* analipa milioni mbili hakuna

tofauti wote kama wakipewa *flatrate* wote wakasaidiwa, tunachotaka ni kwamba watoto wasome lakini pawe na uaminifu huyu kuna nini. Kwa sababu kuna wengine wamefiwa na wazazi wao. Unakuta mama amekufa, baba amekufa lakini sasa inahitaji Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia asaidie. Lakini watu wake wafanye kazi kuanzia huyu mtoto. Wewe *primary* umelipa laki saba, sekondari milioni moja na nusu, leo laki mbili za asilimia 40 unasema ni matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani kuna mahala ambapo tunahitaji kusaidia. Kamati imezunguka, imefanya kazi vizuri lakini nadhani wamelisha pua wamesahau mdomo. Sikusikia wanataja hizi hela za Ofisi za Wabunge. Hatuna Ofisi, je, mmeona huko? Hatuna Ofisi, mimi kwangu ni taabu na naomba mtembee ikiwezekana mfike kwangu muende mpaka Rwamgasa msikie wananchi wanavyoishi na wachimbaji ni taabu tupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuzungumza angalau wananchi wapate taarifa hiyo lakini naomba Taarifa za Kamati zipewe nafasi kwa wakati muafaka ili bajeti ifanane na hali halisi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa mimi nafasi hii ili niweze kuchangia katika siku hii ya leo kwenye hotuba hii ya Kamati ya Bunge ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza sana Kamati hii imefanya kazi nzuri sana, imetembea kwa sababu Halmashauri hizi zipo nchi nzima wamejitahidi wamefika huko na wamekwenda katika maeneo mengi ya vijiji vyetu, wameshuhudia kazi zinazofanywa na Halmashauri zetu. Ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, thamani kubwa ninayoiona katika taarifa ya Kamati zetu hizi ni kwamba taarifa hizi kama zilivyoandikwa vizuri zinatupa nafasi sisi viongozi wa Halmashauri mbalimbali kuweza kujua jinsi Halmashauri nyingine zinavyofanyakazi, ufanisi jinsi ulivyofanyiwa kazi katika Halmashauri na kwa hivyo, inatupa nafasi ya kuweza kujipima uwezo wa Halmashauri moja na Halmashauri nyingine. Bila kuwepo kwa taarifa hizi si rahisi Waheshimiwa Wabunge tukafahamu Halmashauri nyingine zinafanya kazi namna gani. Kwa hiyo, nashukuru sana taarifa hizi zinatusaidia kujipima kati ya Halmashauri moja na Halmashauri nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Halmashauri yangu ya Wilaya ya Muheza. Imefanya kazi nzuri sana na kwa taarifa za mahesabu Halmashauri yangu ya Wilaya ya Muheza kwa mwaka wa pili mfululizo imekuwa inapata hati safi na ninaamini kabisa hata mwaka huu vile vile tutapata hati safi kuweza kuadhimisha mwaka wa tatu mfululizo na ninaomba viongozi wa Halmashauri, watendaji na Baraza la Madiwani tuendelee kushikamana na kushirikiana ili katika miaka mingine yote inayofuatia Halmashauri ya Wilaya ya Muheza iendelee kupata hati safi. Matunda ya kupata hati safi tumeyaona tumepata *Capital Development Grant* kwa miaka yote miwili na fedha hizi si kidogo si haba. Ni zaidi ya milioni 400 na tumezigawa fedha hizi katika Kata zetu kufuatana na idadi ya watu katika Kata na zimefanya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana kwamba zimetusaidia vilevile katika ujenzi wa shule za sekondari mpya ambazo zinaendelea kujengwa hivi sasa na zimetusaidia katika miradi ya maji na nina uhakika kwa wale ambao kwa bahati mbaya walikosa basi watajitahidi waweke vitabu vyao vizuri waweze kupata kwa miaka inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niseme mengine machache. Kwanza kwa kupata hati safi, Wilaya ya Muheza tumethibitisha tunao uwezo wa kusimamia fedha za Serikali, Taasisi mbalimbali na mapato ya Halmashauri yenyewe ya Wilaya ya Muheza vizuri. Ninachotaka kumwomba Mheshimiwa Waziri sasa atufikirie kwa haraka inavyowezekana kutupatia Halmashauri ya Mji Mdogo wa Muheza uwezo wa kusimamia fedha tunaomba Halmashauri hiyo ya Mji mdogo. Msitucheleweshe tukafika mahali tukata tamaa. Ni matumaini yangu kwamba Wilaya ya Mkinga pia, Wilaya mpya inayotokana na iliyokuwa Wilaya ya Muheza na yenyewe watapata nafasi ya kupewa Halmashauri yao ya Wilaya mpya ya Mkinga, shabaha ni kusogeza huduma zaidi sio kuongeza tu idadi ya Halmashauri tunaongeza Halmashauri kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi lakini vile vile tunasogeza kwa wale ambao tuna uhakika wana uwezo wa kutunza na kusimamia fedha hizo vizuri kama ambavyo Wilaya ya Muheza tumeonyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shabaha kubwa zaidi vilevile ni kuendelea kuziimarisha Halmashauri zetu. Pale tunapoona dosari basi tunazizungumzia dosari. Dosari moja imeshazungumzwa na wenzangu lakini ningeomba niisisitizie tu. Mara kadhaa vikao vingi vinafanyika kule katika Halmashauri zetu wakati vikao vya Bunge vinaendelea. Hii inadhihirisha kwamba ratiba ya vikao vya Bunge katika Halmashauri zetu aidha, haitambuliki au haiheshimiki.

Sisi kama ni Madiwani, tunayo haki ya kuhudhiria katika vikao vile. Tuna nafasi ya kuzishauri Halmashauri zetu vizuri lakini mara kadhaa hata *Full Council* zinakaa. Tunakuta maamuzi mengine yamekwishafanywa lakini tunasema mchango wetu katika baadhi ya mambo umekosekana. Kuna matatizo makubwa katika viwango vya ushuru katika soko kwa mfano la Muheza. Viwango vya ushuru ni vikubwa lakini ukipiga mahesabu utaona kwa mfano anayeuza nyanya anaambiwa alipe shilingi 200 kwa siku. Watu wanasau shilingi 200/= kwa siku kwa mwezi ni shilingi 6,000/= kwa muuza nyanya. Lakini wanasahau kwamba muuza nyanya huyo kwa mwaka atalipa shilingi shilingi 72,000/-=. *(Makofi)*

Lakini hebu tutizame kodi yetu ya mapato inasema nini? Ambayo ndiyo kodi kuu inayoainisha mapato ya mwananchi. Kodi ya mapato kiwango cha chini ni shilingi 35,000 mfanyabiashara analipa, muuza nyanya alipe shilingi 72,000 kwa mwaka. Lakini tatizo linakuja hapa ushauri wakati wa kuandaa sheria ile haukuwa kamilifu, hawakutizama vigezo hivi walikuwa wanatizama 200/= wakidhani 200/- ni hela ndogo sana. Ukiitazama kwa mwaka mzima ni shilingi 72,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba kwa kuwa Mheshimiwa Waziri yupo hapa vikao hivi vifanyike wakati Waheshimiwa Wabunge wapo na kila mara tumekuwa tukitoa malalamiko yetu hapa Bungeni na Mheshimiwa Waziri amekuwa akisisitiza kwamba Halmashauri waheshimu vikao hivyo vya Bunge, lakini naomba kukuhakikishia kwamba hili halifanyiki. Wabunge wengi ndiyo maana wanaonyesha

ishira kwamba halifanyiki na ukiwauliza Wakurugenzi, mimi nimemuuliza Mkurugenzi wangu kwa nini anasema tunasikia tu huko kwamba tuainishe mikutano ya Wabunge na hii lakini hatuna *circular*. Sisi hatufanyi kazi kwa kusikia watu wamezungumza Bungeni, tunafanya kazi kwa kuletewa *circular* inayotoka kwa msimamizi wetu ambayo ni Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Sasa kwa kweli naomba kama Wizara haijui hivyo ndivyo wanavyosema Wakurugenzi basi leo ninawaambia, kama kweli mnataka kuanisha vikao hivyo na vya Bunge viende ili Wabunge waweze kushiriki, nawaombeni basi hiyo inayoitwa *circular* pelekeni na sisi mtupe nakala tatizo liishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taarifa hii wamezungumzia mambo mengi. Mimi ningeomba nishauri jambo moja ambalo naomba Kamati ilisisitizie na viongozi walisikie vizuri. Kuna fedha hizi zinazoitwa fedha za *Basket Fund*. Hizi fedha za *Basket Fund* ni fedha ambazo kwa kweli zinakuwa ni mali ya watu wachache sana. *DMO* na sijui hospitali inayohusika na watu wengine. Lakini ukienda hata ndani ya Baraza la Madiwani hawajui ni kiasi gani cha fedha zimekuja ndani ya *Basket Fund.* Hawajui hata *composition* ya *basket fund* yenyewe. Zipo fedha nyingi sana zinakuja kwa njia ya mbalimbali kwenye *basket fund*. Zinatumiwaje fedha hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba muwaambie Wizara ya Afya watupe nakala ya fedha zinazopelekwa kwenye *Basket fund*. Siku zote Waheshimiwa Wabunge tunaambiwa nyinyi ni Madiwani mnapaswa kusimamia. Taarifa za fedha zikipelekwa kule sisi hatupati taarifa. Si rahisi kutegemea taarifa zote za fedha utapewa na Halmashauri ambayo sisi hatuhudhurii. Kwa hiyo naomba nisisitize hapa fedha hizi za *Basket Fund*. Tupewe taarifa Waheshimiwa Wabunge kila mara fedha hizo zinapopelekwa na kwa hivyo, ndugu zangu Waheshimiwa wa Kamati hii ya Serikali za Mitaa naomba pia mnapotembelea, mnapofanya ukaguzi basi muweke uzito mkubwa katika eneo hili la fedha hizi za *Basket Fund* kwa sababu kama kuna fedha ambazo hazina mpangilio wa matumizi mazuri ni fedha hizi za *Basket Fund*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuzungumzia eneo lingine moja muhimu. Serikali katika upande huu wa madini nilimtafuta Mkaguzi, anayeitwa Alex Stuart na nimesikia wenzangu wanamfahamu. *Auditor* amefanya kazi nzuri sana, amekuwa akitoa taarifa nyingi sana. Sasa watu wengi wanaweza wakasema kwa nini ninazungumzia habari ya madini wakati Muheza hakuna madini. Muheza tuna dhahabu na bila shaka *Inshallah* Mwenyezi Mungu atajalia tutapata mgodi mkubwa wa dhahabu kule. *(Makofi)*

Kwa hiyo, haya ninayosema, nasema ili yasije yakatokea pia Muheza. Ripoti ya Alex Stuart imetoka, inaonyesha mambo mengi, udhaifu mkubwa. Kwanza, baadhi ya makampuni haya ya migodi hayatoi ushirikiano mzuri kwa huyu Mkaguzi, pili, hata kumbukumbu za mapato na matumizi na *documentation* hazipatikani. Katika taarifa zake baadhi ya taarifa zake zinaonyesha katika baadhi ya migodi, kumbukumbu, *documents* zaidi ya 6,000 zimetafutwa hazionekani. Vile vile sheria inasema kama mwenzangu alivyotangulia kusema kwamba *documents* zote lazima ziwepo hapa. *Financial reports* zote na *document* zote ambazo zinahusiana na matumizi ya fedha zinapaswa kuwepo hapa. Mara nyingi hili halitendeki. Sasa Sheria tuliyotunga inaonekana kana kwamba ina mapungufu. Lakini inawezekana kwa sababu tunatunga Sheria halafu baada ya Sheria

Waziri anakwenda kutunga taratibu na kanuni, je, hizo kanuni kweli baada ya sheria ile kutungwa kanuni zimetungwa za kuhakikisha kwamba hawa wana-*comply* na taratibu na kanuni zilizopo ndani ya sheria kuu? Inaonekana bado kuna matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu *Auditor* vilevile ametengeneza utaratibu maalam wa kuwezesha wataalam wetu wenyewe waweze kufahamu utaratibu wa kufuatilia uchimbaji wa dhahabu, uyeyushaji, upimaji, usafirishaji na mauzo, mpango maalum kabisa. *A program,* sasa wametoa mapendekezo kwamba Watanzania wafundishwe namna ya kusimamia hiyo *program* tangu pendekezo hilo la kutaka watu washirikishwe, waelimishwe, wafundishwe katika kui-*manage program* hiyo. Limepelekwa Serikalini bado halijafanyiwa kazi. Naiomba Kamati iikumbushe Serikali. Wakati tunalia na mpango wa madini pamoja na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa yote aliyoyafanya juhudi zote anazofanya na nina uhakika atakuwa ameisoma *report* ya Alex Stuart basi tujitahidi kama Serikali tuwaandae watu watakaoweza kusimamia *program* hii iliyoandaliwa kwa ajili ya kuinufaisha nchi yetu. Naomba Wizara inayohisika ifuatilie *Auditors report* hiyo na mapendekezo ya *program* hiyo ili itekelezwe, tuwe na Watanzania watakaoweza kusimamia uchimbaji, waweze kusimamia uyeyushaji, waweze kusimamia upimaji, usafirishaji na uuzaji wa dhahabu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi naungana na wenzangu kuwapa pole familia ya kaka yangu Marehemu Juma Jamaldin Akukweti, Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Pili naomba niwapongeze dada yangu Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro kwa kweli imedhihirisha wanawake tuna uwezo, naomba nimpongeza mdogo wangu Mheshimiwa Dr. Batilda Buriani, nakuombea kwa Mwenyezi Mungu akusaidie ufanikiwe katika shughuli zako. Namwomba kaka yangu Mheshimiwa Bernard Membe na yeye nampongeza, pia nawapongeza Manaibu Waziri ndugu yangu Mheshimiwa William Ngeleja mtani wangu na kaka yangu Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mwenyezi Mungu atawasaidia. *(Makofi)*

Pia naomba nilipongeze Bunge safari hii. Bunge kwa kawaida tunatakiwa tusimamie na kuishauri Serikali, lakini kwa utaratibu tuliokuwanao tunaisimamia na kuiamuru Serikali. Kwa nini nasema hivyo? Utaratibu wa kuwa na Kamati za Bunge na kuwaambia njooni Serikali, mmefanya hivi na hivi, fanyeni hivi hivi nafikiri ni utaratibu mzuri. Zamani kulikuwa hakuna Kamati ya *LAAC*. *PAC* ndiyo ilikuwa inasimamia masuala yote ya Halmashauri kupitia Wizara. Huwezi kuamini mimi nimekuwa Mbunge wa muda mrefu, mahesabu yalikuwa hayafungwi, ukienda Wizarani utakuta magunia ya mchele, mahindi, zawadi mbalimbali wanapelekewa wakubwa na walikuwa hawafungi. Lakini baada ya *LAAC* kuingia, naomba nilipongeze Bunge imeisimamia na kuiamuru, sasa hivi Halmashauri zinafunga mahesabu, ukiacha hizo Halmashauri nne kama nimesikia ndio kidogo bado ziko nyuma. Mimi nawapongeza Halmashauri na Wizara na Serikali kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si nia yangu kusema mazuri kwa sababu mazuri ya Halmashauri yameshasemwa, nia yetu kusema upungufu ili Serikali ichukue na

iyaboreshe vizuri. Kwa hiyo, nisionekane kama sijafurahishwa wala sija-*appreciate,* hapana. Nataka nitoe ushauri tu. Kwanza kabisa naomba nikushukuru wewe kunishawishi mimi kugombea Ubunge wa Jimbo, nilipokuwa Mbunge Viti Maalum sikuyaona sasa nayaona ndio nayazungumza kwa uhakika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mimi nakushukuru ulikubali. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Nakushukuru sana dada yangu, lakini nimeona Wabunge wa Jimbo walivyokuwa na kazi, naomba Bunge, Serikali itusaidie, ukisimamia ukweli unaandaliwa mikakati ya kuondolewa Ubunge. Sasa mimi naomba Serikali tusaidieni ili tuwasaidie, ama sivyo tutaogopa na ku-*compromise* ili tuendelee kukaa katika Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu wa Spika, naipongeza Halmashauri yangu ya Kibaha ina hati safi na katika Halmashauri za Mkoa wa Pwani, Halmashauri ya Kibaha Mjini kwa kweli mara nyingi napongezwa. Naomba niipongeze kwa dhati kabisa. Lakini kama alivyosema Mwenyekiti wa *LAAC,* hati safi haimaanishi na wao wako *clean*. Hati safi inaonyesha mambo yao kama ni mazuri kama ni mabovu utayaona katika ile hati. Kwa hiyo, sio wakati wote kwenye hati safi tushehereke. Sasa mimi naomba nioneshe udhaifu ili baadaye tusaidiane na tumsaidie kaka yetu, Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete, mwenye nia nzuri na mwenye kukerwa kuhakikisha anamtoa Mtanzania kutoka hapa kwenda pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu sheria ya *tender,* sheria ya *tender* itizamwe upya ina udhaifu. Rais alipokuwa kwenye *ALAT,* Waziri Mkuu alipokuwa anazungumza na watendaji katika *speech* yake, alisema: *"Weakness* ya watendaji wetu hasa masuala ya uaminifu kwenye pesa." Ninazo hizo *speech,* hata nikiambiwa nizi-*table* nitazi-*table.* Lakini watendaji hawa ndio wamepewa *mandate* ya kusimamia. *Tender Board* inafanya kazi yake bila ya kuishauri Halmashauri ikimaliza pale ina *award* hiyo *tender*. *Tenderer* akishindwa wana-*award* na nyongeza bila Halmashauri. Sijui wenzangu mie Halmashauri yangu ndio inavyofanya. Ukiuliza wanasema huyu Dr. Gama, mkorofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe na utaratibu, unamnyanyasa sana Mwenyekiti wa Halmashauri kitu yeye mwenyewe hakuwa katika kikao na Waziri sizungumzi wewe, unajua kwa sababu nilishakufuata kwenye suala la gari la zima moto, ingawa wamekudanganya mambo mengi. Milioni 300 iliyochukuliwa akawa mtu amekuwa *awarded* ikichukuliwa siri siri bila kibali cha Halmashauri ikapelekwa benki ya *CRDB,* ukiuliza wanasema Mheshimiwa Waziri unajua tulikuwa tunataka *LC* kwa hiyo, tupeleke pale. Sisi tulishamweka *tenderer, LC* inatuhusu nini? *Tenderer* ndio atajua. Sasa baada ya kuwa wakali kidogo nikuchekesheni tumeletewa watu wa *tender* wamesema sisi hatu-*award,* ile nyongeza wametuletea wanasema basi mpeni huyu miezi sita, nikawauliza sheria imebadilika tena? Lakini nataka kusema, kwenye suala la *tender,* naomba litizameni sana ndio rushwa kubwa inaenda kule. Kwa mwaka wangu mmoja niliokaa ndani ya Halmashauri nimeona, huko ndio hela zinaliwa. Naomba kama ikiwezekana basi Mwenyekiti kabla hajasaini aambiwe kwa nini ali-*award* kwa huyu na wakamwacha huyu na ikiwezekana Kamati ya Fedha iambiwe, basi sisi tumeona hivi ni muhimu na siye hivi ndiyo tutakavyowasimamia. Lakini kama hujui chochote hilo nilikuwa nataka tulitizame, sheria ya *tender.*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado na sheria ya hii Kamati ya ajira, ndio Diwani yupo lakini wanakaa kisha wanachambua kisha wanatoka pale watendaji wanaamua ku-*award* watu wanaowajua, mwisho wa siku unajikuta wanaingia watu ambao hata hawana uzoefu, unamkuta hata Mkuu wa Mkoa analalamika. Kwa hiyo, mimi naomba hiyo *board* ya ajira tuitizame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Ardhi, Idara ya Ardhi bado haijajirekebisha sijui wenzangu! Bado. Naomba muitafutie sheria kali, viwanja vinatolewa wanavyojua wenyewe, wana-*award* wanavyojua wenyewe, ukiandika maswali, mimi napeleka maswali kwenye Halmashauri yangu hawakujibu, hawakujibu. Wanakuambia kwa bahati mbaya tulisahau, niambieni viwanja vingapi mme-*award* kwa nani na kwa *qualification* gani? Sasa hawa muwaangalie watu wa ardhi kuhusu fidia, naomba sheria ionyeshe uwazi, hizi fidia watu wanalipwaje, kama ni mnazi analipwa kiasi gani, kama ni mkorosho analipwa kiasi gani, wananchi wanalalamika.

Lingine nilikuwa naomba ushauri, Madiwani wetu tuwasaidie kufahamu sheria mbalimbali *circular* mbalimbali zinazotolewa ili waweze kumsimamia huyo Mkurugenzi, mara nyingi hawafahamu. Kwa mfano, haiwezekani Mkurugenzi anayejua sheria anawaambia Madiwani tuwatoze watu kodi bila ya kuwa na sheria ndogo na Madiwani kwa sababu kuwa hawajui wanakubali na watu wanatozwa. Mbunge ukisimamia wanasema Mbunge anasimamia kwa sababu hataki kukusanya mapato. Wanakuwekea kikao na posho wanaweka, ajadiliwe Mbunge. Sasa bahati nzuri mimi nasoma sana, kwa hiyo, ilipofikia *stage* hiyo nilipowatwanga, wakajua kumbe huyu Mbunge wetu anajua na wakapeleka na sheria ndogo ziko kwako angalau zimechelewa najua zitapita, ili tuwatoze watu kwa utaratibu wa sheria. *(Makofi)*

Lakini lingine kwa mfano unachukua hii mifuko mbalimbali ya Serikali, Madiwani wanatakiwa waelimishwe, mnatupa taabu wengine, kwa mfano *TASAF* inasema mradi huu utashughulikiwa, lakini inatakiwa atafutwe fundi kupitia *TASAF,* lakini Halmashauri wanasema tutaweka mkandarasi na mkandarasi atakuja kuwajibika kwetu na pesa ile itakaa kwetu. Mbunge ukiwa mkali wanasema huyu Mbunge lazima tumwondoe. Sasa mimi naomba tusaidiane, mnatupa kazi wengine si tumeaambiwa tuko *vocal,* tutakosa ubunge na tunautaka na ku-*compromise* hatuwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unisaidie, nilikuwa naomba Kamati sasa iwe na utaratibu wa kutizama ile miradi, najua muda ni mchache, lakini kweli fateni mkatizame miradi, *value for money,* hasa miradi ya barabara inatisha na ninaomba kama inawezekana Waziri atupe *list* kutoka bodi ya makandarasi, *list* yote ya makandarasi wote, ma-*engineer* sijui wa maji, wa barabara, kusudi tunapo *award,* tujue huyu kweli amepitishwa. Lakini makandarasi wengine wa barabarani tu mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu wa Spika, naomba nizungumze suala la bajeti, naomba tupeni utaratibu ni wakati gani Halmashauri, Wilaya inakaa inazungumza bajeti ili kwa utaratibu ifike ngazi ya Taifa. Nimeona tangu nikiwa Diwani vipindi hivyo mpaka nimekuwa Mbunge, ikifika wakati wa bajeti, mnaletewa haraka haraka Serikali imesema tupitishe hata vikao vingine mnaambiwa tuvisitishe. Sasa hilo mimi na wasiwasi, naomba mtupe taratibu lini tuzungumze na wakati unapofikia *ceiling* nani anaruhusiwa kuufuta mradi huu kwa sababu tumekuta hata miradi ambayo tunaona ni muhimu imefutwa. Wanasema huko Hazina wamesema tufute, sasa mimi nilikuwa nataka hiyo ifuatiliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumza bila kuzungumza mambo ya rushwa utanishangaa. Hela zile ambazo zimepangiwa kwenye bajeti kuwa *allocated* katika Halmashauri za masuala ya kupambana na rushwa kuwawezesha, kuwaelimisha watu mbona hamjazileta? Naomba tuleteeni tuzifanyie kazi.

Lakini lingine nataka mtusaidie, kawaida katika Kamati ya Fedha, kwa taarifa ambayo nimepewa inawezekana ni ya barabarani kwamba lazima *internal auditor* atoe ripoti yake. Mbona Halmashauri hatuna ripoti za *Internal Auditors,* wengine wanasema kila mwezi, wengine wanasema kila miezi mitatu. Tuambieni utaratibu na Madiwani wafahamu ili tupate ripoti ya *internal auditor* kusudi akitudanganya ikifika wakati *external auditor* akiona kuna mambo tunamuuliza. Lakini lingine *qualification* ya Mweka Hazina anatakiwa mwenye *CPA* au yupi? Kusudi tusije tukakosa zile pesa za *Local Government, Capital Development Grand* na kama wako Halmashauri ambazo hawana Mweka Hazina *qualified* naomba Wizara ifanye utaratibu ituletee. *(Makofi)*

Lakini kuna suala lingine sasa hivi nashukuru Serikali inatoa pesa kupeleka mpaka kwenye Kata. Lakini Madiwani hawajaelimishwa matumizi ya pesa zile, watendaji sasa wanachukua. Mimi nina Mtendaji mmoja mlevi kabisa alipopata aliifanyia kazi. Alipouliza Diwani wake akasema hii anaijua Mtendaji. Sasa mimi naomba tusaidiwe, je, inapofikia wakati Halmashauri inatumia pesa bila ya kibali Waziri unasemaje? Kwa sababu sasa tume-*experience* kuna pesa za maendeleo zinachukuliwa, zinaanza kununuliwa mafuta tu kwa wingi, unatakuta idara moja ina lita 1,000 kwa mwezi, idara nyingine lita 5,000, ukiuliza anasema sijui Mkuu wa Mkoa kataka, sijui Mkuu wa Wilaya. Jamani hao Wakuu wa Mikoa na Wilaya na sherehe hizo hamzipangii hela mpaka wachukue hela za maendeleo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi jamani hela mnazotuletea hizi za maendeleo zinatusaidia sisi Wabunge na Madiwani, kwa sababu *TASAF* inajenga sekondari, *TASAF* inajenga hiki, sijui ikifanyika mimi ninajivuna kama Mbunge au Diwani anajivuna mnaona maendeleo na Chama changu kina jivuna pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naomba tusaidiwe kwenye hili. Lakini naomba nishauri lingine kwamba inapofika … Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana! *(Makofi)*

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kumalizima muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru! Lakini huku-*declare interest* kama wewe ndiye Mwenyekiti wa Chama cha Kupambana na Rushwa Bungeni. *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hotuba nzuri za Wenyeviti wetu wa Kamati za *LAAC* na *PAC* walizozitoa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Wabunge wenzangu kwa kutoa pole za dhati kabisa kwa wenzetu waliopatwa na ajali ya ndege kule Mbeya akiwemo Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Juma Akukweti. Mwenyezi Mungu azilale roho za marehemu wote mahala pema peponi, amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niwapongeze wote ambao wamebahatika kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kumsaidia katika shughuli mbalimbali za Serikali, nikimtambua Mheshimiwa Bernard Membe ambaye kwa kweli amewekwa mahala pake. Nina imani kabisa hatamwangusha Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, ni mwanamama ambaye kwa kweli alikuwa anajitahidi shughuli zake. Nadhani vile vile hawajakosea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndugu yangu Mheshimiwa William Ngeleja, mimi ninamfahamu vizuri nadhani hapo yuko sahihi na nadhani shughuli yake itaenda vizuri tu. Mheshimiwa Gaudence Kayombo, yeye ni *Banker,* sasa amepelekwa kwenyewe. Awawezeshe wananchi ili angalau waweze kufanya kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Mhreshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa namna ya pekee, kwa kweli Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, wamemtendea haki kumpa cheo hicho cha kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, yuko sahihi kabisa na Watanzania tutafaidi mengi. Tuumuunge mkono na Mwenyezi Mungu amjalie katika kazi hiyo ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitakuwa na machache lakini nitagusa gusa katika maeneo mengi hususan katika Wilaya yetu ya Misungwi. Kwanza nipongeze Kamati zote mbili katika taarifa zao. Mimi nimekuwa hapa katika Bunge hili letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, lakini sikuona kitendo kama hiki ambacho kwa leo kinaonekana ni cha ajabu. Ni haki yetu lakini ilikuwa imejificha mahali. Kwa *style* hii Kamati zote zizungukie maeneo zinakofika, zilete taarifa hapa tuweze kuijadili kama jinsi ambavyo tumeishaanza sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilibahatika, Kamati ya *LAAC* ilipofika Misungwi na mimi nilikuwepo niliungana nao. Hawakuwa wengi wa kutisha, walikuwa ni watatu tu. Namkumbuka sana Mwenyekiti wa Kamati hiyo *Engineer* Laus Mhina na Mheshimiwa Gosbert Blandes na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakari, kazi waliyoifanya ilikuwa ni ya kutikisa. Walikuwa ni ma-*auditor* ambao kwa kweli kazi ndio inatakiwa namna hiyo, kuihoji Serikali kuangalia imefanya nini.

Sehemu walizopangiwa, zingine walibadilisha wenyewe. Badala ya kwenda mahala fulani, sasa tunaenda mahala fulani kuvamia. Waliyoyaona ni ya ajabu kabisa. Nadhani tabia ya kuvamia bila kupangiwa iendelee. Mkifika mahala kwenye Wilaya, ombeni kwamba badala ya kwenda mahala fulani, tunaenda mahala fulani maana pesa kule zimeshapelekwa. Mtajionea mengi na mtakuwa mmetusaidia Wabunge katika maeneo, maana yake unapozungumzia Jimbo lako inaonekana kama unavuta kitu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti amezungumza kuhusu hati chafu. Imetugusa wananchi wa Misungwi hiyo hati chafu wote hata wale tusiohusika na masuala ya mahesabu. Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, alipokuwa akichangia, alielezea matatizo ya watendaji walio wabovu kuna Mtendaji, Mweka Hazina aliharibu kule Ukerewe, akafungiwa na pesa za barabara karibu shilingi milioni 200 hivi, baadae akahamishwa yule Mtendaji mbovu kuja kwenye Wilaya ya Misungwi. Yale yale yameendelea mpaka leo hii nazungumza hapa, wananchi wa Misungwi wamezuiliwa

pesa zinakaribia kwenye shilingi milioni 160 za Mfuko wa Barabara kutokana na makosa ya yule yule. Waliodhibiwa ni wananchi wa Misungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kuna haki hapo, wananchi wa Misungwi wanaadhibiwa kwa kosa la mtu mliyetuletea ninyi wenyewe ni haki? Mnajua ameharibu mahala fulani, mmemhamishia kwenye Wilaya nyingine ameharibu hivyo hivyo, wanaowajibika sasa hivi kurudisha zile pesa zaidi ya shilingi milioni 29 ni wananchi wa Misungwi. Bado wanahangaika nazo, Ofisa wa Waziri wa Serikali ya Mitaa amefika kule Misungwi na Tume yake, mpaka leo hajatoa ripoti. Tunaendelea tu kusuasua kutafuta pesa, hatujapata zaidi ya shilingi milioni 160. Sasa hivi wananchi kutoka Misungwi kwenda Mondo kupitia Nguge, hawawasiliani tena. Shilingi milioni 160 ziko mahala fulani kutokana na Sheria ya *Road Fund* kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika ningeliomba basi katika majumuisho, Waziri anayehusika na TAMISEMI anieleze anawasaidiaje wananchi wa Misungwi, shilingi milioni 60 kwa mtu wao aliyekuja kuvuruga kwenye eneo hilo? Naona kwa sababu ni ujumbe, hapo utakuwa umeshafika na nitakuwa nasubiri majibu ya kuwaridhisha wananchi wangu wa Misungwi ili angalau na wenyewe waweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado niseme kwamba kwenye *Development Grant,* Misungwi haipati na Halamashauri zingine zaidi kama nne hivi, kuna Halmashauri ya Mji wa Mtwara na kuna Handeni. Nina imani kabisa matatizo haya sio ya kwao ni ya watendaji. Unapowanyima ule msaada wa pesa zile za maendeleo, watafanyaje kazi! Hujawatendea haki wananchi hao. Wapo watumishi walioharibu, unawafahamu, na wapo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni juzi tu, naipongeza Serikali mmeniletea watumishi. Ustawi wa Jamii umeshaleta, Afisa Ushirika umeshaleta pale na *DT* mwingine tayari umeshaleta, lakini ndani ya mwezi mmoja, tayari tena uhamisho mwingine. Yule *DT* anahama tena pale. Hivi alikotoka nani alimlipa kuja Misungwi na hapa anapotoka Misungwi kule anakoenda hajafanya kazi hata mwezi mmoja, anahamishwa tena. Analipwa na nani kama siyo kuharibu hela ya wananchi!

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kimemtoa Misungwi mara hii? Ulipokuwa unamleta, ulimleta kwa madhumuni yapi? Tunazidi kupata matatizo tu. Tulifikiri tumepata Mhasibu ambaye tena ni *qualified,* ambaye sasa angeweza kutusaidia. Ameshahama! *Either* ameona *income* ya pale ni ndogo, sasa hapa hapastahili, ngoja nihamie tena kwenye madini. Keshaenda Geita, tumeachwa sisi tunahangaika. Hatuna Mhasibu aliye imara wa kuweka Mahesabu yetu katika utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itufikirie, ituletee mtumishi ambaye ni imara, tuweze na sisi kufanya kazi kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie katika hotuba ambayo imetolewa na wenzetu, wajumbe ambao walipata nafasi ya kufika kwetu hawa wajumbe wa *LAAC.* Wamezungukia maeneo mengi, lakini wakaja kushangazwa zaidi na hospitali yetu ya Wilaya ya Misungwi. Juhudi zinazofanyika pale, huwezi kuamini kwamba hawa watu wote wanaofanyiwa operesheni hapa na wanatoka salama katika mazingira haya,

unawapongeza zaidi hao waganga walioko Misungwi, wanafanya kwa mazingra magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali haina chumba cha upasuaji cha wagonjwa wa kawaida hivyo hutumia chumba cha upasuaji wa wazazi kama *theatre*. Sasa unajikuta wananchi wanakuwa na matatizo kweli na ni watu wawili tu ambao wanaweza wakafanyiwa operesheni kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali iwaonee huruma sana wananchi wa Misungwi, iwatengee angalau fungu tuweze kujenga angalau chumba cha upasuaji kingine. Tupate wodi nyingine kwa ajili ya shughuli zetu za wazazi katika eneo hilo. Matatizo ni makubwa sana kwenye eneo hilo. Wananchi nawashukuru sana wanajitahidi sana katika michango mbalimbali. Wanachangia masuala ya shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la shule mpaka sasa hivi tunategemea kufungua zaidi ya shule nane. Wako katika utaratibu mzuri tu, wanaendelea vizuri. Niwapongeze ndugu zangu wananchi wa Bulemeji kule wanaendelea vizuri, Kata yangu ya Mwaniko, Kasololo wanaenda vizuri, Sumbugwa wako mbioni, Irujamati wanafanya kazi vizuri, Lubili wako mbioni na wenyewe watafungua. Nina imani kabisa shule zote nilizozitaja Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi nitafika mbele zako kuja kunipa usajili wa shule hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kikubwa, matatizo ni walimu. Sasa hapo Isakamayo yenyewe nina walimu watatu tu sasa hivi na iko *Form two* saa hivi. Kwa hiyo, naomba hilo Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Elimu alifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Madiwani kwa muda mfupi sana. Madiwani wamekuwa wasidizi wetu wa karibu sana. Wanafanya kazi kwa kujituma sana. Posho yao ni kidogo sana, wamepiga kelele wee! Bunge limekuwa likienda utaratibu wa kuwafikiria kwamba na wenyewe angalau wapate posho ya msimamo. Sijapata taarifa kwamba hivi ni shilingi ngapi na ni lini watapewa. Hivi ni lini hasa watapata hawa Madiwani posho yao hii? Itisha watu, tunataka shule za sekondari za Kata, ukifeli hutapewa fomu ya kugombea Udiwani, tumewabana watu hawa, lakini posho yao ni ya ajabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majumuisho, ningependa Serikali itamke waelewe watapata kiasi gani na ni lini kitaanza ili angalau na wenyewe waweze kupata chochote. Baadae Serikali iendelee kuwafikiria Wenyeviti wa Vijiji, uteremke mpaka kwenye Wenyeviti wa Vitongoji, ndio wasimamizi wa shughuli zetu zote. Najua itakuwa kazi moja ngumu sana. Lakini hebu tujaribu kuanza kuwafikiria hawa watu, mikutano yote, michango yote, anaacha shughuli zake, yeye anakuwa yuko katika shughuli hiyo tu. Tuangalie utaratibu mzuri tu ambao tutaona kwamba tunawezaje kuwasaidia Wenyeviti wetu wa vijiji na vitongoji. Ni utaratibu mzuri, tuna imani mtakapouangalia mtawafikiria angalau na wenyewe waweze kuona kwamba kazi hii inafanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niungane na mwenzangu Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, kwenye maeneo ya uchimbaji wa madini hayo. Ukiona mwenzako ananyolewa na wewe utie maji. Mimi juzi tu yamejitokeza machimbo ya dhahabu kwenye eneo langu la Bugunda. Wananchi wamepata dhahabu pale, wameanza kuchimba

pale. Baadae wamekuja wataalam wanawaambia kwamba hili eneo tayari limeshachukuliwa na watu wengine, kwa hiyo, hakuna kuchimba tena hapo na limeshazuiwa mpaka sasa hivi na wala hakuna fidia yoyote iliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi utaratibu ukoje? Hao wenyewe wamejitafutia wakagundua hapa kuna dhahabu. Sasa hivi kuna walinzi wana mbwa, wana nini, hakuna mtu kuchimba pale. Jamani hivi huyu mchimbaji mdogo mdogo yeye ni wapi hasa atafika mahala achimbe kwa uhuru wake? Akigundua, anaambiwa hapa sasa ni mali yetu ya Serikali, mkae pembeni, tunaleta wawekezaji wengine kutoka nje, ninyi tafuteni mahala pengine. Wakipata mahala fulani, wanaambiwa hapa mhame, tena tunaleta kitu kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Buhunda wana matatizo makubwa sana. Walipata dhahabu nyingi tu, lakini lile likawa *fenced* na wakaambiwa kwaherini tutawatafutia eneo lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo. Ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kumbukeni tunajadili hotuba za utekelezaji wa Serikali katika mwaka wa fedha unaohusika. Sasa, tukianza kuomba hela za vijiji, za nani, mbona haimo kwenye taarifa ya hawa jamaa? Kwa hiyo, inakuwa ni *budget session* sasa. Hapa tunazungumzia utekelezaji. Kwa hiyo, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia taarifa mbili ambazo zimetolewa mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitauelekeza kwa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali na mchango wangu hautakuwa mrefu kwa sababu unazungumzia sekta moja tu, sekta ya madini ambayo wananchi wa Jimbo la Kahama na Wilaya ya Kahama wanahusika nayo kwa karibu sana. *(Makofi)*

Wilaya ya Kahama ni Wilaya ambayo imejaliwa kuwa na dhahabu nyingi, inapatikana karibu kila sehemu. Wilaya ya Kahama kuna Mgodi mkubwa wa Bulyanhulu na hivi karibuni kama sikosei tutakuwa na mgodi mwingine wa Buzwagi nje kidogo ya Mji wa Kahama na maeneo mengine mengi ambako wachimbaji wadogo wadogo wanachimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siyo mchumi lakini nina wasi wasi na taarifa ambazo zimekuwa zikitolewa na Serikali na vyombo mbalimbali kuhusu mchango wa sekta ya madini kwa Pato la Taifa, kwa maana ya kwamba sekta ya madini inachangia kwa takribani asilimia nne ya Pato la Taifa. Tafsiri yake ni kwamba wananchi wanaiona kule vijijini na wananchi wanaoishi hususan katika maeneo haya ambayo yanazalisha madini ya dhahabu au madini, wanaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Wilaya ya Kahama katika miaka ya karibuni wameilalamikia sana Serikali kwamba madini yanayotoka katika Wilaya hii hayawanufaishi kwa namna moja au nyingine. Taarifa ya Kamati inasema kuna pesa nyingi sana ambayo Serikali ilikuwa ipate, lakini pesa hiyo haijapatikana *either* kutokana na jamaa hawa kutokulipa kwa visingizio kwamba wamepata hasara na kadhalika. Mimi

naanza kupata wasiwasi, hivi biashara ambayo kila mwaka inapata hasara, ina uhalali kweli wa kuendelea ku-*survive*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uelewa wangu mdogo wa biashara, biashara ambayo kila mwaka inazalisha hasara, hiyo ni ya kufilisiwa tu au inafungwa kufanya kazi zake. Lakini makampuni hayo bado yanaendelea kuchimba na bado mwananchi wa kawaida pale Kahama anaona malori kila siku yanapeleka mchanga kwenda Isaka. *(Makofi)*

Mimi ombi langu na ndio maana nimesimama hapa, sheria hii ya madini iletwe hapa Bungeni, irekebishwe haraka iwezekanavyo. Visingizio vyote hivi vinavyotolewa ni kutokana na jinsi sheria ilivyo. Ukimuuliza mwananchi wa Kahama leo, hii Bulyanhulu imeleta manufaa gani kwa wananchi wa Wilaya hii na kwa bahati mbaya unapokuwa Mbunge, unakuwa jalala la kila aina ya maswali. Watakujibu watakwambia, mgodi huu haujaleta manufaa yoyote kwetu sisi, badala yake imekuwa ni kero. Wananchi katika maeneo ambako kuna migodi, kuna vitalu vya kufanya utafiti, wamezuiwa kufanya shughuli zao za kawaida za kilimo na kadhalika. Lakini bado Serikali hiyo hiyo, kila siku inakuja na mchango mpya, sekondari, zahanati. Wachimbaji hawa ukiwaomba pesa wasaidie walau vijiji vinavyozunguka maeneo haya, hawana pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili ni kubwa. Wananchi wanaoishi katika maeneo ya migodi ni binadamu kama binadamu wengine wowote na wana hisia sawa sawa na binadamu wengine. Tatizo hili likiachwa liendelee, tutapata matatizo makubwa miaka inayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo narudia tena, sheria hii ya madini iletwe haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza kuhusu hali ya maisha katika maeneo ya migodi. Ukitazama barabara ya kutoka Kakola kwenda Kahama Mjini ambayo miaka 15 kabla ya mgodi wa Bulyanhulu haujaanza kufanya kazi pale, ulikuwa unaweza kuchukua safari ya nusu saa. Leo hii, kama una bahati ni saa nne au tano kwa sababu barabara zimeharibiwa na malori haya makubwa yanayopeleka mchanga Isaka. Halmashauri ya Wilaya haina uwezo, hata hizo shilingi milioni 200 walizozitoa, haziwezi kuifanyia matengenezo hiyo barabara ya kutoka Kakola mpaka Kahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio hiki tunakitoa kila mwaka. Katika bajeti iliyopita, tumezungumza hapa Bungeni. Sasa mwananchi wa kawaida atakuelewa nini kuhusu sekta hii ya madini kwamba sekta hii ni muhimu, inachangia katika Pato la Taifa kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi! Tunapata matatizo makubwa kuwaelimisha wananchi waielewe falsafa kwamba maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana. Kule Kahama hawaelewi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilisema sitakuwa na mengi ya kuzungumza kwa sababu nilitaka kuchangia katika sekta hii ya madini ambayo kwa kweli inawagusa sana wananchi wa Jimbo la Kahama na niliona siyo busara nikakaa kimya. Kwa hiyo, naomba niishie hapo niombe tu kwamba Serikali isikie kilio hiki. Nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru kwa kunikopesha muda, maana yake hautoshi. *(Makofi)*

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia nami katika hoja zilizoko mbele yetu. *(Makofi)*

Kwanza kabisa kwa niaba ya wapigakura na wananchi wa Jimbo langu la Magu, naomba kama wenzangu waliotangulia, nitoe rambirambi kwa ndugu yetu Mheshimiwa Juma Akukweti, aliyetangulia mbele za haki. Bwana alitoa na Bwana ametwaa, mapenzi yake yatimizwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa za Uwaziri hivi karibuni, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Gaudence Kayombo. Nawatakia kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nizungumze masuala matatu ya kibajeti, kama taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali ukurasa wa 31, kuna taarifa kwamba asilimia 55 ya fedha za maendeleo hazikupatikana ama hazikukusanywa. Hii ina maana kwamba miradi iliyopangwa kutekelezwa, haikutekelezwa. Ukichukulia mfano wa bajeti ya mwaka huu 2006/2007, asilimia 36 ya bajeti ni bajeti ya maendeleo na asilimia 64 ni matumizi ya kawaida.

Kwa hiyo, naamini mwaka 2003/2004 kiasi ambacho kilikwenda kwenye maendeleo kilikuwa kidogo zaidi. Kwa hiyo, ukichukulia hii asilimia 36 ya mwaka huu wa fedha, uki-*assume* kwamba asilimia 54 ya fedha za maendeleo hazikutolewa, ina maana zilizopatikana ni asilimia 18 na hali hiyo inafanya asilimia zaidi ya 80 zilikwenda kwenye matumizi ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaashiria kwamba fedha nyingi za Serikali zilikwenda kwenye matumizi ya kawaida zaidi kuliko maendeleo. Nafikiri hii hali siyo nzuri sana kwa sababau tutaonekana tunakuwa Taifa la watumiaji kuliko la maendeleo. Kama Taifa hatu-*invest,* kunakuwa hakuna *Public Investment*. Kwa hiyo, *in the long run,* unakuta tunakula zaidi kuliko kuwekeza. Hali hii siyo nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 34 wa Taarifa ya *PAC* kuna taarifa kwamba zilikusanywa shilingi bilioni 68 kwa ajili ya *Road Fund,* lakini bilioni tano zilibaki Hazina, hazikupelekwa Wizara ya Ujenzi na wala hazikupelekwa Halmashauri kwa ajili ya kujenga barabara. Sheria inasema kwamba zinakusanywa tu na Serikali kwa ajili ya Mfuko wa Barabara. Bilioni tano zingeenda vijijini, zingeenda Jimbo la Magu kutengeneza barabara, nafikiri zingefanya kazi kubwa zaidi na naamini hata zingeenda Karagwe, pia zingefanya kazi kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ingekuwa vizuri Serikali ikazingatia sheria kwa maana kwamba *Road Fund* wanahitaji fedha kwa ajili ya kuboresha barabara hasa za vijijini. Naomba suala hili lisijirudie, fedha zinazokusanywa na Hazina kwa ajili ya kupelekwa kwenye maeneo mbalimbali, zipelekwe kama sheria inavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya mwaka huu inasema asilimia 66 ya fedha zote zinabaki Wizarani na asilimia 23 ndio zinaenda kwenye Halmashauri, asilimia mbili zinakwenda kwenye Mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha asilimia 66 za fedha kubaki Wizarani inaashiria mambo mawili, aidha, Halmashauri hazijapata uwezo wa kutumia fedha ndiyo maana zinapata asilimia 23 peke yake na hali hii inaonyesha kwamba kuna haja kubwa ya kujenga uwezo kwa Halmashsuri ili fedha zitoke Wizarani ziende Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza miradi ambayo Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kwamba barabara za vijijini zinapata fedha kidogo kidogo sana, zinapata matone matone kwa sababu fedha nyingi zinabaki Wizarani. Naomba fedha nyingi ziende kwenye Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze sasa kwenye masuala mawili ya kiuchumi, la kwanza ni kushuka kwa thamani ya shilingi na uhusianao wake na fedha zinazopatikana kwenye *export* ya madini. Kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania, athari zake kwenye bajeti ni kwamba shilingi inapoporomoka thamani yake kwa haraka ni kwamba bajeti ya nchi inaporomoka kwa sababau fedha ambazo zilikuwa zinakwenda kulipa deni la Taifa inabidi ziongezeke kwa fedha za ndani na pia mfumuko wa bei unaathiri bajeti ya Taifa kiasi kwamba inafikia sasa baadhi ya wafanyabiashara na hata makandarasi wana-*quote prices* zao kwa dola. *(Makofi)*

Hili suala la *dolasation* ya uchumi ni suala siyo zuri sana kwa maana ya kwamba *legal tender* yaani fedha halali ya Tanzania imegeuzwa kwenye baadhi ya sekta kuwa ni dola na hii imegeuzwa kwenye baadhi ya sekta kuwa ni dola na hii inatokana na ukweli kwamba shilingi inashuka thamani yake kiasi kwamba baadhi ya wafanyabiashara wanakuwa hawana imani tena na shilingi kwamba inashuka thamani haraka. Naomba Benki Kuu na Serikali wachukue hatua za haraka ili ku-*arrest* kuporomoka kwa thamani ya shilingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho hakieleweki sana ni kwa nini thamani ya shilingi inaporomoka kiasi hicho wakati dhahabu ambayo thamani yake haitegemei dola ya Kimarekani inaongezeka na tunapata asilimia 40 ya mapato yetu ya nje kutokana na madini. Ningependa kufahamu Serikali inachukua hatua gani ya kuyafanya madini yaweze kuchangia katika ku-*stabilize value* ya shilingi ya Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza sana Mkaguzi Alex Stuart na naipongeza Serikali kwa kuchukua uamuzi wa kumteua huyu Mkaguzi ili aweze kutufungua macho ya nini kinaendelea katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa katika ripoti ya *PAC* kwamba makampuni hayaweki fedha kwa ajili ya mazingira mara migodi hiyo itakapofungwa. Lakini hii inatokana na udhaifu wa Serikali kutokufuatilia na kuhakikikisha kwamba hawa wanaweka hizi fedha. Inakadiriwa kwamba hivi sasa bilioni 50 za Kitanzania zingekuwa zimewekwa kwenye akaunti. Kwa sababu hakuna akaunti yoyote iliyofunguliwa kwa ajili ya hii, naomba Serikali ilichukulie hili suala kwa unyeti wake ili fedha hizi ziweze kutolewa kwa wenye migodi ili ziweze kuwa *standby* kwa ajili ya kufanya *environmental decapitation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hasara iliyotajwa inasemekana kama trilioni 1.38 hii ni karibu asilimia 25 ya bajeti ya mwaka huu. Sasa hasara hii haikuwa *justified* na hii inatupunguzia uwezo wetu kama Taifa wa kufanya shughuli zetu za maendeleo. Naamini kwamba fedha hizi zingepatikana tungeweza kufanya mambo mengi kwenye Taifa letu na hatimaye kupambana na tatizo kubwa la huduma za jamii, la miundombinu ambalo linatukabili katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi najiuliza miaka 20 ijayo wengine hatutakuwepo hapa duniani kwa kuwa tutakuwa tumetangulia mbele za haki. Lakini watoto wetu, wajukuu wetu watakumbukaje kwamba Tanzania ilikuwa na madini mengi sana ikiwemo? Watakumbukaje kuwa nchi iliyo na madini ya kiasi hicho? Hii ni *windfall gain* ambayo kwa hali yoyote tungeitumia ili hapo baadaye tuje tukumbuke nchi hii ilikuwa na dhahabu, tusije kukumbuka kwa wingi na ukubwa wa mashimo ambayo yatakuwa yameachwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa napendekeza kwamba tungekuwa na utaratibu wa kutengeneza vitu ambavyo tutavikumbuka miaka ijayo kwamba tulikuwa na dhahabu kwa mfano, kila Wilaya ikachagua barabara moja ikawekewa lami hata Mbinga wakawekewe wasiokuwa na lami, hata Makete wakawekewe lami ya dhahabu tukawa na hospitali kule Lindi moja ikaitwa *Gold Hospital* maalum kabisa kwa ajili ya kukumbuka kwamba tulikuwa na dhahabu. Habari ya kuweka hela zote zinazotoka kwenye dhahabu kwenye kapu, zinazotoka kwenye msamaha wa kodi, kwenye kapu, sasa *at the end of the day* hatuwezi kujua na kukumbuka kwamba tulikuwa na dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu kwa leo niishie hapo nikiamini kwamba Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha na Benki Kuu na Serikali kwa ujumla watajipanga vizuri baada ya kilio cha Wabunge kwamba madini hayatufaidishi kama nchi na kwamba tuna matatizo mengi na maisha bora ambayo yameaihidiwa itakuwa ndoto kupatikana kama hatutakuwa makini kudhibiti *windfall* ama kitu ambacho Mwenyezi Mungu ametuletea madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana dada yangu kwa kunipa nafasi hii, ili na mimi niweze kutoa mchango wangu. Awali ya yote napenda nichukue nafasi ya kwanza, kutoa rambirambi zangu kwa kifo cha marehemu Juma Akukweti, kifo ambacho kilinitia majonzi makubwa sana nikikumbuka kwamba Mheshimiwa Akukweti aliongea mara ya mwisho Bungeni akijibu swali langu. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi pamoja na marehemu wote waliokuwepo kwenye ajali hiyo. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie nafasi hii kumpongeza dada yangu Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kwa madaraka makubwa aliyoyapata, madaraka ambayo yametupa heshima sisi akinamama, wamelipa heshima Taifa letu la Tanzania, Afrika na ulimwengu kwa ujumla. Mwenyezi Mungu amtie nguvu, amuongoze ili aifanye kazi yake vizuri zaidi ili tuendelee kupata sifa Watanzania. *(Makofi)*

Vile vile nitumie nafasi hii, kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri waliopata nafasi za Uwaziri, nikianza na ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, ndugu yangu Mheshimiwa Bernard Memba, Naibu Mawaziri Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Gaudence Kayombo. Mungu awatangulie katika nafasi zao ili waweze kuitumikia nchi yetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi sasa nijikite katika hoja iliyo mbele yetu Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali. Nikianza na suala la majengo ya Serikali, mimi niko kwenye Kamati ya *LAAC* na tumefanya ziara mbalimbali kuangalia *value for money*. Ni ukweli usiojificha kazi inayofanywa huko kwenye Halmashauri zetu za kusimamia majengo ya Serikali yakiwemo madarasa, zahanati, hospitali zetu na majengo mbalimbali haziridhishi. Kuna majengo tumeyakuta wakati tuko katika Mkoa wa Tanga Wilaya ya Pangani ukigusa ukuta tofali zinamomonyoka. Ni wazi kwamba ufyatuaji wa matofali umetumika mfuko mmoja labda tafoli 60 au 50 kitu ambacho siyo kiwango cha Serikali. *(Makofi)*

Naomba sana Serikali iwahimize watendaji wetu wahakikishe wanafuata taratibu na viwango vinavyostahili ili majengo yetu yaweze kudumu. Bila kufanya hivyo tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika mabati, ziko Halmashauri zinazotumia mabati kinyume cha taratibu za Seriakali. Serikali imeagiza *gage* 28 lakini unakuta Halmashauri imenunua *gage* 30 Serikali inatazama. Naomba haya mambo ambayo yanachelewesha maendeleo yetu, yanatoa sura tofauti ya viwango vya majengo tunayotarajia kwamba yatadumu katika nchi yetu kwa kipindi kirefu. Nitashukuru sana Serikali kama italitazama hili kwa makini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo naomba niongelee suala la kuhamisha akaunti. Ziko Halmashauri zimekuwa na taratibu ambazo ni kinyume cha Serikali, unakuta anachukua akaunti A anapeleka akaunti B. Anafanyia shughuli fedha za Serikali ambazo zililengwa kufanyiwa kazi nyingine, suala ambalo linapotosha kabisa taratibu za Serikali. Naomba Serikali mapungufu haya yatiliwe maanani Wakurugenzi wakemewe pale mnapoona kwamba wamekiuka taratibu ili tuweze kufanikiwa katika haraka yetu ya kusonga mbele kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka nizungumzie hili ni msiba kabisa, naamini kama tungekuwa tunapiga kura suala la Halmashauri kunyimwa ruzuku ya ziada Bunge lingepiga kura ya asilimia 100 ya Wabunge wangekataa suala hili.

Naomba Serikali isikie kilio cha Wabunge leo, ruzuku ya ziada ndiyo fedha pekee ambayo ilikuwa ni ukombozi kwenye Halmashauri zetu kuendesha miradi mbalimbali. Kuwanyima wananchi fedha za ruzuku ya ziada kwa madhaifu ya watendaji, kwa mambo ambayo hayakutekelezwa na Serikali ni kutokuwatendea haki. Halmashauri haziajiri, Serikali ndiyo inaajiri. Tunakuwa na makaimu, unakuta Kaimu Afisa wa Maendeleo ya Jamii, anakaimu miaka mitatu, Serikali inamtazama tu. Hivi huyu mtu kama ana sifa kwa nini msimthibitishe? Kama hana sifa kwa nini msimwondoe? Matokeo yake unakuja upembuzi wa kupata hati safi kigezo hicho kimoja tu kinafanya Halmashauri hiyo ikose ruzuku ya ziada. *(Makofi)*

Ninaamini hata Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama hili litakuwa limemkumba kwenye jimbo lake amelilaani. Hivyo, tushirikiane tu kulitazama hili upya liweze kujirekebisha, tutafute vigezo vingine siyo vigezo ambavyo havihusiani na Halmashauri zetu, hatuwatendei haki wananchi. Unamweka Mweka Hazina hana sifa kwa nini usimpeleke shule? Naomba sana Wabunge wenzangu humu wamelalamikia sana, tulitazame upya tena tulitazame kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine napenda niongelee kuhusu Wakurugenzi, kituo kukaa kituo cha kazi, hasa walioteuliwa juzi. Nashukuru sana Serikali imeteua Wakurugenzi wapya wengi tu katika hao wengi na wanawake nusu yao Mungu awabariki sana. Hili tumelipokea kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nashauri wako Wakurugenzi walioteuliwa kwenye vituo vyao walikuwa wako hapo hapo wakiwa wakuu wa Idara. Kuna Mkurugenzi labda alikuwa Afisa Mipango, kapewa cheo cha Ukurugenzi, unamwacha hapo hivi huyu tunamtendea haki kweli? Unajua aliishije na wenzake? Unajua alikuwa na uhasama kiasi gani? Unajua aliishije na Madiwani? Kumwacha hapo ni kumpa matatizo kwa sababu ataishi katika mazingira magumu, kwanza heshima anayostahili anaweza asiipate kwa sababu inawezekana kuna madhaifu ambayo, binadamu haishi kuwa na madhaifu huwezi jua. Anabaki pale pale, ninaomba wale tuwahamishe tuwabadilishie vituo. Tukiwabadilishia vituo tutakuwa tumesaidia sana ili kuweza kuwapima vizuri ili waweze kumudu nafasi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo wamesema sana na wenzangu kuhusu posho za Waheshimiwa Madiwani, hatuwatakii heri Waheshimiwa Madiwani, ndiyo kila wakati Madiwani ikifika miaka mitano amewekwa pembeni. Madiwani wetu wanakuwa na posho ndogo. Miradi yetu ya maendeleo ni ya kuchangia nguvu za wananchi na wewe kama kiongozi lazima uchangie. Hivyo na Madiwani wetu kwa nafasi zao lazima wachangie. Hivi hizo hela za kuchangia watazipata wapi? Waheshimiwa Madiwani, hata kufanya ziara tu ya kuzunguka kata yake ni taabu. Wako Madiwani hata baiskeli hawana. *Means* zozote za kutembelea kata hana, uwezo wa kusaidia yatima katika zao hawana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwatazame Waheshimiwa Madiwani, kwa jicho la huruma, tuhakikishe tunafika mahali tuwaongezee posho ili na wao wafike mahali wapate nguvu za kutumikia kata zao vizuri. Nina hakika dada yangu Waziri wa Fedha, hili amelisikia, nina hakika kabisa atalitazama kwa jicho zuri tu, si muda mrefu tutapata lugha nyingine juu ya Waheshimiwa Madiwani kwa suala la posho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongelee suala la elimu kwa Waheshimiwa Madiwani. Ni kweli Waheshimiwa wetu Madiwani walio wengi hawana uwezo hata wa kuhoja masuala ya Halmashauri, pamoja na semina mbalimbali mlizowapa bado haitoshi. Endeleeni kuwapa semina, endeleeni kuwapa warsha mbalimbali ili waweze kuwadhibiti watendaji wao vizuri. Mahesabu yanayoletwa mbele ya Kamati hayafanani kabisa mpaka unafikiria hivi haya yamepita mbele ya Baraza la Madiwani, lakini kweli yamepita hapo hapo. Kugundua mapungufu ni kazi sana. Inahitaji taaluma, tuwasaidie wenzetu ndiyo jukumu la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongelee suala la ujenzi wa barabara hasa hizi za vijijini na barabara za mitaa. Tunashukuru tunapata fedha kidogo kutoka *TANROADS* kwa maana ya mfuko wa *road toll,* lakini fedha hizo hazitoshi. Barabara nyingi za vijijini ni kero. Naiomba Serikali suala la barabara za vijijini, barabara za mitaa jukumu hili lichukuliwe na Serikali kwa 100% kama kweli tunataka kumkomboa Mtanzania. Watanzania vijijini wanatembea katika mazingira magumu, barabara ni matatizo. Kama barabara tu za Kitaifa ni tatizo itakuwa za vijijini? Naomba sana Serikali itazame mpango mpya kabisa wa kuhakikisha sasa suala la barabara linakuwa chini ya Serikali kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongelee suala la madawati. Kumbuka suala la madawati wananchi wanachangishwa, miaka mitatu iliyopita tulikuwa na njaa, mwaka jana, mwaka juzi njaa, hivi hawa wananchi tunaowachangisha kila leo hizo hela za kuchangia wanapata wapi? Serikali la madawati chukueni jukumu kwa asilimia 100 wananchi wetu hawana fedha, wanahangaikia riziki zao. Michango itakuwa ni mingi hawataweza kuimudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la wahisani, wahisani wetu tunashukuru wanatusaidia kuendesha miradi mbalimbali katika Halmashauri zetu. Lakini wahisani wanachagua maeneo ya kwenda. Kama wahisani wanakuja kwenye nchi yetu, naomba Serikali iwapokee na kuwapangia wao maeneo. Tuangalie vipaumbele, tusaidiane ni Halmashauri gani zenye dhiki zaidi? Ni wapi hawana maji? Ni wapi wana kero mbalimbali kuliko wao wajipangie. Utakuta Halmashauri moja ina miradi 25 unakuta Halmashauri ya Iramba ina miradi mitano, hivi kweli mnatutendea haki namna hii? Twendeni kwa uwiano. Waambieni shida zetu ni moja, mbili, tatu, leteni fedha sisi tutapanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee kuhusu watumishi wanaosoma, watumishi wanapata shida wanasoma kwa gharama zao. Serikali mmeagazi watumishi wajiendeleze na wenyewe wamekubali kwa asilimia 100 kusoma, sasa hivi kweli mshahara huo huo wa laki moja mtumishi ajisomeshe, atalipa kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali, iwasomeshe watumishi wetu ili waweze kwenda sambamba na azma ya Serikali ya kujiendeleza. Wako watumishi wengi wanasoma watendaji wa vijiji, watendaji wa kata, walimu, wauguzi na kada mbalimbali lakini wanasoma kwa mazingira, fedha hawana. Tunaomba tulitazame hili, Serikali ibebe mzigo huo kwa sababu hawa ni abiria yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie kuhusu hizi ruzuku ambazo Halmashauri zinaomba, zinatengeneza bajeti ya vile vyanzo vya mapato vilivyofutwa inapopeleka hazina, Halmashauri ya Manispaa ya Singida, imeomba shilingi milioni 800 inapewa shilingi milioni 200, hivi kweli Halmashauri hiyo itaweza kujiendesha?

Naomba jinsi Halmashauri zinavyoomba fedha nao muwalipe hivyo hivyo. Mnapowalipa fedha kinyume na maombi yao wanaendesha Halmashauri kwa mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongea hilo najua dada yangu, Waziri wa Fedha amelisikia. Sasa niongelee kuhusu watumishi wanaopanda vyeo, wanachelewa kurudishiwa *areas* zao na kubadilishiwa mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kama nilivyosema naomba tujadili utekelezaji, maana sasa mnajadili bajeti. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hizi zilizowasilishwa na Wenyeviti wa Kamati. Kabla ya kutoa mchango wangu nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya aliyekuwa Mbunge wa Tunduru, Mheshimiwa Juma Akukweti, naipa pole sana familia na zile familia nyingine zilizokumbwa na misiba katika ajali ya ndege iliyotokea kule Mbeya. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuwapongeza wale wote waliopata nafasi mpya ndani ya Bunge na hata nje ya nchi yetu. Ninawapa pongezi sana na ninawatakia kila la kheri kwenye kazi zao mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa mchango wangu ningependa kwanza niwaombe wale wote walioko kwenye Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, waliaminiwa na Watanzania waweze kutimiza wajibu wao na ili Watanzania waweze kuondokana na kero walizonazo. Ninasema hili kwa sababu baada ya kufanya ziara na kukagua vitabu vilivyoletwa mbele ya Kamati yetu ya *LAAC* tumeweze kugundua makosa mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nitakumbuka vizuri Mheshimiwa Rais, alisema wale wote ambao wanatuhumiwa ni wabadhilifu katika sehemu zao za kazi, hakuna haja ya kuwabadilisha vituo ni bora kuwapeleka kwenye mahakama na mahakama itaamua. Lakini hii tunayowabadilisha viongozi kuwatoa Halmshauri moja kuwapeleka kwenye Halmashauri nyingine, bado tunaendeleza tatizo linakuwa pale pale Watanzania wanakosa maendeleo kwa sababu ya wale wachache ambao wanashindwa kutimiza wajibu wao. *(Makofi)*

Kamati yetu ilijielekeza kwenye ukaguzi wa vitabu na kazi ya pili tuliyofanya ilikuwa ni kukagua miradi. Nilivyoviona katika vitabu kuna mapungufu mengi tuliyoyaona lakini kubwa wale viongozi wa Halmashauri, aidha, wanaandaa zile taarifa haraka bila kuzipitia na kuzileta mbele ya Kamati kwa sababu wanapofika mbele ya Kamati, unapouliza swali kutokana na vitabu vyao kwanza hawaelewi mradi uko wapi ndani ya kitabu chao, wakati kitabu wao ndiyo wamekiandaa. Hii inaonyesha mapungufu makubwa kwa watendaji wetu wa Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vitabu pia tuligundua miradi mingi ambayo haikutekelezeka baada ya kuzunguka kwenye ziara za kukagua miradi. Pia wanakuja mbele ya Kamati, wakijua kwamba tutakagua tu vitabu na hatukwenda eneo la miradi kukagua. Baada ya kufanya ziara kwenye miradi tumegundua miradi ambayo walituambia kwa taabu imekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mikoa tuliyozungukia katika Mkoa wa Tanga, kuna mradi wa maji wa uvunaji wa mvua walituandikia kwenye kitabu kwamba mradi huu umekamilika. Lakini tulipofika Tanga mradi huu haukuwepo, tulichokikuta ni kisima cha ujenzi wakati walipokuwa wanajenga Kituo cha Afya. Kwa hiyo, mradi wa uvunaji wa maji ya mvua haukuwepo na waliidanganya Kamati. *(Makofi)*

Mradi mwingine tulioutembelea ulikuwa ni mradi wa shamba la mikorosho. Mradi huu nao haukuwepo, baada ya kufika na kubadilisha ile ratiba ya miradi waliyokuwa wametupangia nahisi walikimbia kutafuta mkulima mwenye shamba la mikorosho na wakaipeleka Kamati kutembelea shamba hilo. Hilo shamba halikuwa na chochote. Hii inavyoonyesha jinsi Kamati za Bunge tunavyodanganywa na watendaji kutuletea taarifa za uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati yetu ilitembelea Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Kigoma, tulitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, katika mradi wa elimu niwapongeze kwamba wameweza kujenga shule nyingi za Sekondari na *primary*. Lakini tatizo miradi hii wameitelekeza, haikukamilika wameiacha kwenye vichaka na kutokana na mvua zinazoonyesha majani na miti mingi imeota, hutaamini kama mnapopelekwa kuna shule. Hivyo tungeitaka ile Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma waweze kumalizia miradi wanayoianzisha.

Pia tulitembelea mradi maji Kalenge. Halmashauri hii ilipofika mbele ya Kamati yetu walituambia kwamba chanzo cha maji kilitafutwa na Halmashauri hiyo. Lakini baada ya kuongea na wananchi tuliowakuta katika eneo lile la mradi walisema mradi ule ulitafutwa na Kanisa. Kwa hiyo, Halmashauri hii pia ilidanganya Kamati kwamba ilitoa fedha kwa ajili ya kutafuta chanzo kile wakati si kweli, chanzo kimetafutwa na Kanisa. *(Makofi)*

Pia napenda kuipongeza Kanisa lililoweza kuwasaidia wananchi wa Halmashauri ya Kigoma, kupata maji hayo. Hawa ni wale watendaji ambao wanashindwa kutekeleza wajibu wao. Pia tulitembelea mradi wa Maji Kazolamimba hapa tulikuta kuna tatizo kulikuwa kuna mradi wa maji lakini mradi wa kwanza wa maji *engineer* alituambia walifanya utafiti hawakuweza kupata maji walitumia shilingi milioni mbili. Lakini kabla ule mradi wataalam hawajasema kama maji yatapatikana, *engineer* yule aliweze kutumia zaidi ya shilingi milioni 156 kununua vifaa ambapo chanzo chenyewe kile hakijagundulika kama kinaweza kutoa maji. Taarifa zilizopoletwa walisema chanzo kile ni kidogo na vifaa vilivyonunuliwa katika mradi ule haviwezi kutumika. Hii inaonyesha watalaam wetu jinsi wanavyoshindwa kuzitumia fedha zinazotolewa na wananchi wa Tanzania kuleta maendeleo katika Wilaya zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuliweze kutembelea Mkoa wa Tabora, niwapongeze Wabunge wa Tabora wamejenga shule nzuri, lakini tulikuta tatizo moja katika shule ya *day* ya Urambo, watalaam wa Halmashauri hiyo badala ya kupeleka fedha katika shule wao walikuwa wananunua vifaa na kuvipeleka shuleni. Hii ilishindwa kutunza kumbukumbu kwa mwalimu mkuu wa shule kwamba ni kiasi gani kimetolewa na Halmashauri. Hii inaonyesha kwamba hapa kuna ubadhirifu, wananunua vitu hawataki kupeleka mahesabu sahihi kwa shule husika. *(Makofi)*

Vile vile tulikuta tatizo lingine katika Hospitali ya Wilaya ya Urambo, kulikuwa kuna ujenzi wa *Mortuary,* katika kitabu chao walicholeta mbele ya Kamati yetu waliandika mradi huu umekamilika. Lakini baada ya kutembelea mradi huo mradi haujakamilika na mkandarasi hawajui aliko na fedha zimekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuona hayo Mwenyekiti wetu alitoa maelekezo kwamba *engineer* huyo atafutwe ili ile kazi amalizie mkandarasi huyu na itafutwe fedha ya kumalizia mradi huo kwa sababu hospitali ile haina *mortuary*.

Baada ya Urambo pia tulitembelea Mpanda. Huko nako katika Hospitali ya Mpanda kwenye Jimbo la Mheshimiwa anayehusika na Wizara hii tulikuta kuna ubadhirifu wa kutisha. Katika hospitali hiyo, kuna vitanda vya akinamama vya *Labour,* waliandika vilinunuliwa shilingi 665,000 katika vituo vingine vitanda hivyo vilinunuliwa kwa 345,000 kama niko sahihi. Tulipombana na Daktari wa Hospitali, ile alituambia kwamba ile taarifa hakuandaa yeye iliandaliwa na mwenzie yeye alikuwa masomoni. Tukamwuliza unakubalije kusoma taarifa ambayo hukuandaa wewe, sisi tunayemjua ni wewe uliyekuja kusoma mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii tunaomba Wizara inayohusika, hawa watu waweze kuchukuliwa hatua kwa taarifa ambazo wanazileta mbele ya Kamati ambazo hazina usahihi. Pia kulikuwa kuna makabati 20 lakini makabati tuliyoyakuta pale ni makabati 10 na bei waliyoiandika baada ya kufika pale Daktari, alituambia kwamba bei walikosea ilikuwa ni *typing error* bei halisi waliambia ilikuwa ni shilingi 200,000. Hii inaonyesha kabisa kwamba watendaji wetu wengi wanatumia fedha za wananchi vibaya na ndiyo maana wananchi wanashindwa kujitoa kwenye zile kero ambazo kama watendaji wangesimamia vizuri wangeweza kuachana na hizo kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tulitembelea Halmashauri ya Sumbawanga Mjini. Hapa tulikuta jengo la Manispaa ambalo limekwisha kutumia fedha nyingi sana lakini limeshindwa kumalizika. Halmashauri inasema haina fedha ya kuweza kumalizia jengo lile. Naomba Wizara inayohusika basi iweze kuingilia kati jengo lile liweze kumalizika ili wenzetu wa Sumbawanga waweze kupata ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine ambayo tulishindwa kuitembelea kwa sababu ya mvua ilikuwa ni miradi ya barabara na katika mikoa tuliyokwenda Tabora, Kigoma na Rukwa barabara zilikuwa zimeharibika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikutana na matatizo makubwa njiani, magari yalikuwa yanakwama. Lakini kwa bahati nzuri msafara wetu tulikuwa tuna *four wheel*. Tulikutana na wananchi waliokuwa wamekwama kwenye mabasi na walikuwa wana hasira baada ya kugundua kuwa sisi ni Wabunge na ninaelewa kwa nini walikuwa na hasira hizo. Wana haki ya kuwa na hasira, kwa sababu wengi tuliwakuta akinamama wako kwenye gari na watoto, watoto wengi walikuwa wamefungua shule, wanarudi shuleni. Wamekwama hawana msaada wowote. Wengi walisema nyie ni Wabunge, hampati adha hii kwa sababu mpo kwenye *four wheel* hamkwami.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi ile Wizara inayohusika katika ile Mikoa niliyoona kwa macho, Tabora, Rukwa na Kigoma waweze kuwasaidia ndugu zetu wanaotoka huko kwa kweli wana hali mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naomba kuunga hoja mkono. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nilikuwa nimekataa kama nitapata nafasi ya kuchangia. Nashukuru sana kwa kunipa hii nafasi ya mwisho ili niweze kuchangia katika hoja zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nijumuike na wenzangu kutoa pole na rambirambi kwa familia ya marehemu ndugu yetu Mheshimiwa Juma Akukweti, pamoja na wafiwa wengine katika ajali hiyo.

Lakini vile vile niungane na wenzangu kuwapongeza Wabunge wenzetu ambao wamepata nafasi za kuchaguliwa kuwa Naibu Mawaziri na wengine kuwa Mawaziri. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo sasa kwa sababu muda wangu ni mfupi sana basi nijielekeze katika kuchangia hizi hoja. Hoja zangu zimekuwa fupi sana baada ya Wajumbe wengi kuwa wamechangia sehemu ambazo nilikuwa nimezipanga kuzichangia.

Lakini ninazo sehemu kuu mbili muhimu sana. Moja, kwamba wakati Kamati hii ya Serikali za Mitaa ikizunguka iliweza kutembelea miradi mbalimbali ikiwepo miradi ya kilimo. Nimeona jinsi ilivyofika kule *Kimila Irrigation Scheme, Shilanoma Irrigation Scheme* jinsi ambavyo haikuweza kutekelezwa kulingana na mikataba ilivyokuwa imewekwa. Lakini mimi hapa nataka kuchangia kitu kimoja kwamba kuna tatizo moja ambalo linajitokeza katika utengaji wa fedha. Kuna vigezo ambavyo vinatumika kutenga fedha za *OC* ambavyo vigezo hivi vimekuwa ni vile vile kwa muda mrefu sana ambapo wakati sasa umefika kwa wanaohusika kuangalia vigezo hivi hawazi-*counter check* kuziona kama zinaendana na wakati wa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *OC* ambao ni *Other Charges* ambazo ndiyo fedha ambazo zinawawezesha Watendaji katika Halmashauri zetu kuweza kutekeleza majukumu yao. Ninao mfano mzuri sana wa vigezo hivi kwamba wale wataalam wetu wa vigezo wameviseti, hawaviangalii, wamekariri tu kwamba sisi tulishaweka vigezo basi hatuna muda tena mwingine wa kuzipitia. Kwa hiyo, unakuta kwamba fedha ambazo zinatengwa ni fedha ndogo sana ambazo haziwezi kukidhi mahitaji ya Wilaya ile. Mfano, katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Meatu katika sekta ya kilimo na mifugo, fedha ambazo zimetengwa kwenye *OC* kwa ajili ya mifugo ni milioni nne tu. Wilaya nzima, fedha kwenye kilimo, *OC* ya kilimo ni shilingi milioni 9.8. Fedha yote ya Wilaya nzima, kwa hiyo, Wilaya nzima katika sekta ya mifugo na kilimo imetengewa shilingi milioni 14 tu. Sasa shilingi milioni 14 unatekeleza kipi katika kipindi hiki ambacho Wizara hii tumeielekezea nguvu zote. Tumetenga fedha nyingi sana kuzipeleka kwenye Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Tuna hiyo *DADPs,* tuna *DAZP,* tuna *ASDP,* sasa mimi nina shilingi milioni 14 tu. Ukiuliza kwa nini Wilaya ya Meatu inatengewa milioni 14 katika bajeti yake unaambiwa kwamba Wizara inazingatia vigezo. Lakini sasa vigezo hivi vinakuwa vya namna gani. Kwa sababu Wilaya ya Meatu ambayo ni kubwa kabisa yenye Kata 19, yenye majimbo mawili inatengewa milioni 14 kwenye Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Lakini

tatizo ambalo najifunza ni kwamba wale wanaopitia vigezo hawaviangalii vigezo vyao sawasawa. Kwa sababu....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, jadili utekelezaji wa Serikali na siyo bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kupingana na wewe, lakini haya ni baadhi ya mambo ambayo yamejitokeza kuwa matatizo katika bajeti, katika utekelezaji wa shughuli hizi za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hayo kwa uchungu kwa sababu shughuli katika Wilaya yangu upande wa Kilimo na Mifugo hazitaweza kwenda. Katika Manispaa, Wilaya hiyo hiyo ya Meatu Mkoa huo wa Shinyanga ukienda Manispaa ya Shinyanga wametengewa shilingi milioni 41, pale mjini Shinyanga kwenye Kata 10 tu. Lakini kule kilimo kinafanyika kila kitu kinafanyika, hivi vigezo vinatofautiana kwa kiasi hicho kwa vipi. Kwa hiyo, ombi langu tu ni kwamba hawa wanaoangalia vigezo hivi waviangalie upya, Wilaya ya Meatu inahitaji iongezewe fedha kwa ajili ya *OC* ya Kilimo, milioni 14 hazitoshi, tumeandika barua nyingi sana kwa ajili ya kuongezewa fedha hizo. Tumeandika barua tukiomba kwamba walau tuongezewe shilingi milioni 26 kwa ajili ya kukamilisha shughuli zetu za Idara ya Kilimo. Pamoja na kukuudhi kwa kusema hayo, lakini ni muhimu niyaseme. *(Makofi/Kicheko)*

Kuna suala lingine ambalo limo kwenye taarifa hii ya Serikali, Halmashauri za Wilaya ya Meatu hasa mradi huu wa maji ambao Kamati ilipokuja kutembelea Wilaya ya Meatu mimi nilikuwepo na nilitembea nao mpaka tukaenda kwenye mradi ule. Mradi huu tulipata ufadhili wa Uholanzi kupitia mradi wa *RWSSP* jumla ya shilingi bilioni 2.3 ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huo na mkandarasi *Wenson Tanzania Limited* tukawa tumempata kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana mkandarasi huyu kwa sababu kazi zake amefanya vizuri kwa kweli. Fedha zote zilizokuwa zimetengwa na Serikali ambazo zimeletwa pale jumla ya shilingi bilioni 2.1 zimeshafanya kazi. Mradi ule sasa hivi umefikia asilimia 85 ya utekelezaji. Mpaka sasa hivi kuanzia mwaka jana fedha zimepungua kutoka Ubalozi wa Uholanzi haziletwi tena kwa sababu Waholanzi wamesema kwamba sisi bwana tumefikia hapa sasa hatuna fedha, jumla ya shilingi bilioni 2.1 zimeshaletwa lakini kuanzia hapo hatuna fedha tena kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Halmashauri pamoja na Wizara muone ni namna gani mnautekeleza mradi huu. Nayo hii tumeandika barua nyingi sana kumwandikia Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji kuhusu utekeelezaji wa mradi huu wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha nyingi sana za mwekezaji zimewekwa pale shilingi bilioni 2.1 ametoa kusaidia Wilaya yetu, kusaidia wananchi wa Wilaya ya Meatu wenye tatizo kubwa la maji. Lakini mpaka sasa hivi Wizara mradi ule umeonekana sasa umekuwa na upungufu wa fedha kama zilivyotajwa hapa na Kamati ni jumla ya shilingi milioni 651.5. Lakini kwa nini fedha zimepelea? Fedha zimepelea kwa sababu hasa ya *variations* ambazo zilijitokeza katika utekelezaji. Jumla tu ya *variation* ambazo zilijitokeza thamani yake ni shilingi milioni 147.9. Lakini kuna kazi zingine ambazo hazijaweza kutekelezwa jumla yake ni shilingi milioni 252.5. Tuna fedha za kumlipa *Consultant* shilingi milioni 37. Kuna fedha za *retantion* shilingi milioni 213.5. Lakini

sasa tulikuwa tunaomba walau sasa hizi shilingi milioni 400 hizi za *retantion* zinaweza zikawa *allocated* hata kwa mwaka kesho. Lakini hizi za kukamilisha mradi huu, ili wananchi wa Wilaya ya Meatu waweze kupata maji, tunaziomba hizo tupate ili wananchi wa Wilaya ya Meatu waweze kutekeleza mradi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba tumeandika barua ya awali kutoka tarehe 15 Januari, 2007 barua ya pili tumeandika tarehe 2 Februari, 2007 zote hizo hatujapata majibu. Sijui ni sababu gani ambayo inapelekea tunakuwa na kigugumizi cha namna hii. Hata wale wafadhili ambao wanatufadhili miradi ya maendeleo watatucheka. Kama mtu anaweza kukufadhili shilingi bilioni 2.1 utekeleze mradi wako wewe leo hii shilingi milioni 400 imeshakuwa kigugumizi kuziruhusu kwenda kutekeleza mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi kama nilivyosema kwamba muda wangu umekuwa ni mfupi, lakini nimeona hayo ni muhimu sana niyazungumze na Waziri wa Maji anipe jibu la uhakika la fedha za kwenda kutekeleza mradi wa maji Meatu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namwona ndugu yangu Mpina hapa anasema, nimekasirika au nimeudhiwa kwa maneno yake. Hapana, iko hivi, tuna kipindi cha kujadili bajeti, ndiyo wakati wa kuomba na kuomboleza. *(Makofi)*

Sasa hapa tunafanya kuangalia Serikali, fedha zile tulizoomba na kuomboleza zimefanya kazi gani? Ndiyo kazi tunayoizungumza hapa. Sasa kama anavyosema Mheshimiwa Mpina, kama yale mabilioni ya Waholanzi yaliibiwa ndiyo maneno haya. Nani aliiba zile hela na mradi haukupatikana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ndiyo tunachokisema, kwa sababu tunajifunza pamoja basi ni vizuri tukazingatia, kwa sababu tutapata mantiki nzuri zaidi kuliko tena tuanze kuomba hela, wakati wa bajeti tutaomba pesa na hawawezi kukujibu, kwa sababu siyo Bajeti. Lakini unaweza kwenda kuomba mwenyewe kwa Mawaziri peke yako kwa namna yako.

Baada ya kusema hayo, ningependa mumtambue Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ambaye anafanya kazi na Kamati hizi Bwana Uttoh, naomba usimame. Ahsante sana. *(Makofi)*

Halafu napenda pia nitangaze kwamba baada ya kuahirisha kikao hiki sasa hivi, Kamati Ndogo ya Maandalizi ya Uzinduzi wa Mpango Mkakati wa *TWPG* wakutane baada ya kikao hiki kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Spika. Halafu kesho tutaendelea kidogo na orodha hii. Lakini tutakuwa na saa moja tu.

Kwa hiyo, orodha niliyonayo kuna Wabunge karibu kumi na ngapi waliobaki, tutawapata wanne tu. Kwa sababu hoja hizi lazima saa saba mchana ziwe zimeisha kwa maana ya kwamba tupate majibu kutoka kwa Mawaziri na watoa hoja waweze ku-*re act* kwa hiyo, tutakuwa na watu wanne tu asubuhi.

Kwa hiyo, wengi watabaki. Kwa sababu hizo hizo ile semina mliyoambiwa ingekuwepo siku ya Ijumaa, imeahirishwa mpaka Bunge la Aprili, 2007, sababu hizo hizo za kukosa

muda mpaka mwezi Aprili. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, sina lingine. Napenda kuahirisha Bunge hili mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 10.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 8 Februari, 2007 saa tatu asubuhi)*